

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tisa– Tarehe 28 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Thelathini na Tisa.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Michezo.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Na. 321

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa sababu Hospitali iliyopo haikidhi mahitaji kutokana na uchakavu na ongezeko la watu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu kwa watu wa Manyoni, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa hospitali 43 kongwe na chakavu za Halmashauri ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Serikali inaendelea kufanya tathmini ya miundombinu ya hospitali hizo ili kuona namna bora ya kuziboresha ikiwemo kuzikarabati au kujenga hospitali mpya kulingana na matokeo ya tathmini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kukamilisha kwanza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 28 na hivyo baada ya ujenzi huo kisha hospitali chakavu zitawekewa mpango.

**SPIKA:** Dkt. Chaya swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini sasa tathmini ya uchakavu wa miundombinu ya Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni itaenda kukamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hii hospitali ilianza mwaka 1973 na mwaka 1992 ilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya na kwa kuwa bado inaendelea kutoa huduma katika Wilaya ya Manyoni na kwa kuwa tuna upuungufu mkubwa sana wa wataalam katika hospitali na Jimbo zima la Manyoni Mashariki, nini *commitment* ya Serikali ya kupeleka wataalam katika Jimbo la Manyoni Mashariki? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaweka utaratibu wa kufanya tathmini katika hospitali zetu zote kongwe na chakavu 43 ambazo tumekwishazitambua ikiwemo hospitali hii ya Manyoni na kazi hiyo tayari imeanza na inaendelea. Tunatarajia ifikapo mwezi wa tatu mwaka ujao tutakuwa tumekamilisha na kufanya maamuzi wapi tutajenga hospitali mpya na wapi tutakwenda kuzikarabati zile hospitali ambazo bado zinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna changamoto ya upungufu wa watalaam katika huduma za afya katika vituo vyetu na Hospitali za Halmashauri ikiwemo Manyoni na Serikali imeendelea kuomba na kutoa vibali bvyaa ajira na katika mwaka huu wa fedha tumeomba vibali vya watumishi 12,000 lakini kipindi hiki tunaendelea na mchakato wa kuajiri watumishi 2,796 wa kada mbalimbali za afya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Manyoni pia itapewa kipaumbele cha kupata watumishi hawa wa afya.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Nashon Bidyanguze Mbunge wa Kigoma Kusini.

Na. 322

**Ujenzi wa Barabara Tatu Zinazounganisha  
Mkoa wa Kigoma**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara tatu za Lukoma – Lubalisi, Kalya – Ubanda na Kalya – Sibwesa zinazounganisha Mkoa wa Kigoma kupitia Wilaya ya Uvinza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa David Ernest Silinde - Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, asante sana; kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 barabara za Lukoma - Lubalisi, Kalya - Ubanda na Kalya - Sibwesa zilitambuliwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) na kuwekwa kwenye mfumo wa barabara zinazotambuliwa na *TARURA* (*DROMAS*). Barabara hizo

zitaingizwa kwenye mpango wa matengenezo ya barabara kupitia fedha za matengenezo ya barabara zinazotolewa kwa *TARURA* katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi pamoja na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji la Kuendeleza Kilimo – Kigoma (*SAKIRP*) inaendelea na ujenzi wa madaraja 10 kwa kutumia teknolojia ya mawe kwa gharama ya shilingi milioni 190 ambapo madaraja matatu yamekamilika likiwemo Daraja la Mto Ruega katika barabara ya Kalya – Ubanda lililojengwa kwa shilingi milioni 37 katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti zake ili kuzifanyia matengenezo barabara hizo kwa kadiri upatikanaji wa fedha utakavyoendelea kuimarika.

**SPIKA:** TAMISEMI nawapongezeni kwa majibu mafupi yanayo jielekeza moja kwa moja kwenye maswali, mnafanya vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri yaliyotolewa mbele hapa, lakini ninalo swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Kigoma Kusini linao urefu wa barabara hii ya Simbo kwenda Kalya ndio hiyo ambayo inazalisha hizo barabara tatu nilizozisema. Barabara ya Kalya kwenda Sibwesa inatoka nje ya nchi kwa sababu kuna bandari pale Sibwesa, lakini barabara hii pia ya Lubalisi inatoka nje ya mkoa na hii ya Kalya – Ubanda inatoka nje ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali iangalie kuweza kuipa kipa umbele barabara hizi kwa sababu zinaufungua mkoa kupitia Halmashauri ya Kigoma Kusini kwa maana ya Jimbo la Kigoma Kusini, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alichoomba ni kwamba Serikali tuizingatie ile barabara na mimi nipokee ombi lake kwa sababu tumeshakiri katika jibu letu la msingi kwamba moja hiyo barabara tumeitambua na kuiingiza katika mpango. Awali *TARURA* wakati inaanizishwa tulikuwa tulikabidhiwa barabara zenyet urefu wa kilometra 108,000; kwa hiyo sasa hivi kuna ongezeko la barabara karibu 36,000 mpya.

Mheshimiwa Spika, miiongoni mwa barabara hizo ambazo zimetambulika ni pamoja na hizi barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge umeziainisha. Kwa hiyo, kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha na tutakavyoendelea kuziweka katika mpango basi barabara hiyo tutaipa kipaumbele katika mwaka wa fedha unaokuja.

**SPIKA:** Ahsante, nimekuona Mheshimiwa Maimuna. Washa chombo.

**MHE. MAIMUNA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ingawa swali langu lilikuwa linaenda kwenye...

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba.

Na. 323

**Ujenzi wa Barabara Inayotoka Mtwara Mjini  
Kwenda Msimbati**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Mtwara Mjini kwenda Msimbati ambako kuna mitambo ya visima nya gesi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mtwara Mjini kuanzia Mangamba – Madimba – Msimbati inayokwenda kwenye visima nya gesi nya Mnazi Bay yenye urefu wa kilometra 35.63 na barabara ya Madimba – Kilambo inayokwenda kwenye Kivuko cha Kilambo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji yenye urefu wa kilometra 16.87 ni barabara za mkoa zinazosimamiwa na Wizara yangu. Barabara hizi zinafanyiwa matengenezo kila mwaka na Wakala wa Barabara nchini Tanzania (*TANROADS*) na zinapitika wakati wote. Katika mwaka wa fedha ujao wa 2021/2022 zimetengwa jumla ya shilingi milioni 231 kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hizi pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami. Ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hizi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, swali la nyongeza .

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante; pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kutokana na umuhimu wa barabara ya ulinzi inayozunguka maeneo ya mipaka yet una nchi Jirani ya Msumbiji, je, lini Serikali itaanza kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kurahisisha hata vyombo vyetu vya ulinzi vinapofanya doria vifike kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na uwepo wa miundombinu muhimu ya umeme na visima vya gesi, Vijiji vya Msimbati na Madimba. Je, Serikali halioni sasa ni wakati sahihi wa kuboresha miundombinu ya barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili kutoka kwa Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya ulinzi aliyoitaja ni barabara muhimu sana na ina urefu zaidi ya kilometra 350 na hadi sasa barabara hii baada ya kwamba ilitumika kipindi kile haitumiki na sasa hivi inafunguliwa upya na tayari na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imeshafungua karibu kilometra 250 na inaendelea kuifungua mpaka itakapokamilika. Na baada ya kukamilika kuifungua ndipo tutakapoanza utaratibu wa kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii aliyoisema ni lini tuaanza, tayari tumeshaanza ndio maana tumeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kilichobaki sasa ni kutafuta tu fedha na tutakapopata basi tuaanza kujenga kwa kiwango cha lami ili kufikia hayo maeneo muhimu ya Mnazi Bay, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa.

Na. 324

**Mradi wa Kuhifadhi Mazingira na Kufuga Samaki  
Ziwa Nyasa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Ludewa hutegemea Ziwa Nyasa kwa shughuli za uvuvi.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kupeleka mradi wa uhifadhi mazingira Ziwa Nyasa ili kutunza mazalia ya samaki ambao wameanza kuadimika?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha pamoja na wataalam kutoa elimu ya kuanzisha mradi wa ufugaji samaki kwenye vizimba ndani ya Ziwa Nyasa ili kuzalisha ajira kwa wananchi na kuongeza kipato?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kwa swali hilo, Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kutekeleza jukumu la kulinda, kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini imekuwa ikitoa elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira kote nchini ikiwemo Ziwa Nyasa. Aidha, kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuandaa mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya uvuvi ambao utakapokamilika unatarajiwa kubainisha miradi ya uvuvi

itakayotekelawa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji kwa kutumia teknolojia mbalimbali ikiwemo teknolojia ya vizimba, imetoa mafunzo ya vitendo kwa wananchi 1,885 kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki, kilimo cha mwani na uongezaji thamani zao la mwani.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepanga kutoa mafunzo kwa wakuzaaji viumbe maji wapatao 3,000 kote nchini wakiwemo wafugaji wa samaki Ziwa Nyasa kuititia Kituo cha Kuendeleza Ukuzaaji Viumbe Maji cha Ruhila – Songea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa, swali tafadhali.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ziwa Nyasa lina Kata zisizopungua nane; Kata ya Ruhuhu, Manda, Iwela, Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilondo na Ruhila. Je, ni lini Serikali inakusudia kupeleka vifaa vya uvuvi kama *engine* za maboti kwa vikundi vya wavuvi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningetamani kufahamu ni lini Serikali itapeleka kituo cha kufanya utafiti wa samaki na viumbe maji huko Wilayani Ludewa maana kata hizi zina wakazi wasiopungua 28,000 ambaao wanatumia ziwa hili kama *swimming pool* na njia tu ya usafiri. Ningependa kufahamu *commitment* ya Serikali juu ya kupeleka kituo cha utafiti wa samaki?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo mawili Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya kupatikana kwa vifaa vya uvubi katika makundi ya vijana kwenye Kata za Ruhuhu, Manda, Makonde na kwingineko katika Jimbo lake la Ludewa naomba nimhakikishie kwamba katika mwaka wa fedha huu ambao leo tunaendelea kujadili bajeti yake, Serikali imejipanga kuhakikisha vijana wote waliopo katika maeneo hayo na wenyewe wanaweza kuwezeshwa kupata vifaa vya kufanya shughuli zao za uvubi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kituo cha utafiti; Ziwa Nyasa ni katika maeneo ambayo Shirika letu la Utafiti la Uvubi (*TAFIRI*) litakwenda kufanya utafiti kule na uwezekano wa kuweza kupata kituo kidogo pale kwa ajili ya utafiti kwenye eneo la Ziwa Nyasa upo na naomba nichukue jambo hili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanya jitihada ya kuhakikisha kituo kinapatikana pale ili na Ziwa Nyasa wakati wote liwe linatazamwa na kuangaliwa kwa karibu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Mohammed nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; bado wavuvi wanalazimika kwenda mbali kwa ajili ya kutafuta samaki kutokana na changamoto mbalimbali za bahari na uhifadhi wa mazalia ya samaki, jambo ambalo linasababisha pia wavuvi hao muda mwingine wanapata ajali za baharini, wanapotea wenyewe pamoja na vyombo vyao.

Je, Serikali ina mkakati gani wa utoaji wa mafunzo kwa wavuvi hasa mafunzo ya uhifadhi wa mazalia ya samaki na hasa kwa wavuvi ambao wanatokea pande za Nungwi, Matemwe na sehemu zingine ambao wanatokea katika ukanda wa Zanzibar? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu, Waziri Mifugo na Uvuvi, bahati nzuri maeneo hayo ya bahari unayafahamu vizuri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu wa 2021/2022 kwenye mpango wetu tumeweka mkakati maalum, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pamoja tunao mpango madhubuti kwa kutumia mashirika yetu ya *Deep Sea Fishing Authority* (Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu), lakini vilevile kwa upande wa Tanzania Bara (*TAFIRI*) na kwa upande wa Zanzibar (*ZAFIRI*) tumesafanya *partial marine monitoring program* ambayo tumeainisha maeneo yetu ya mavuvi.

Mheshimiwa Spika, lengo letu tunataka tuwatoe wavuvi wetu kwenye kufanya uwindaji, sasa tunakwenda katika uvuvi wa kidigitali. Mvuvi kabla hajakwenda kuvua, kupitia vituo vyetu aidha Ofisi za Vijiji au *MBU* au kwingineko apate taarifa za mavuvi, wapi walipo samaki, umbali anaokwenda; kwa hiyo, tutakuwa na mfumo wa *GPS* utakaokuwa ukiwasaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba mfumo huu utawawezesha wavuvi wetu watumie gharama ndogo sana ya mafuta, lakini vilevile wasitumie muda mwingi wa kwenda kuwinda. Tunataka tutoke katika uvuvi wa kuwinda twende katika uvuvi wa uhakika zaidi, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu haya ya uhakika. Kwa sababu ya muda tuende na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum - Tabora.

Na. 325

### **Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Tabora na Singida**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi katika mikoa ya Tabora na Singida ili wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa utulivu na amani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kuhusu migogoro ya mipaka, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Angelina Mabula tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa imekuwepo migogoro ambayo kwa muda mrefu haikuwa imepatiwa ufumbuzi. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara iliajiza Ofisi zote za Ardhi za Mikoa nchini ikiwemo Singida na Tabora kuanzisha jedwali la migogoro ya ardhi ili kuibainisha na kuitatua. Kwa Mkoa wa Tabora, jumla ya migogoro 211 iliorodheshwa na katiba hiyo migogoro 102 ilipatiwa ufumbuzi. Aidha, kwa Mkoa wa Singida jumla ya migogoro 226 imetambuliwa na katiba hiyo migogoro 34 imetatuliwa na iliyobaki asilimia 85 inatokana na madai ya fidia ambayo wananchi wanadai Halmashauri na taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Wizara katika kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la migogoro ya ardhi nchini ni pamoja na kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kwa wananchi, kuzitaka taasisi za umma kulipa fidia kwa wananchi kwa wakati, kuendelea kutoa

elimu kwa umma, kushirikiana na Serikali za mitaa kudhibiti ujenzi kwenye miundombinu ya umma kama shule, viwanja vyatia michezo, maeneo ya wazi, Wizara za Kisekta kushughulikia kero za makundi mbalimbali ya watumiaji ardhi kama wafugaji na wakulima na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wadau wote hasa taasisi za umma ambazo zinadaiwa fidia na wananchi inayochangia asilimia 39 migogoro yote nchini kuacha kuchukua ardhi za wananchi bila kilipa fidia na taasisi zinazodaiwa fidia kulipa mara moja vinginevyo maeneo hayo yatarejeshwa kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa ameridhika.

Tunaendelea na swali linalofuata litaulizwa kwenda Wizara ya Maliasili na Utalii, muuliza swali ni Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi na kwa niaba yake Mheshimiwa Tadayo.

Na. 326

**Kuweka Upya Mipaka ya Hifadhi ya  
Taifa Mkomazi**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MHE. DKT. DAVID M.  
DAVID** aliuliza:-

Idadi ya watu wa Same imekuwa ikiongezeka tangu tupate Uhuru na mpaka wa Hifadhi ya Taifa Mkomazi upo kilometra tatu kutoka Same Mjini. Wanyamapori na hasa tembo wameonekana Same Mjini mara nyingi.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuweka upya mipaka mipyaa ya hifadhi ili kutoa maeneo kwa ajili ya makazi ya watu na shughuli nyingine za kijamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa utaona jibu lako refu tunapoenda Maliasili na ninyi punguzeni majibu.

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -**

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Hifadhi ya Taifa Mkomazi yapo eneo la Zange lilitopo umbali wa kilometra sita kutoka Same Mjini. Wanyamaporii hususan tembo wanaoonekana karibu na Mji wa Same mara nydingi ni wale wanaotoka katika maeneo ya Ruvu na Simanjiro kuelekea Hifadhi ya Taifa Mkomazi na wale wanaotoka katika Hifadhi ya Taifa *Tsavo West* nchini Kenya kupitia Ziwa Jipe na Kijiji cha Toloha katika Wilaya ya Same. Ikumbukwe pia kuwa maeneo mengi ambayo wananchi wanaishi kwa sasa yalikuwa yanatumiwa na wanyamaporii kama mapito (shoroba) kuelekea maeneo ya Ruvu na Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kumega eneo la hifadhi kwa kuweka mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa Mkomazi siyo suluhu ya mgogoro huo kwa sababu eneo hilo litaendelea kuwa makazi na mapito ya wanyamaporii. Hata hivyo, katika kudhibiti wanyamaporii hao, Serikali itaendelea kuimarisha mikakati inayotumika ambayo ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa wananchi ya mbinu za kukabiliana na wanyamaporii wakali na waharibifu ambapo mafunzo hayo yanaendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Pia kuimarisha, kuendeleza tafiti na kutumia mbinu mbalimbali za udhibiti na ufuatiliaji wa tembo. Mbinu hizo ni pamoja na mikanda ya elektroniki (*collaring*) kwa ajili ya kufuatilia makundi ya tembo ambayo ni korofi na kufundisha na kuviwezesha vikundi vya wananchi kwa ajili ya kufuatilia maeneo walipo tembo.

Mheshimiwa Spika, pia matumizi ya ndege zisizokuwa na rubani, matumizi ya pilipili, matumizi ya mizinga ya nyuki na matumizi ya vilipuzi na vifaa vyenye mwanga mkali; lakini

pia kutengeneza minara ya kuangalia mbali katika maeneo yanakabiliwa na changamoto ya tembo kuingia. La mwisho ni kuhamasisha wananchi kutoa taarifa mapema pindi wanyamapor ikiwemo tembo wanapoonekana kwenye maeneo ya makazi au mashamba.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa wananchi wote wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Mkomazi waendelee kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi iliyowekwa pamoja na kushirikiana na Serikali katika kutatua changamoto za wanyamapor ikiwemo tembo pindi zinapojitokeza katika maeneo ya makazi ya watu na shughuli nyingine za kijamii.

**SPIKA:** Kama nilivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri huko mbele muangalie majibu yenu yasiwe marefu sana. Swali ni lini tu mtafikiria upya kuiangalia mpaka ya Hifadhi ya Mkomazi.

Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na juhudzi za Wizara ambazo tunaziona, lakini kwa kuwa mpaka ya hifadhi hii iliwekwa mwaka 1954 na idadi ya watu imezidi kuongezeka kiasi kwamba sasa hivi Makao Makuu ya Mji Mdogo wa Same yapo kilometra nne tu kutoka kwenye mpaka wa hifadhi.

Je, Serikali haioni kwamba suala la eneo hili la Same Magharibi lichukuliwe kama *special case* ili kuwapa watu nafasi ya kuweza kufanya kazi zao kwa sababu mpaka upo karibu sana na Makao Makuu ya Mji Mdogo wa Same? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante, *actually* kilometra nne ni kutoka katikati ya Same hadi mpakani, lakini vimeshagusana Mji wa Same na mpaka *neck to neck*. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Malisili na Utalii naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Tadayo, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba Same ipo kilometra sita kutoka maeneo ya makazi ambayo wanaishi wananchi mpaka kwenye eneo la hifadhi. Kama ambavyo nimeelezea kwamba sasa hivi tuna changamoto ya tembo na hawa tembo wanarudi kwenye maeneo yao ya zamani, kwa hiyo, kuendelea kumega hili eneo ni kuendelea sasa kuongeza migogoro kati ya wananchi na wanyama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati Serikali inaangalia utaratibu mwininge basi wananchi waendelee kuishi kwenye maeneo hayo kuliko kuendelea kuwasogeza kwenye hatari zaidi kuliko ilivyo sasa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela nilikuona.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli wakazi wengi wa Same amba wanaishi karibu na *Mkomazi National Park* wapo kwenye *risk* kubwa ya kupata matatizo na kupoteza maisha yao. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri tulikuwa naye Jumamosi na Jumapili kule Same na ameona hali ilivyo, haoni kwamba ni vyema zile sehemu zote ambazo zina *risk* kubwa kukawepo askari amba wanakuwepo kuwafukuza wale tembo kuliko kuacha hali ilivyo mpaka sasa? (*Makofî*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo anasema sio pale Same tu hata ukienda Kisiwani, wapi wananchi ni palepale. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulienda ziara na Mheshimiwa Anne Kilango, changamoto ya tembo ipo, ni kweli na ni kubwa, lakini tulitoa maelekezo na naomba hili niendelee kuelekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba tutaweka kambi ambazo zitakuwa ni za doria kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaishi kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, na hili nikuahidi kwamba maeneo yote ambayo yana *risk* kubwa ya tembo, tutahakikisha kwamba askari wanaishi maeneo yale ili changamoto hii hasa kipindi hiki cha mavuno tuweze kuidhibiti na wananchi waishi kwa amani, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata Wizara hiyo hiyo ya Maliasili na Utalii, litaulizwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu.

Na. 327

#### **Uhaba wa Watumishi na Vitendea Kazi Idara ya Wanyamapori Maswa**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imekumbwa na wimbi kubwa la uvamizi wa wanyamapori kwenye maeneo ya vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Maswa na Hifadhi ya Wanyamapori Makao na kusababisha uharibifu wa mazao na kutishia usalama wa watu.

(a) Je, ni lini Serikali itashughulikia tatizo la uhaba wa watumishi wa Idara ya Wanyamapori?

(b) Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi vikiwemo gari na silaha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Naibu Waziri tafadhali.

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatayyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Maswa liliopo Mkoani Simiyu katika Wilaya za Bariadi, Meatu na Itlima limepakana na vijiji 32 ambapo vijiji 18 vipo katika Wilaya ya Meatu. Pori hilo lina ukubwa wa kilometa za mraba 274 na lilianzishwa mwaka 1974 kwa Tangazo la Serikali Na. 275. Mwaka 2016 usimamizi wa pori hilo ulihamishwa kutoka Idara ya Wanyamapori kwenda Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (*TAWA*) na wakati huo kulikuwa na watumishi 62.

Mheshimiwa Spika, kwa vipindi tofauti *TAWA* imechukua hatua za kuongeza watumishi kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa eneo hilo. Hadi kufikia Januari, 2021 pori hilo lina watumishi 87 sawa na ongezeko la asilimia 40 kutoka watumishi waliokuwepo mwaka 2016. Serikali inaendelea kuziba mapengo ya idadi ya watumishi kwa kadri ya upatikanaji wa vibali vya kuajiri watumishi. Vilevile Wizara itashirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kujenga uwezo wa Halmashauri kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa vitendea kazi, Wizara itaendelea kutenga fedha za ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari na silaha ili kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Maswa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru na ninaishukuru Serikali kwa kuleta shilingi milioni 51 kwa ajili ya kulipa fidia na kifuta machozi.

Je, ni lini Serikali italeta muswada Bungeni wa kuongeza viwango vya kifuta machozi pamoja na fidia? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na watumishi wa Idara ya Wanyamapori Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ambao ni wawili tu wameelemewa kutokana na upungufu wa vitendea kazi.

Je, Serikali haioni kwa kipindi hiki cha miezi miwili watumishi wa *TAWA* wakawepo doria wakati wa usiku ili kusaidiana na wananchi wanaokesha ili wananchi waweze kuvuna mazao yao katika kipindi hiki? (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Uatlilii naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na hili la pili; ninaomba nimuahidi Mbunge na Wabunge wengine wote ambao wana changamoto ya tembo kwamba kipindi hiki ambacho ni cha mavuno, askari watasimamia zoezi mpaka pale ambapo wananchi watatoa mazao yao na hili litaanza kuanzia sasa. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge hili tutalitekeleza sisi kama Wizara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza ambalo alisema kuleta muswada wa kuongeza kifuta machozi na kifuta jasho kwa wale ambao wameathirika na wanyama wakali hususan tembo; nimelipokea lakini wakati huo huo Serikali inaendelea kuangalia tathmini ya namna ya kufanya, lakini wakati huo huo tunaangalia nchi zingine wamefanyaje.

Mheshimiwa Spika, suala hili kwenye nchi za wenzetu/majirani zetu ambao wana changamoto kama hii, wao

liliwashinda wakaamua kuachana na mambo ya kifuta machozi kwa sababu kadri changamoto inavyozidi kuongezeka, ndivyo gharama zinavyozidi kuongezeka. Serikali ya Tanzania kwa kuwathamini wananchi wake iliona bora iweke hili eneo ili angalau wananchi waweze kufaidika. Kwa hiyo, tunalipokea lakini tutaenda kulichakata na tuone faida na hasara kwa pande zote mbili, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso nimekuona.

**MHE.CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba idadi ya watu nchini inaongezeka, lakini ardhi tuliyonayo haiongezeki na yapo mapori kama hayo na mengine ambayo kwa namna moja ama nyingine hayana tija kwa Taifa.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kufanya tathmini mapori mengine kuyagawa kwa wananchi ili waweze kuyatumia?

**SPIKA:** majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea mawazo hayo na hata sasa kwa sababu kuna changamoto na migogoro mingi kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi, Serikali inaendelea kufanya tathmini na yale maeneo ambayo yanaonekana sio ya faida sana, Serikali itaangalia na italeta mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri na mwisho Mheshimiwa Rais atatoa maelekezo, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya wanyamapori mimi naona kwamba sasa tunapokwenda tutabakiza nchi ya wanyamapori. (*Kicheko*)

Sasa mimi najiuliza hivi ni tembo wangapi wanatosha kuishi katika mapori ya Tanzania ambayo watalii watakuja kuona, kwa sababu kama tembo hawa hawana uzazi wa mpango maana yake sasa tuwaruhusu waishi kwa wananchi, ni tembo wangapi wanatosha ili watalii waone kwamba hawa tembo wametosha tunakwenda kuwaona. Maana yake tunapoamini tembo wakiwa wachache ndio watalii watawatafuta, sasa wakiwa wengi ... kwenye utalii gani?

**SPIKA:** Swali lako tayari Mheshimiwa umeshaeleweka, Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri una mpango gani kuhusu uzazi wa mpango kwa tembo? Majibu taafdhali. (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe tathmini ya idadi ya tembo mpaka sasa; mwaka 2009 kulikuwa na idadi ya tembo 134,000 lakini kabla ya hapo walikuwa wanafika tembo 300 na kadhalika, lakini walishuka mpaka kufika 134,000. Toka mwaka 2009 mpaka 2014 ambapo kulikuwa na *poaching* kubwa, tembo walishuka mpaka wakafika 43,000. Kutoka mwaka 2014 mpaka 2020 wanakadiriwa sasa wameongezeka kufika 60,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaangalia hata ile idadi ya mwaka 2009 bado hatujaifikia; kinachotokea hapa ni kwamba tembo anahamasika hasa kipindi cha mavuno, anaweka kambi kwenye maeneo ambayo ni shoroba zao na anapoweka ile kambi basi wanahamasika kula mazao

ambayo pengine huyu tembo toka azaliwe hajawahi kukutana na hindi, muhogo anahamasika ndiyo maana sasa changamoto sasa hivi imekuwa ni kubwa kwa sababu ni kipindi hiki hasa cha mavuno, ahsante.

**SPIKA:** Lakini alitaka kujua yaani uzazi wa mpango ni *pirliton* au nini, ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri inatosha. (*Kicheko*)

Tuhamie Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki.

Na. 328

### **Hitaji la Umeme Vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika vijiji 28 ambavyo bado havijapata umeme kati ya vijiji 50 vya Jimbo la Singida Mashariki?

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa tuko Nishati, majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Nishati - Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) inaendelea kupeleka umeme vijiji na kuufikisha katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Singida Mashariki lina jumla ya vijiji 50. Vijiji 22 tayari vina umeme; vijiji 12 vinapatiwa

umeme sasa kupitia Mradi wa Ujazilizi (*Densification*) ulioanza kutekelezwa katika Mkoa wa Singida mwezi Novemba, 2020 na unatarajiwा kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, vijiji 16 vilivyobakia vinaendelea kupatiwa umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa *REA* wa kusambaza umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulioanza kutekelezwa mwezi Machi, 2021 na utakaokamilika mwezi Desemba, 2022. Gharama ya mradi ni bilioni 8.47.

**SPIKA:** Safi sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tumeelewana vizuri, yaani *exact*.

Mheshimiwa Mtaturu una swali la nyongeza kweli kwa majibu hayo?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Haya, uliza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa majibu ambayo pia nahitaji nipate uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme ni chachu ya maendeleo na kwa kuwa ni asilimia 44 tu ya vijiji vya Singida Mashariki vina umeme, ninalotaka kujua na wananchi wa Singida Mashariki, hususan Tarafa ya Mungaa ambayo ina kata saba na ambayo haina umeme kabisa.

Ni lini mkandarasi atakwenda kuanza kazi kama alivyosema mwezi Machi mpaka sasa hajapatikana na tunataka tujue jina la mkandarasi huyo?

Mheshimiwa Spika, swalı la pili. Kwa kuwa, vijiji ambavyo amevitaja anasema vina umeme na kwa sababu kuna mradi wa ujazilishaji na mpaka tunavyoongea sasa ni unaenda taratibu mno. Hawaoni sababu ya kuongeza kasi ya kuweza kuweka umeme katika vitongoji vilivyobaki? (*Makof!*)

**SPIKA:** Yaani Mheshimiwa Mtaturu kuna tarafa ambayo haina umeme, tarafa nzima?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, Tarafa nzima ya Mungai yenyewe Kata za Mungaa, Lighwa, Makiungu, Kata ya Ituntu, Mungaa na Kikiyo pamoja na Kata ya Msughaa zote hazina umeme ambazo ni mpakani mwa Chemba.

**SPIKA:** Ngoja nikae vizuri. (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali hilo. Yaani humtakii mema Mheshimiwa Mtaturu kabisa, hebu tusikilize majibu Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakiri ni kweli kwamba mpaka sasa kuna baadhi ya vijiji Tanzania havijafikiwa na umeme. Kama tulivyosema tulianza tukiwa na vijiji 12,268 lakini tumepunguza mpaka sasa tuna vijiji 1,974 ndio havina umeme na mpango uliopo kwa sasa ni kuhakikisha kabla ya mwezi Disemba, 2022 vijiji vyote hivyo 1,974 vyote vinakuwa vimepata umeme na tuko tayari tumeshawapata wakandarasi wa kupeleka umeme kwa kila eneo katika *REA III, Round II*.

Mheshimiwa Spika, Jumanne ya wiki hii tulikuwa tuna kikao na wakandarasi hao ambao tuymewapa kazi hizo na tumewaaagiza kabla ya Jumatatu inayokuja wawe wote wamewapigia simu Waheshimiwa Wabunge pamoja na viongozi wengine kwenye maeneo kuwaambia kwamba tumekuja na tumeripoti kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri juzi kuna maeneo wakandarasi wetu wameenda, lakini hawakuwa wametoa taarifa ya kutosha kwa Waheshimiwa

Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, ili kuweza kujua kwamba wapo. Sasa mimi nimechukua jitihada ya kuwapatia wakandarasi namba za Waheshimiwa Wabunge na kuwaelekeza kabla ya Jumatatu nitakuwa nime-*verify*kwaa Mbunge mmoja-mmoja kujua kama amepigisha simu au kutumiwa *message* kuambiwa kwamba mimi ninaenda kuripoti katika eneo hilo. Kwa hiyo, niseme katika maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Mtaturu ameyataja kazi inaendelea na tutafikisha umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali la pili, kwenye *densification* (ujazilizi); mkandarasi anayeendelea kufanya kazi katika Mkoa wetu wa Singida anaitwa Sengerema, ni mkandarasi mzuri, anafanya kazi yake vizuri na anakwenda hatua kwa hatua na tunatarajia kufikia mwezi Disemba mwaka huu atakuwa amemaliza vitongoji vyote. Kwenye kupeleka umeme kwenye vitongoji tunapaleka kupitia miradi yetu ya REA ambao wanapeleka kwenye vijiji wanashuka kwenye vitongoji, lakini tuna mradi maalum huu wa *densification* ambao wenyewe unalenga vitongoji, lakini pia na wenzetu wa TANESCO bado wanalenga vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kufikia mwaka 2022 tunatarajia kuwa tume-*cover* vijiji vyote, lakini tunakuwa tume-*cover* vitongoji vingi sana. Mpango wetu kuendelea kupeleka umeme katika vitongoji kwa sababu kupeleka umeme ni zoezi endelevu.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati bahati nzuri umefika, kuna tarafa nzima kule kwa Mheshimiwa Mtaturu, tarafa yenye kata saba haina umeme kabisa. Mheshimiwa Mtaturu angekusikia tu kidogo ingemfariji, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, tarafa nzima yaani hapa Singida tu. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipongeze majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika Jimbo la Mheshimiwa Mtaturu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jimbo la Mheshimiwa Mtaturu kimsingi ile tarafa ambayo haijapata umeme pamoja na tarafa nyingine zote wakandarasi wameondoka jana kwenda Singida kwenda kufanya kazi, pamoja na tarafa hiyo. Mheshimiwa Mtaturu alikuwa na vijiji 12 ambavyo havijaguswa kabisa pamoja na hiyo tarafa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mtaturu pamoja na Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa wananchi wa Singida katika jimbo lake wote watapata umeme ndani ya miezi 18 kuanzia jana walipoondoka wakandarasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa mtapata umeme katika miezi 18 kwa hiyo, tulieni.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali la Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge*, Mbunge wa Viti Maalum Tanga. Mheshimiwa Mwanaisha.

Na. 329

### **Makubaliano ya *TICAD* Kati ya Tanzania na Japan**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N.ULENGE** aliuliza:-

Je, ni kwa namna gani Serikali imetumia fursa ya makubaliano ya *TICAD* kati ya Tanzania na Japan ili kupata wawekezaji nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Silaoneka Kigahe, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (*TICAD*) ni chombo kilichoanzishwa na nchi ya Japan mwaka 1993 kwa lengo la kukuza mahusiano, maendeleo na kuondoa umaskini Afrika. Vipaumbele vya *TICAD* vinaenda sambamba na agenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika na agenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, kupitia *TICAD* Serikali ya Tanzania imeweza kuandaa mfumo wa *blueprint* unaoboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na hivyo kupelekea kukuza sekta za uzalishaji, ujenzi wa miundombinu na huduma ikiwemo nishati na kujenga uwezo wa wajasiriamali. Sekta hizo huandaa miradi mbalimbali na kuiwasilisha *TICAD*, ili kupata ufadhilli wa kifedha chini ya uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kiuwekezaji ambayo imeteklezwa nchini kutokana na *TICAD* ni pamoja na maboresho ya Bandari ya Kigoma, uendelezaji wa huduma za usambazaji wa maji Zanzibar, ujenzi wa kituo cha uzalishaji na usambazaji wa umeme kwa kutumia nishati ya gesi mkoani Mtwara, maboresho ya barabara jijini Dodoma na utoaji wa mikopo nafuu kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukuza mahusiano mazuri ya kibiashara baina ya Tanzania na Japan ili kuendelea kunufaika na *TICAD* katika kuvutia wawekezaji zaidi wa ndani na nje ya nchi.

**SPIKA:** Ahsante, Viwanda na Biashara na ninyi punguzeni majibu yenu.

Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, uliza swalii la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; *Tokyo International Conference on African Development (TICAD)* pamoja na mambo mengine inahusisha nchi zote za Afrika kupeleka vijana kwenda

kusoma katika vyuo nchini Japan na kupata uzoefu kwenye kampuni kubwa za nchini Japan kwa lengo kwamba wanapotoka huko waje kufanya uwekezaji hapa nchini kwa kushirikiana na kampuni hizo za Japan. (*Makofi*)

Kwa nini mpango huu kwa Tanzania umekoma ilhali nchi nyingine za Afrika zinzendelea kupeleka vijana Japan kujifunza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; vijana hawa ambao tayari tumebahatika kuwapeleka Japan na wamesharejea. Serikali imewatumiaje kwa kushirikiana na kampuni sasa walikopata uzoefu huko Japan kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili muhimu, Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Silaoneka Kigahe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania na Japan bado wanaendelea na mipango ya kuwapa mafunzo na pia kupata uzoefu wa kazi mbalimbali kuititia taasisi zake nydingi ikiwemo *JICA*, lakini pia kuna utaratibu maalum baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa vijana kwenda kupata mafunzo Japan. Kwa hiyo, sio kweli kwamba tumekoma au utaratibu huo umesitishwa kwa sababu hata mwaka 2019 ambayo ni *TICAD* ya mwisho iliyofanyika nchini Japan baadhi ya maeneo ambayo yaliongelewa ni kuendeleza au kukuza ushirikiano wetu ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, alikuwepo kule Tokyo moja ya maeneo yaliyoongeleta ni kuona namna gani kutumia vijana wetu katika miradi mbalimbali ikiwemo kuvutia kampuni mbalimbali za uwekezaji nchini kama vile *TOSHIBA*, ambayo yanaweza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya

kielektronic, lakini kuhusu kuwatumia vijana ambao wamepata mafunzo au uzoefu mbalimbali nchini Japan.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bado inaendelea kuwatumia vijana hao wengi, lakini pia kwa Taarifa yako na mimi ni mmoja wa vijana hao ambao nimeweza kupata mafunzo Japan na ninaendelea kutumikia Serikali ya Tanzania katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika sekta ya viwanda. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Swalii la mwisho kwa siku ya leo, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Balozi.

Na. 330

**Ujenzi wa Jengo la Utawala *Central Police – Njombe***

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Jengo la Utawala la *Central Police Njombe*?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jengo la ofisi zinazotumika kwa sasa kama jengo la polisi la utawala (*Central Police*) Mkoa wa Njombe lipo katika hifadhi ya barabara kuu iendayo Mkoa wa Ruvuma. Kwa sasa Jeshi la Polisi limeshaomba eneo toka Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa ajili ya kujenga ofisi za

utawala na makazi ya askari na Halmashauri imeshatoa hekari 40 eneo la Lunyunyu.

Mheshimiwa Spika, tathmini kwa ajili ya kulipa fidia wananchi walioko eneo hilo imeshafanyika kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Njombe na kiasi cha shilingi 322,000,000 zinahitajika kwa ajili ya malipo ya fidia na kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia hii ili ujenzi uanze mara moja. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, asante. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Njombe, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza; Serikali imesema kwamba, wanatafuta hizi fedha shilingi milioni 322. Ningependa kujua mkakati mzima wa upatikanaji wa hizi fedha na zitakuwepo kwenye bajeti ipi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; eneo ambalo wamepanga kujenga Ofisi ya Mkoa wa Njombe (*Central Police*), ni eneo hilohilo Ofisi ya Mkoa imepangwa kujengwa na Mahakama ya Mkoa; Ofisi ya Mkoa na Mahakama zimeshajengwa, sasa hii bado.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Njombe wangependa kujua ni lini hasa ofisi hii itajengwa?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe, maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa anauliza; je, katika bajeti hii tumepanga kuweza kupata hizo fedha?

Mheshimiwa Spika, kubwa tu nimwambie kwamba katika bajeti hii hakuna fungu hili, lakini tutajitahidi katika bajeti ijayo pesa hizi ziwepo na tumuahidi Mheshimiwa kwamba, tutampa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba, eneo hili linapata kituo hicho cha polisi ambacho kitatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini je, ni lini sasa Serikali italipa hiyo fidia? Nimwambie tu kwamba, tutajitahidi na tumuahidi mwaka ujao wa fedha tutajitahidi tulipe hiyo fidia, ili sasa ujenzi huu uweze kuanza haraka na wananchi waweze kupata huduma hizo za ulinzi na usalama. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kulipa madeni ya askari ambao unaendelea kwa kuwa wameanza kulipa 2018/2019 na wameacha 2017, lakini pia askari walipandishwa vyeo kutoka Mainspeksa kuwa Warakibu wa Polisi 99, askari 99 ambao walipanda mwaka 2013 mpaka 2017 hawajalipwa mshahara kwa cheo hicho wameanza kulipwa 2018? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca unaishi *line police* au?  
(*Kicheko*)

Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama utakuwa una kumbukumbu hizo, lakini jitahidi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa

Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii hili la Mheshimiwa Jesca kwamba suala hili ni suala ambalo linahitaji takwimu na linahitaji *data* za uhakika. Kwa hiyo, kubwa tu nimwambie Mheshimiwa kwamba pamoja na kwamba utaratibu umeshaanza kupangwa, lakini nimuombe tu kwamba, suala hili aendelee kulipa muda ili tukalifanyie kazi halafu tutajua namna ya kuja kumjibu, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umeisha na leo mambo ni mengi kwa sababu pamoja na mambo mengine, leo siku ya Ijumaa na tungependa leo saa 7:00 mchana tukitoka hapa tuwe tumemaliza. (*Makofi*)

Kwa makofi hayo, maana yake tumeelewana. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kilimo - Ndugu Japhet Justine, simama pale ulipo Ndugu Japhet Justine kama uko, yuko wapi? Hayupo Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kilimo?

Ooh, hayupo bwana, huyu mtu alikuwa anahitajika sana maana anatajwa mara nyingi sana humu ndani ya Bunge. Yupo ee, *camera*, yuko wapi? Ahsante. (*Makofi*)

Meneja wa Kanda ya Kati, Yodas Mwanakato wa hii Benki ya Kilimo; inaelekea mtu na bosi wake hawapo hawa.

Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Ndaki ni wamiliki wa vitalu vya *NARCO* wakiongozwa na Ndugu Elpidius Kalabamu; ahsante na karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 42 wa Mheshimiwa Doto Biteko - Waziri wa Madini ambao ni wanafunzi na walimu wa Taasisi ya Teknolojia ya *DOMAC* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Chuo hicho Ndugu Happy Mwajunga, ahsanteni popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni 23 wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaao ni walimu kutoka Jimbo la Mkuranga wakiongozwa na Mwalimu Bakari Jiri, ooh, karibuni sana walimu kutoka Mkuranga, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Ulega ambaao ni wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Jimbo la Mkuranga wakiongozwa na Ndugu Ally Msikamo, ahsante. (*Makof*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wakiongozwa na Ndugu Sunday Mbogo. *UDOM*, wale kule, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Yahya Mhata ambaao ni wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali wanaotokea Nanyumbu Mkoani Mtwara, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Sajani Mterume; wale wa kutoka Nanyumbu, karibuni sana ndugu zangu. (*Makof*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa *Engineer Ezra Chiwelesa* ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) kutoka Biharamulo, Mkoani Kagera wakiongozwa na Ndugu Frank Faustine; wale wa Biharamulo, karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa *Engineer Chiwelesa* ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Biharamulo, Mheshimiwa Leo Lushau, karibu Mheshimiwa Leo popote pale ulipo, ahsante. (*Makof*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Saasisha Mafuwe ambaao ni wanafunzi wanaosoma *UDOM* kutoka Jimbo la Hai wakiongozwa na Ndugu Ngao Godliving; wale wa Hai, karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Neema Lugangira ambaye ni Mkurugenzi wa *NGO* ya *Ethelstars Kids Books Foundation* Ndugu Evelyn Kweka karibu sana Evelyn yupo kule juu. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Midimu ambao ni wachungaji kutoka jijini Dar es Salaam, Mchungaji Dolomi Magoti na Mchungaji Johnson Chiragi, karibuni sana wachungaji. (*Makofi*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Kasalali Mageni waliokuwa wagombea Ubunge wenzake kwenye kura za maoni ndani ya CCM kutoka Jimbo la Sumve wakiongozwa na Ndugu Charles Mpelwa, karibuni sana, karibuni sana sana sana. (*Makofi*)

Hebu endeleeni kusimama kidogo ninyi watu waungwana sana, ninyi ni wa kutilia mfano hamna nongwa, hamna noma, basi pale mlipotaka kuja ndio hapa, ndio mjengo wenyewe huu, basi karibuni sana tunafurahi na tunafarijika kuwaona na wengine muwalete wenzenu, waje watembelee mjengo kidogo, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Segerea Ndugu Tatu Khamisi, Ndugu Madaraka Msigara na Ndugu Nasma Salum, karibuni sana karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Manyoni Magharibi na wadau wa *VICOBA* kutoka Itigi Mkoani Singida wakiongozwa na Sophia Richard, karibuni sana wana *VICOBA*. (*Makofi*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Yahya Mhata nafikiri imejirudia hii imejirudia hii.

Wageni 11 wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mante Ntonja, karibuni sana kutoka Dar es Salaam. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni wavuvi kutoka Jimbo la Buchosa, Mkoani Mwanza wakiongozwa na Ndugu Scolastica Honolant, wavuvi mpo karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Njalu Silanga ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu William Isack, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Deus Sangu ambaao ni rafiki zake na wafanyakazi wa Benki ya Posta Dar es Salaam wakiongozwa na Meneja Manunuzi wa Benki hiyo Ndugu Leonard Mafuru, karibuni sana Posta. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Protas ambaao ni rafiki zake kutoka Igala Mkoa wa Tabora Ndugu Karim Haji na Ndugu Alija Mwami, karibuni sana wako pale. (*Makof*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaao ni wafanyabiashara wa *Capital City Mall* wakiongozwa na Ndugu Elirehema Msuya, karibuni sana *Capital City Mall*. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge ziko *malls* za uhakika hapa Dodoma moja wapo ni hii *Capitali City* na vijana hawa wanafanya kazi nzuri sana pale kwenye ile *mall* mnakaribishwa wakati wowote mkitaka kujua ipo wapi na inafanya kazi gani muulizeni Mheshimiwa Anthony Mavunde, mwenyeji wetu. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Martha Mariki ambaao ni rafiki zake kutoka Mpanda, Mkoa wa Rukwa ni Mstahiki Meya wa Mpanda Mheshimiwa Hillary Sumary na Mheshimiwa Joseph Mwakayoka, ahsanteni sana. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa John Pallangyo ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Maji ya Chai Ndugu Tateni Mbise na Diwani Kata ya Maji ya Chai Mheshimiwa Elirehema Mbise, karibuni sana popote pale mlipo. (*Makof*)

Kwa mafunzo ni wageni wawili kutoka Jijini Arusha ambaao wamekuja kujifunza Ndugu Eva Temu na Ndugu Glory Njau wale pale, karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni kutoka Jijini Dodoma Ndugu Gladness Kirei ambaye amekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya

shughuli zake, karibu sana Gladness yule kule kwenye kona kabisa, safi sana tunawakaribisha wageni wote mkiwa ni pamoja wale wa kutoka Arusha, Arusha kuna mambo, ujue Arusha bwana, Arusha. (*Makofi/Kicheko*)

Ninayo matangazo Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake humu ndani ya mjengo Mheshimiwa Shally Raymond anawaomba niwatangazie Wabunge wanawake wote kuwa kesho tarehe 29 Mei, 2021 kuanzia saa nne asubuhi kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wanawake kuhusu lishe bora katika Ukumbi wa Msekwa. Kesho Ukumbi wa Msekwa Wabunge Wanawake kuna mafunzo kuanzia saa nne yanayohusu lishe na utaratibu wote umezingatiwa mambo yanayohusu utaratibu yapo sawa sawa. (*Makofi*)

Nimearifiwa kwamba leo siku ya Ijumaa tarehe 28 Mei, 2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu Cassim Majaliwa Majaliwa atasafiri, hivyo hatokuwepo Bungeni, kwa ajili hiyo Mheshimiwa George Boniface Simbachawene - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atakaimu majukumu ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Seif Gulamali sasa sijui hili kaandika kama Meneja wa *Bunge Sports Club* au kama Mwenyekiti wa Yanga, nadhani kaandika kama Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mechi ya kujipima nguvu iliyofanyika asubuhi hii ya leo kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge dhidi ya Watumishi wa Bunge timu ya Waheshimiwa Wabunge imeshinda magoli manne na timu ya Watumishi wa Bunge wamepata goli moja, yaani Wabunge wanastamina kuliko watumishi, hii mechi itabidi irudiwe hii watumishi wa Spika wakinangusha tena itabidi wachukuliwe hatua za kinidhamu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge waliofunga magoli ni pamoja na Mheshimiwa Simai Sadiki, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa

Cosato Chumi, na watumishi wa Bunge Ndugu Rajabu Kipira ndiye aliyefunga, ahsanteni sana. (*Kicheko/ Makof*)

Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA  
MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea.

Sasa kwa sababu zile nllizozieleza za muda nitaomba sana twende kwa dakika tano/tano ili tuweze kuchukua angalau wachangiaji wengi tunavyoweza kwa wote dakika tano/tano tujaribu hivyo.

Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuataiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara iliyoko mbele yetu.

Awali ya yote ninataka kuipongeza na kuishukuru Wizara, Mheshimiwa Waziri na timu yako ya Naibu Mawaziri, Naibu Waziri Gekul wakati akiwa Naibu wako na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega ambao wamefanya ziara katika Wilaya yetu na kutatua changamoto zilizokwu zinatukabili, nawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Ulega ulivyokuja lile ulilolifanya limeleta matumaini makubwa kwa Wana-Mkinga, lakini limeibua mahitaji makubwa sana, tunashukuru wa *engine* ya boti ile kwa kikundi kile cha ushirika, lakini sasa kuna vikundi kwenye mwambao ule karibu 12

mahitaji ya *engine* za boti zile kwa ajili ya uvuvi ni makubwa, nitawasilisha Wizarani kwenu kwa maandishi majina ya vikundi vile tunaomba mtusaidie. (*Makof!*)

Lakini Mheshimiwa Waziri tulifika Wizarani kwako na Madiwani wawili kuzungumzia changamoto ya mnada kwenye mpaka wetu wa Horohoro, nakushukuru sana, mma-act kwa haraka tumeefanya jitihada sasa za kuanzisha mnada ule, naomba mwaka wa bajeti huu utakapoanza tukamilishe yale yaliyobaki ili mnada ule uweze kuanza, tuweze kupata mafanikio. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nijielekeze kwenye eneo la ufugaji wa samaki; ninaiona jitihada inayofanyika hasa hasa kwenye upande wa uzalishaji wa vifaranga, nawapongeza, lakini ninaamini bado tungeweza kufanya vizuri zaidi hasa kwenye ukanda wa Pwani tumeusahau, aidha tumeusahau au tunaogopa gharama za kuwekeza kwenye eneo hili. Ndugu zangu samaki wanaoliwa duniani zaidi ya asilimia 50 wanatokana na samaki wanaofugwa. Kwa hiyo, hatuwezi sisi kuacha kuwekeza kwenye eneo hilo, hatuwezi kuuacha uchumi mkubwa kiasi hicho, kuna kipindi nilisema hapa hivi wenzetu Afrika ya Kusini *Western Cape* na *Eastern Cape* wamewezaje kwamba eneo hili la ufugaji wa samaki linawabeba? Kwa nini tusiende kujifunza kule? Hivi kwa nini sisi leo hii tuzidiwe na Zambia kwenye kuzalisha na kuuza samaki? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, miaka michache iliyopita tulikuwa tunazungumza na Katibu Mkuu Dkt. Tamamatamah tukiona ni jinsi gani ambavyo Wazambia wale wamekwenda kupata fedha kutoka *African Development Bank* wameanzisha mradi mkubwa wa ufugaji wa samaki na sasa umeanza kutoa matokeo. Kwa nini sisi tusifanya hivyo? Lakini Wizara kwa nini msichukue *initiative?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imetoa fursa kwa Halmashauri kuwa na miradi ya kimkakati, watu wengi wanaenda kuwekeza kwenye *stand* na vitu vya namna hiyo, kwa nini ninyi Wizara msiichukue hii *initiative*, msichukue

*opportunity* hii, mkatuma wataalam wenu kwenye Wilaya zile zinazopakana na hahari mkasema tunataka kutengeneza *pilot district* hata tano tu bila kuisahau Mkinga, mkaenda mkafanya *study*, mkafanya *visibility study*, tukaja na Mkakati Wilaya hizo badala ya kuwekeza kwenye *stand* waende wakawekeze kwenye ufugaji wa samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkiweza kufanya hivyo mtaibua ufugaji wa samaki kwenye maeneo haya na shughuli za kiuchumi zitakuwa. Ninawaomba bajeti hii ikipita tumeni wataalam wenu Mkinga, waje tukae, tutengeneze *visibility study*, tuweze kufuga samaki kwenye mwambao ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Mheshimiwa Khadija Aboud utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniamsha salama asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwanza sina budi kutoka pongezi za dhati kwa Wizara hii Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudji mbalimbali wanazofanya kuhakikisha sekta zetu mbili za uvuvi na mifugo zinapiga hatua na kumsaidia mwananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na maoni ya Kamati kwamba Bajeti ya Wizara hii ni ndogo, utoaji wa fedha hauendi kwa wakati, hivyo inachangia kurudisha nyuma mipango kabambe ambayo imepangwa na Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali itoe fedha kwa wakati na iongeze bajeti kwa ajili ya kutatua changamoto na kupiga hatua mbele mbalimbali za maendeleo, kwa sababu Wizara hii ina mchango mkubwa katika kuongeza

pato la Taifa. Tutapata fedha za kigeni kupitia Wizara hii, tutaongeza ajira, lakini pia Wizara hii itatusaidia kwenye usalama wa chakula kwa maana tutapata vitoweo, maziwa na vitu vinginevyo ambavyo vitasaidia usalama wa chakula katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na mawazo ya Kamati kwamba sheria za uvuvi na mifugo na kanuni zake zifanyiwe haraka zikamiliike ili kutatua changamoto za wavuvi na wawekezaji wa uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea ninakuja kwenye sekta hii ya uvuvi, kwenye uvuvi wa bahari kuu nawapongeza sana Serikali kwamba sasa tunaingia kwenye uchumi wa *blue* kwa vitendo na imesema hapa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 itanunua meli mbili za uvuvi kwa kuanzia. Sasa mimi ninataka nliamble Wizara kwakuwa chombo hichi *DSFN*cha Kitaifa mell mbili za uvuvi za Zanzibar zitanunuliwa kwa awamu gani ya bajeti? Naomba hapo nayo ituweke sawa ili tujue tunafanya nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye uwekezaji wa viumbe kwenye maji, hapa pana soko kubwa sana la ajira kwa vijana na wanawake. Eneo hili litakwenda kutatua changamoto za ajira kwa vijana na wanawake, lakini pia itaongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja, kitaongeza kipato kwa vikundi, lakini pia kipato kikubwa kwa Taifa, kwa sababu tutawekeza kwenye hii sekta, tutauza nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uingizaji mkubwa wa samaki kutoka nje hivi kweli hata saladini tunaagizia kutoka nje, vibua vile ambavyo vimejaa nchini mwetu, lakini tunaagiza kutoka nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa kuna vyuo ambavyo vinatoa mafunzo ya ufugaji wa samaki vyuo vile ninawashauri serikali iwe na programu tofauti, programu ya muda mrefu na ya muda mfupi, zile za muda mrefu ziendelee kwa wale wanaotaka utaalamu zaidi, lakini zile za muda mfupi ziwe kwa vijana wetu hawa wa katni na katni

ambao watatoka kupata ajira wakaanzie miradi yao. Ninashauri ili kuvutia uwekezaji katika sekta hii kwa wananchi mbalimbali wale wataalam ambao wamepata mafunzo kwenye vile vyuo vyetu nya mafunzo Wizara iwe inawatangaza, waweke kumbukumbu zao na wajulikane wako wapi ili mwananchi anapotaka kuanzisha huu mradi ajue mtaalam nitampata wapi wa kunisaidia kutengeneza huu mradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na wale vijana ambao tunawapatia mafunzo kwa program ndogo ndogo zile zitakazoundwa na Wizara ninashauri kuna mifuko ile ya vijana ya uzalishaji mali ya wanawake sasa badala ya kuwapa *cash* watengeneze ile miundombinu, hawa vijana wameshapata mafunzo, watengenezewa miundombinu, wajengewe mabwawa, vifaa na vifaranga waanzishe, hii itakuwa chachu kwa vijana wengine watakapoona wenzao wanafaidika na wao kutaka kujifunza utaalamu huo wa ufugaji samaki na wa viumbe kwenye maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye ufugaji wa samaki na viumbe kwenye maji sio samaki tu, pweza, na nini, lakini kuna madini pale yanapatikana madini ya lulu. Madini ya lulu yanahitajika sana duniani, yana soko kubwa, tunayapata kwa kupitia ukuzaji wa viumbe kwenye maji, kuna lulu zinapatikana baharini, lakini lulu tunaweza tukazitengeneza wenyewe kwenye vizimba vyetu, lulu ni madini makubwa duniani yanahitajika sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwa dakika zangu chache zilizobaki labda nijikite kidogo kwenye suala la ufugaji. Wizara ijitahidi sana ufugaji wenye kuhifadhi mazingira ya nchi kwa maana zile Ranchi za Taifa, Kamati imeshauri vizuri, zile Ranchi za Taifa na nyongeza yangu hii iwe kama shamba darasa sasa kwa wafugaji ili kuwepo na mabwawa, kuwepo na malisho, halafu kuwe na program kuwachukua wale wenye ng'ombe wengi wafugaji wakubwa waliopo kwenye Mikoa yetu waje pale wajifunze namna ya kuhifadhi mazingira, yaani wafuge kitaalamu, wavutike na ile ranchi kwamba hapa tukifanya hivi na sisi tunaweza tukafanya kwa

sababu wakirudi kule kwenye maeneo yao waanzishe hiyo miradi kwa sababu uwezo wa kuanzisha wanao kwa sababu wana ng'ombe wengi wanaweza wakauza wakaanzisha hayo malambo na vitu vingine vyta kulishia wanyama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaweza tukawekeza mabwawa kwenye maeneo, lakini bado wafugaji hawahamasiki kukaa pale pale wanaendelea bado kuendelea kuhamza hama lakini tukifanya programu maalum...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija muda wako umekwisha.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na kwa sababu muda ni mfupi nitachangia kidogo na ninaanza kwa kuunga mawazo yote ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kweli inafikia haiwezi kufanya maajabu bila ya kupata fedha za kutosha na hasa fedha za kutosha za maendeleo kama nilivyosema kwenye taarifa ya Kamati mpaka mwezi Aprili kwa upande wa uvuvi ilipata asilimia 31 tu na miaka yote mitatu iliyopita ilikuwa inapata fedha pungufu kwenye fedha za maendeleo. Kwa hiyo, ninaomba na ninaishauri Serikali iongezee fedha hizi Wizara kusudi iweze kufanya mambo mazuri kwenye uvuvi pamoja na mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuongelea ni ufungaji wa kisasa; wananchi wote waelewe

kuwa kufuga siyo kuchunga, tuweze kufuga ufugaji wa kisasa Wizara waweze kujikita kutoa elimu ili kusudi tuweze kufuga ufugaji wa kisasa, tuweze kupata maziwa ya kutosha, ng'ombe mmoja anaweza akatoa maziwa lita 32 kwa siku. Nenda mkajifunze kwa mwekezaji wa Iringa yule ASAS ambaye anafuga ufugaji wa kisasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikifika hapo naomba Wizara pia iangalie hawa wawekezaji iweze kuwapa mazingira mazuri ya uwekezaji, kwa mfano uwekezaji kwenye viwanda vya samaki, unakuta wawekezaji wengine wanapata shida, uwekezaji kwenye mifugo waweze kuwawekea mazingira mazuri tuweze kupata uwekezaji wa kisasa. Kwa mfano, kwa upande wa maziwa bado tunaagiza maziwa mengi kutoka nje, mimi nashangaa tuna mifugo mingi ni nchi ya tatu Tanzania, lakini bado tunaagiza maziwa kutoka nje. Wizara tuangalie jinsi ya kuboresha maziwa tuweze kuzalisha na kusindika maziwa yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende tena kwenye Bwawa la Mindu wote mnalijua Bwawa la Mindu pale Morogoro, naomba wale wananchi wawekewe utaratibu mzuri unaoeleweka waache kuvua kwa kijiiba, waweze kuvua kwa utaratibu uliopo kusudi waweze kunufaika na Bwawa hilo la Mindu.

Mheshimwia Spika, nikienda Kilombero kwenye Mto Kilombero sasa hivi Samaki wamepungua zamani samaki walikuwepo wawekee mazingira mazuri kusudi samaki waweze kuzaliana na wananchi wa Kilombero na wa Morogoro waweze kupata kitoga ile waliokuwa wanavua kwenye Mto wa Kilombero. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa vifaranga wananchi wengi sasa hivi wamehamasika kufuga vifaranga kwa hiyo iwepo uzalishaji wa vifaranga na elimu kutoka kwa Maafisa Ugani wa Uvumi ambao sasa hivi ni wachache. Naomba liangaliwe ufugaji huo huo wa vifaranga ili kusudi waweze kupewa wananchi waweze kufuga kwenye mabwawa

pamoja na vizimba, uvuvi ni uvuvi mzuri sana kwa hiyo inaweza ika...

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *NARCO* naomba matatizo yote yaliyopo kwenye *NARCO* yaweze kutatuliwa, pia muda wa kupewa vitalu usiwe mwaka mmoja wapewe vitalu kwa muda mrefu kusudi aweze *ku-own* kwani kitalu chake na aweze akawekeza vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wale wananchi wanaozunguka ranchi hizo hizo waweze kunufaika na ranchi hizo. Nikija kwenye Ranchi ya Kongwa mpaka sasa hivi naomba iangaliwe vizuri kwa sababu sasa hivi imezungukwa na magugu ya Kongwa, hayo magugu ya Kongwa yaweze kutolewa kusudi iweze kuonekana kuwa ni ranchi na wananchi waliozunguka ranchi hiyo waweze kunufaika na vitalu hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa kuwa masoko kuna masoko vijana wanaweza wakanufaika na masoko kusafirisha wanyama na nyama nje, kwa hiyo waweze kupewa elimu jinsi ya kuweza kuwanufaisha vijana na watu wengine nje bado wanahitaji nyama, bado wanahitaji maziwa kusudi tuweze kunufaika na masoko ya nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuimarisha afya ya wanyama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja, lakini naomba tasnia hii ya uvuvi na mifugo iangaliwe vizuri inanufaisha wananchi wengi, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Christine Ishengoma - Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Selemani Kakoso atafatiwa na Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii na niwashukuru sana Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hasa kwa kushughulikia kero za wavuvi kwenye eneo la Ziwa Tanganyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita zaidi kwenye eneo la uvuvi. Uvuvi ni eneo ambalo linaweza likalipatia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa sana. Lakini kwa bahati mbaya sana Ziwa Tanganyika ni ziwa ambalo halijawekezwa kitu chochote ambacho kinaweza kikatoa tija kwenye sekta ya uvuvi. (*Makofii*)

Niombe sana Mheshimiwa Waziri sisi Watanzania tunatamani keki iliyo ndogo iweze kuwanufaisha sehemu zote, kwa bahati mbaya sana Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa ni mikoa ambayo inapakana na Ziwa Tanganyika na tunapakana na nchi jirani ya Zambia, Kongo na Burundi.

Mheshimiwa Spika, mazao yanayozalishwa ndani ya maeneo hayo wanufaikaji wakubwa ni nchi jirani kuliko sisi ambao tuna eneo kubwa sana eneo la ziwa na hiyo ni kwa sababu Serikali haijawekeza kitu chochote ziwa Tanganyika lina kina kirefu na bahati mbaya asilimia kubwa ya mazao yanayotoka kwenye ziwa hili mengi yanapatikana kwa uvuvi ule wa kubahatisha. Tunaiomba Serikali sasa ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais ya kujenga kiwanda kwenye eneo hilo na kuhakikisha wanapeleka zana za kisasa liweze kutekelezwa, kinyume na hapo tutakuwa tuna shuhudia samaki ambao wanakufa ndio unawajua kwamba kwenye ziwa hili kuna samaki wakubwa kama hawa.

Mheshimiwa Spika, niombe Mheshimiwa Waziri aje na maelezo ya kutueleza uwekezaji mkubwa utakaowekwa kwenye Ziwa Tanganyika, tumeshuhudia kila mradi unaokuja kwenye Wizara unaelekezwa ukanda wa Pwani, unaelekezwa ukanda wa Ziwa Victoria na pengine Naibu

Waziri anatoka ukanda wa Pwani na Waziri anatoka ukanda wa Ziwa Victoria. (*Makofii*)

Sasa tunataka watuthibitishie katika Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Rukwa ni mradi upi ambao watakuja kuwekeza kwenye ziwa Tanganyika. Nilikuwa naomba maelezo yatoke ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo hilo bado tuna mialo ambayo inahitaji kujengwa kwenye ukanda wa ziwa, kwa bahati mbaya sana mialo iliyopo kwenye eneo hilo ni kidogo mno. Nilikuwa naomba maelezo ya Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake ni lini ataleta mwalo kwenye Kijiji cha Karema, Tarafa ya Karema ambako kuna wavuvi wapo na wanahitaji huduma hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna eneo la mifugo; sisi tuna mifugo mingi sana ambayo imetoka Ukanda wa Ziwa iko kwenye Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa; tuna idadi ya mifugo mingi sana, lakini hakuna uwekezaji wa aina yoyote ile. Tulikuwa tunaomba atueleze Mheshimiwa Waziri sisi tutakuwa tunapokea tu idadi ya mifugo, lakini miradi ya maendeleo hakuna. Hakuna cha kiwanda chochote hata cha maziwa kilichoko kwenye maeneo hata kidogo, lakini bado wafugaji wanaishi kwenye mazingira ya kuhamahama kwa sababu hawana malisho ya kutosha. Tulikuwa tunaomba atueleze ni lini atatujengea mabwawa; atajenga mabwawa ambayo yatawasaidia wavuvi na wakulima na wafugaji ambao wapo kwenye maeneo hayo ili yaweze kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji sana mipango ya masoko ya zao la ng'ombe tuna ng'ombe ambao ukweli wanauzwa kwa bei ya chini mno ni kwasababu hatuna masoko mazuri. Kwa hiyo, tunaomba sana atuhakikishie Mheshimiwa Waziri ana mikakati ipi ya kuimarisha masoko kwenye maeneo ya minada. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilishakutaja Mheshimiwa Fredy Mwakibete atafatiwa na Mheshimiwa Hassan Mtenga.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye ametufanya leo tuwepo asubuhi hii, na kipekee nikushukuru wewe namna ambavyo unaongoza Bunge lako zuri na zaldi pia niishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Waziri Mheshimiwa Mashimba Ndaki, pamoja na Naibu Waziri - Mheshimiwa Ulega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie katika maeneo mawili ya uvuvi pamoja na ufugaji hususan katika Jimbo la Busokelo, lakini kabla sjafika huko ningeanza kwanza kwa kuishukuru Wizara mmetujengea majosho, mmetununulia majokofu ya chanjo, mmeanzisha mfumo ambao utatumika kwa wafugaji wote kwa ajili ya kuripoti maradhi yote ya wanyama kupitia mfumo huu najua Serikali itakuwa inapata taarifa sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko na kilio cha wavuvi kwa muda mrefu hususan suala la nyavu. Siku za nyuma Serikali ilikuwa ikichoma nyavu ambazo hazijakidhi vigezo, lakini kwa bahati mbaya sana kulikuwa hamna uhalali ama uhalisia kwa nini wanachoma nyavu ambazo kimsingi kulikuwa kuna *contradiction* ama muingiliano wa kati ya Wizara pamoja na *TBS*. *TBS* wao wanatambua nyavu za milimita sita, lakini Wizara inatambua nyavu za milimita nane. Kwa hiyo, hawa watu wa Wizara wakienda kukamata nyavu kwa wavuvi wanaona hazijakidhi vigezo, lakini wakati huo yule anayetengeneza ama kutoka kiwandani China kwa nje

ya *box* anaandika milimita nane, lakini kiuhalisia ndani ya *box* hizo nyavyu inakuwa ni milimita sita. Kwa hiyo, ni hasara kubwa ambayo imetokana na kutokuwa na mahusiano katil ya Wizara pamoja na *TBSambavyo* vyote viko chini ya Serikali. Nafikiri kuna haja ya jambo hili kuliweka vizuri ili tusiwatie hasara wavuvi wetu wakati ni makosa yetu sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka pia nichangie suala la uvuvi wa bahari kuu; kwenye Mpango wa Serikali mwezi wa pili nilichangia namna ambavyo bahari kuu (*blue zone*) inaweza ikaleta fedha nyangi sana katika pato la Taifa na niipongeze sana Serikali kwa kuchukua hatua madhubuti na wewe mwenyewe mwaka 2018 Bunge lako lilipounda Tume Maalum ya Masuala ya Uvuvi ilikuja na ripoti nzuri na ndio maana matokeo yake hivi leo Serikali imeamua kwenda kununua meli za uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana katika jambo hili sina sababu ya kurudia tena takwimu hizo kwa sababu tayari ninaamini Serikali mnakwenda kuyafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kwenye ng'ombe wa maziwa; Jimbo langu la Busokelo tunazalisha maziwa mengi sana na maziwa mengi sana yanapotea na kwa bahati mbaya sana nchi tunaagiza tena maziwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe taarifa takwimu zifuatazo; kwanza tuna ng'ombe 31,079; lakini kwa siku tunazalisha lita 124,320; kwa mwezi tunazalisha lita 3,729,600 ambapo kwa mwaka sawa na lita 44,755,200. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini bei ya maziwa yanayozalishwa Busokelo kwa lita ni shilingi 600 na kwa bahati mbaya sana maziwa ambayo yanaingia sokoni kwa ajili ya kununuliwa kwa siku ni lita 5,000 kutoka lita 124,320 yanayonunuliwa pekee ni lita 5000 wakati kwa mwezi yananunuliwa pekee ni lita 150,000 kutoka lita 3,729,600 na kwa mwaka maziwa yanayonunuliwa ni lita 1,800,000 kutoka

lita 44,755,200 sawa sawa na kusema tunapoteza kwa mwaka fedha za Kitanzania shilingi 25,773,120,000 ni fedha nyingi sana hizi.

Sasa swali ambalo Waziri uje uwaambie wananchi wa Busokelo na Watanzania; kwa nini tunaagiza maziwa kutoka nje ya Tanzania angali maziwa lita zaidi ya 42,955,200 zinazalishwa Busokelo kupitia njia ya *zero grazing?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini Waziri utakuja na majawabu sawasawa ili tusiendelee kuagiza maziwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niunge mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Mwakibete. Mheshimiwa Hassan Mtenga atafatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo, lakini Mheshimiwa Hassan Mtenga kwanza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa kuweza kuchangia Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo, lakini inawezekana Wabunge tukazungumza sana humu ndani, lakini bila kuelewa au kujua kwamba tunakoelekea kwenye Wizara hii ili kuleta tija ni wapi.

Mheshimiwa Spika, tunayo bajeti ya shilingi bilioni 121 bajeti hii kama itaweza kutoka kwa wakati na ikafika kwenye maeneo husika na ikaweza kufanya kazi haya mengine ambayo ni changamoto ndani ya Wizara hii inawezekana yakapungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kule kwetu Mtwara tuna bandari lakini tuna bahari kubwa mno na bahari ile takribani ndani ya miaka miwili iliyopita tumeshakamata meli zaidi ya mbili na zile meli ni meli za kigeni zinakuja kuvua kwenye eneo letu. Lakini meli ya kwanza imekamatwa ikiwa ina tani zaidi ya 150,000 za samaki, meli kubwa na samaki hawa wanavuliwa kwenye bahari za kwetu lakini kikubwa zaidi

ambacho tunaweza tukapiga kelele tunao wavuvi, wavuvi hawa ni wavuvi ambao tunasema ni wajasiriamali, lakini bado Wizara haijapeleka kuwatambua hawa wavuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoa mfano leo tunazungumza kwamba mvuvi anayekwenda kuvua ambaye hana boti ana mtumbwi tu tunamwambia aende akavue mita 50. Mita 50 unazzungumzia pale Nungwi na mita 50 ili aweze kuzama mita 50 lazima awe na mtungi wa gesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwangu pale Mtwara hawa wavuvi hakuna aliyeruhusiwa kuingia baharini na mtungi wa gesi. Sasa tukienda Dar es Salaam tunakuta kuna wavuvi ambao wanatumia mitungi ya gesi, sasa sielewi hizi sheria zinafanyaje na tunaangalia wapi watu wanahaki na wapi watu hawana haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala la uvuvi wa usiku, leo ukienda Dar es Salaam wako matajiri wakubwa wanavua mchana na matajiri wale wana maboti makubwa na wameruhusiwa, na kazi hii yote anafanya Katibu Mkuu ndiyo mwenye maelekezo ya kuwaelekeza kwamba matajiri waende wakavue mchana, maskini waende wakavue usiku, athari za uvuvi wa usiku kwasababu unapokwenda kuvua usiku, sisi ni watu wa baharini kuna maeneo yanakuwa na miamba, unapokwenda na jahazi au na chombo mwamba huwezi kuujua usiku, lazima ufile mahala uchemke ndiyo utakapojuwa kwamba hapa ninapoelekea pana mwamba.

Mheshimiwa Spika, Mtwara yenyewe ukizungumza Kilambo, Mtanga Mkuu, Kianga, Mikindani hapa ninapozungumza takribani ya watu zaidi ya 100 wamepotea baharini, wamefariki. Sasa huku tunakokwenda tunakoelekeea Wizara yetu bado haiwawezeshi wavuvi wadogo, kinachofanya sasa hivi Wizara bado inakwenda kuwamaliza wavuvi wadogo.

Natoa mfano hawa wanaumoja wao wana asasi zao, lakini leo Katibu Mkuu unashindwa kuwaita viongozi hawa wa wavuvi mkakaa nao mkajadiliana. Lakini ukiangalia

kwenye mijadala yao yote, katika *paper* zao zote ni za kiiingereza, wale wamesoma darasa la nne hamna aliyefika hata darasa la saba wale viongozi wote wa uvuvi, wanakwenda kuelewa kitu gani? Lakini mnaptisha mle sheria, kwamba hatuwezi kuvua hapa na *ring net*. (*Makof*)

Mheshimiwa Hayati Magufuli wakati akiwa kwenye Wizara hii alileta hapa waraka na mkakubaliana Bunge zilizopita kwamba *ring net* iwe sahihi kwenda kuvua sasa leo kwanini nyavu za *ring net* zinapigwa marufuku na wavuvi wanakamatwa? (*Makof*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Ahsante, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Mwakamo atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohamed Juma. Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia kwenye Wizara hii.

Kwanza nami niungane na wenzangu kumshukuru Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri ambayo wameiwasilisha. Lakini pia niungane na michango mingi ambayo imetoka ukiwepo ule ambao wewe mwenyewe umeuzungumza kwa uchungu sana jana wa *NARCO* ni hali halisi ambayo Waziri anatakiwa aone ni namna gani chombo kile kilivyo kwa sasa kwenye Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi kulingana na muda nitachangia maeneo mawili na nitaanza na eneo moja la rasilimali za malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa sana linalosababisha ukosekanaji wa malisho ya mifugo na hii inasababishwa na ufinyu wa maeneo ambayo wafugaji wetu wa kawaida wanafugia na jambo hili linasababishwa vilevile na watu hawa ambao ni wafugaji wadogo wa kwenye maeneo yetu kutokuwa na uhakika wa kumiliki ardhi. Matokeo yake wanakwenda kwenye maeneo ambayo yana maji ya asili kama mabonde ya Mto Ruvu, mabwawa mbalimbali na kwa kuyafuata maji hayo wanasababisha kuwe na matatizo makubwa ya migogoro ya wakulima na watumiaji wengine wa ardhi hasa hasa wafugaji. (*Makof*)

Kwa hiyo, nilikuwa naushauri kwa Wizara, ipo migogoro ambayo inasababishwa na matatizo haya na ufumbuzi wake ni kutaifisha maeneo ambayo hayatumiki kwa sasa na kupewa hawa wafugie, maeneo ya kwanza yakiwa haya naitwa *NARCO*. Hizi Ranchi nyingi, ranchi hizi ni sawasawa na wawekezaji wengine wowote, kama Serikali kupitia Wizara ya Ardhi inayouwezo wa kufuta hati kwenye mashamba makubwa ya wawekezaji na yakagawiwa wananchi au wakarudisha Serikali kwa ajili ya kupangiwa matumizi mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri Wizara ya Ardhi itazame hizi ranchi ikiwezekana wazifutie umiliki, wazirudishe kwa wafugaji wadogo, wapewe bure, wakakatiwe vitalu kule ndani na wasilivipie, wamilikishwe ili waendeleze shughuli zao kwa sababu wao ni Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ambalo ninataka nilizungumzie ni suala nzima la utatuzi wa migogoro. Nimeona kwenye hotuba ukurasa wa 48 Waziri ameeleza namna alivyoshungulikia migogoro hasa kwenye jimbo langu na amevitaja vijiji ambavyo amehisi kwamba amemaliza migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwanza niombe nimueleze Waziri kwamba migogoro hii anayohitaji hajjamalizwa na mimi wasiwasi wangu inawezekana wataalam hawa wamemaliza mgogoro kupitia ofisi kwenye ramani, wameitazama ramani

ya ukubwa wa shamba, wakaligawanya kwa majibu haya walioyatoa, lakini halilisi kwa wananchi siyo hii. Leo hii ukienda Dutumi ambako wao wanazungumza wamewaachia hekta 1,600. Ukienda kule kuna mgogoro mkubwa hili jambo siyo kweli, wametaja wamekwenda Madege wamewakabidhi hekta 400 siyo kweli maana yake juzi tu Wizara ya Ardhi imepeleka kule wapimaji kwa ajili ya kurekebisha maeneo kwa ajili ya kutaka kuapatia Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha eneo la kuliendeleza pale katika eneo la bandari kavu, bado kule wamekwenda wataalam wamekwama. Kuna mizozo mikubwa, wananchi hawajaridhika, hawaelewi na wanachozungumza wao hawa wananchi ni kwamba hili shamba linatajwa kwamba ni mali ya Wizara ya Mifugo, lakini ukweli halisi kwa maisha yao yote hajawai kuona likiendelezwa wao wameishi mle kwa muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapa nilitaka niikumbushe Wizara kwamba tukukumbuke historia ya nchi yetu, maeneo mengi tulianzisha *operation vijiji*, na tulipovianzisha vijiji vile watu walienda kuingia kwenye maeneo ambayo yalikuwa wazi, leo wao wanapokwenda kumaliza migogoro kwa kutazama ramani zao za miaka iliyopita ufumbuzi unakuwa haujapatikana kwenye maeneo husika. Ningeomba Wizara ifike kwenye maeneo haya ili ikaone namna gani tunaweza tukamaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lipo tatizo la migogoro kwenye maeneo haya na ningeomba Waziri...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo dakika tano ni chache.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza na mimi kutoa mchango wangu katika Wizara ya Mifugo na Uvubi, lakini kadhalika ningependa kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake Ndugu Ulega, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika Wizara hii. (*Makofii*)

Ningependa kuwapongeza watendaji wa Wizara hii kwakweli wamefanya kazi nzuri na ndiyo maana sasa hivi maeneo mengi yameanza kuimarika hasa yale ambayo yamezalia samaki hasa katika masuala ya matumbawe au *coral leaves.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuelekeza mchango wangu katika maeneo mawili makubwa; la kwanza ni kuhusu suala la usafirishaji wa biashara ya dagaa ambayo jana nilliliza swali langu, lakini la kwanza ningependa kumpongeza vilevile Mheshimiwa Ulega kwa kweli toka jana ameanza kulifua tililia hili suala na imenitia moyo sana na huu ndiyo uwajibikaji haswa wa Serikali hii ya Awamu ya Sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza tu kwamba tuisiwategemee tu sana watendaji wetu wakati mwiningine wanakuwa wanatuangusha kwa sababu wanaporipoti inakuwa sivyo wanavyofanya, kwa hiyo nashukuru hili ambalo tulikuwa tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia ningependa tu kuwaomba wenzetu watendaji hawa wakajaribu kuwasaidia hawa wafanyabiashara na dagaa kwa sababu ni nieneo ambalo linaajiri watu wengi sana na hasa wanawake, na hivi sasa biashara hii imekuwa inafanya sana na wageni ambao wanakwenda mpaka kwenye madiko na kununua dagaa; ingekuwa vyema kama tukawapa-*incentives* watu wetu wakaweza kufanya biashara wao moja kwa moja na wakasafirsha dagaa badala ya wageni kuja moja kwa moja kwenye mwalo na kununua dagaa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ningechangia kuhusu masuala mazima ya maeneo ya mazima ya maeneo ya

mazalia ya samaki hasa masuala ya mikoko au *mangroves* yaani mikandaa kwa jina lingine. Kuna uharibifu mkubwa sana katika maeneo ya mikoko au mikandaa, ukaenda Rufiji na maeneo ya kanda mbalimbali za fukwe za bahari, mikoko imekuwa ikiathirika sana na nimaeneo ambayo ni mazalia makubwa ya samaki. Sasa hapa ningewaomba wenzetu wa uvuvi mkashirikiana na Wizara na Maliasili kwa sababu ingawa mikoko au mikandaa ni miti, lakini ni mazalio na ni malisho ya samaki.

Mheshimiwa Spika, sasa tukiwaachia wenzetu wa Maliasili peke yao, sisi tukaendelea zaidi kwenye masuala ya uzalishaji wa samaki au uvunaji na biashara moja kwa moja basi tutakuwa tunaacha eneo muhimu ambalo linaweza likasaidia. Kwenye Mradi wa *MANCEP* ulifanya kazi nzuri ya kuendeleza mikandaa, lakini Mradi wa *SWIOFish* bahati mbaya umeliacha hilli eneo haukuliedeleza, kwa hiyo hizi *resources* tunavyozipata tuangalie maeneo haya kwa sababu nayo ni maeneo muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Semesi katika mwaka 1992 alifanya utafiti wa mikoko au mikandaa na akaandaa *management plans* ikiwemo uzalishaji na ulishaji au malisho ya samaki. Lakini bahati mbaya hizi *management plan* zote ziko kwenye ma-shelf, hazikufanyiwa kazi toka mwaka 1992 mpaka hii leo. Ningombwa wenzetu wa uvuvi mkaziangalia hizi *management plans* na tukaangalia tukazi-reviewili kuona uwezekano kuziendeleza tujue tunaanzia wapi katika kuendeleza mikandaa au mikoko iwe ili iwe ni sehemu salama zaidi ya kuweza kuwasaidia kuzalisha samaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kugusia vilevile suala zima la mabadiliko ya tabia nchi. Mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri sana wafugaji na kipindi cha ukame maeneo mengi ya maji na malisho yanaathirika na kuna miradi kama Mradi wa *Decentralize Government Finance* ulianzishwa ili kuzisaidia Halmashauri kuweza kusimamia maeneo ya malisho na kuzitafuta fedha kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji. Sasa mradi ule umemalizika mpaka hii leo zile jitihada hatukuziendeleza, kwahiyoo miradi hii inakuwa

ni mizuri lakini sasa stability inakuwa haipo. Kwa hiyo ningeliomba tu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu leo hii kutujaalia tuko wazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikiwa leo tunaendelea na Wizara hii ya Mifugo na Uvubi mimi nitajikita zaidi kwenye suala la uvubi. Kwenye suala la uvubi kuna watu ambao wanajishughulisha na suala la Mwani, ingawa wachangiaji wengi hawajalizungumzia suala hili, lakini ni suala ambalo ni muhimu sana na suala ambalo ni nyeti. Ukiangalia kuna baadhi ya Mikoa Tanzania Bara na kule Zanzibar kuna Mikoa Tanzania Bara isioyopungua mitano upo Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga ndiyo mikoa ambayo imeshamiri sana katika kujikita kushughulika na suala la uvubi huu wa mwani.

Mheshimiwa Spika, lakini bado sijaona mipango mikakati kupitia Wizara hii mbali na ripoti ambayo imewasilishwa hapa mezani, bado sijaona fungu la fedha au mikakati yoyote ambayo Wizara imejikita kwa ajili ya kunusuru hili zao la mwani. Miaka ya nyuma mnamo mwaka 1980 zao hili la mwani lilishamiri sana lilipoletwa Zanzibar na tukafanikiwa kwa muda wa miaka 10 na ikaonekana Zanzibar ambayo kiujumla ndiyo Tanzania ikaonekana kama nchi ya Tatu katika kufanikiwa katika kulipanda zao hili la mwani.

Mheshimiwa Spika, lakini mnamo mwaka 1990 na kuendelea zao la mwani hili likaendelea kulimwa huku Tanzania Bara, na wengi wao walikuwa wanapanda huu mwani ni wakinamama. Ukiangalia asilimia 90 ya kinamama ndiyo washughulikaji wakubwa sana wa zao hili la mwani, miaka hiyo ya nyuma mwani ilikuwa ina *value* kubwa sana na ulikuwa una faida kubwa sana, lakini cha kushangaza baada ya mwaka 2010 na kuendelea zao hili la mwani halina thamani hata kidogo, mbali na gharama kubwa sana za wavuvi hawa wa mwani walotumia kwa ajili ya kulikuza hili zao la mwani na matokeo yake kupata faida gharama kubwa sana ambazo wanazitumia, sijaona mpango mkakati wa kunusuru zao hili mwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingawa Tanzania inatajwa ni nchi ya tatu baada ya Uphilipino na Indonensia katika kuongoza zao hili la mwani. Kwa hiyo nalomba sana Wizara, naiomba sana kuititia Wizara hii ya Mifugo na Uvvi iende ikaangalie na kunusuru zao hili la mwani, tukiangalia Zanzibar wamejaribu kutumia mbinu tofauti tofauti kwa ajili ya kunusuru zao hili la mwani, wameanzisha makongamano mbalimbali, kutafuta wawekezaji bado changamoto kwenye soko, lakini bado kwa Tanzania Bara inaonekana kwamba zao hili halijapewa mkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana ndugu yangu Naibu Waziri ingawa ni mmoja ambaye unafuatilia sana suala hili la mwani na kufuatilia sana, lakini bado sijaona mikakati ingawa mwaka jana mlitenga zaidi ya shilingi milioni 41, lakini fedha mlizozitowa ni shilingi milioni 14 kwa ajili ya kununua kamba, lakini mwaka huu sijaona kabisa, sijaona kabisa fungu la fedha ambalo limetengwa kwa ajili ya kunusuru zao hili la mwani. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara hii mtenge fedha kwa ajili ya kunusuru zao hili la mwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia la pili tutafute wawekezaji kutoka nje, tusing'ang'anie wawekezaji hawa tuliokuwa nao sasa hivi, lazima tufungue *forum* ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kunusuru zao hili; asilimia 90 ya kinamama ndiyo

wanajishughulisha na zao hili la mwani. Najua tukisema tunaendelea pia tunawadharau na bei ndogo ya soko tunaenda kulididimiza zao hili la mwani.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukiweka mpango mikakati mizuri zao hili linaweza likainuka na tukarejea kwenye *top one* ile ambayo tayari kidunia zao ili la mwani Tanzania miaka hiyo, basi tukaweza kuirejesha ndani ya miaka hii. Mimi ninaamini ndugu yangu Abdallah Ulega bado ujachelewa na ninaamini maarifa mengi na unauwezo mkubwa sana kwa ajili ya kunusuru zao hili la mwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tusiishie hapa tu tunao ndugu zetu wa Zanzibar, kwa nini tusishirikiane kwa pamoja kwa sababu ni suala la kutafuta soko nje ya nchi ni suala la Muungano, Katiba imezungumzia ibara ya kwanza na ya pili kwamba tunapokwenda nje kule tunakuwa kitu kimoja tukaazisha angalau japo makongamano kwa mfano kama tukianzisha masuala ya *Seaweed Vast Value Tanzania* tunaweza tukanusuru zao hili la mwani na mwisho wa siku tukavutia wawekezaji na zao hili likaleta tija ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa kweli kwenye hotuba yake

nimepita nimeona miradi kadhaa wameweka kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Hai, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nianze kwa kuchangia kwenye eneo la Vyama vya Ushirika Maziwa na hapa niwapongeze sana wenzenetu wa Vyama vya Ushirika ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro, lakini hususani Jimbo la Hai wanafanya vizuri sana na wanafanya vizuri kwa sababu wamejiratibu vyema na sasa hivi tuna mradi wa kutengeneza chakula cha mifugo pale Uduru ni kwa sababu ya ushirika mzuri; huko haufanani na kule kwingeine nilipokua napigia kelele, lakini hapa wanafanya vizuri sana.

Nimuombe Mheshimiwa Waziri tafadhali tusaidie kuratibu vyama hivi vya ushirika kwa sababu viko tofauti tofauti vikae pamoja na wawe na mipango ambayo inatuwezesha kuwa wamoja, kama wakiweza kuunganisha nguvu yao tunaweza tukapata kiwanda cha maziwa na bahati nzuri walishaanza mchakato wa kutafuta eneo la kujenga kiwanda cha maziwa. Kwa hiyo, mtusaidie kuwa *coordinate* vizuri ili wawe na mpango uliofanana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye ushirika huo kumekuwa na changamoto kwa sababu hawajakaa pamoja kwa hiyo vyama viko *scattered*, Mheshimiwa Waziri labda nikueleze kidogo namna ambavyo sisi tunafuga; katika Jimbo la Hai tuna ufugaji wa aina mbili tofauti, tuna wafugaji wa Kata hizi za upande wa Kaskazini wanafugia ndani. unakuta mwananchi ana ng'ombe wake wawili/watatu anawafugia ndani, kwa hiyo unalazimu kuwa tafutia chakula na madawa kwa kuwaleta ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini upande huu wa tambarare wananchi wanafuga kwenye jamii ya Wamasai kwa kutafuta malisho. Sasa changamoto zao kubwa hasa sasa hivi wale ng'ombe ambaeo wanafugiwa ndani ni wale ng'ombe wa kienyeji.

Sasa niwaombe sana mtutafutie namna ambavyo tunaweza kupata mbegu mpya kwa sababu tunapata shida

sana sasa hivi hata kupandisha wale ng'ombe, mwananchi ili aweze kupata mbegu ya kupandishwa ng'ombe anahitaji shilingi 20,000; hii ni changamoto kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, lakini pia analetewa mtaalamu anakuja kubandisha ng'ombe huyo anapandisha zaidi ya mara tatu/mara nne na hiyo shilingi 20,000 ni kwa wale ambaao wako karibu na mjini; vijiji kama Ng'uni ambavyo viko nje ya mji kidogo wanakuwa-*charged* mpaka shilingi 50,000 kuweza kupandishiwa ng'ombe mmoja. Kwa hiyo niombe kwa sababu wenzetu wa Tengeru wapo pale karibu na Arumeru, basi tuleteeni mazingira haya yawe rafiki na ikiwezekana mtuletee mbegu ambazo zinaweza kufugika ambazo tunapata maziwa ya kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto nyingine kwenye vyama vyetu hivi nya ushirika; maziwa tunayoya kutosha na niwapongeze sana wenzetu wa kule Mronga kwa kweli chama kile kimejii marisha vizuri, wamefika mahali mpaka wameweza kutengeneza kiwanda kidogo cha kuzalisha maziwa, kule Mronga na kule Ng'uni wamefanya vizuri sana. Sasa tunafikiria badala ya kuendelea kufanya vyama vidogo vidogo waungane pamoja tujenge kiwanda kikubwa na kizuri na pale Uduru wenzetu wa Tanga *Fresh* walikuwa wameweka *cooler* yao wanakusanya maziwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na changamoto, hawa wakusanya maziwa wamekuwa wengi sana, tunaomba sasa tutafute namna ya ku-centralize awe mkusanyaji mmoja ili tuweze kuuza kwa tija. Sasa hivi huku mtaani wanununa shilingi 700, lakini ukiangalia kwa bei ya soko tuna uwezo wa kununua lita kwa shilingi 1,000 kama watakaa pamoja ikiwa ni pamoja na kupata wataalamu. Tunayo shida sana ndani ya Wilaya ya Hai wataalam tulionao hawatutoshalezi. Lakini kwa upande wa tambarare huku bado kuna shida tunahitaji wataalam wa kuwafundisha ndugu zangu na bahati nzuri mimi ni Laigonan nilipewa hishima hiyo na ndugu zetu Wamasai, sasa nina kazi ya kuwalea vizuri ili tufuge kwa faida.

Mheshimiwa Spika, mimi siyo muumini wa kupunguza mifugo, mimi ni muumini wa kuongeza, lakini tufuge kwa tija na maeneo tunayo tukifunga vizuri pamoja ya kwamba eneo lile la KIA lina mgogoro wa aina yake, lakini bado tunaweza kujipanga vizuri kama tutapata wataalamu. Lakini tunayochangamoto ya kuwa na majosho ya kuweza kuwahudumia wanyama wetu, niombe sana yale yalioko pale mengi yamekufa, hatuna hata moja linalofanya kazi.

Kwa hiyo, niombe na nimejaribu kupita kwenye bajeti yako sijaona jambo hili Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba nilikuandikia, sasa nikuombe sana utusaidie maeneo yale ya wafugaji upande wa tambarare waweze kupata maeneo ya kulishia, lakini pia waweze kupata majosho ili waweze kufuga kwa kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa tunalohitaji upande ule ni elimu wapewe elimu kwa sababu ng'ombe ni *deal*, ukianza ngozi yake, ukienda maziwa, sasa tunafuga kwa upande wa tambarare tunajikita sana kwenye upande wa nyama maziwa tumesahau...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Hhayuma*.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

**SPIKA:** Ni dakika tano pia.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** ...niweze kuchangia kwenye sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ninaweza kuzungumzia kwa wavuvi wadogo wadogo. Kwenye Jimbo la Kawe ninapotoka wavuvi wadogo wadogo wapo kwenye kata ya Kunduchi na Kata ya Mbweni, lakini wanachangamoto, changamoto yao kubwa ni Sheria ya Uvuvu ambayo inawabana. Wavuvi hawa wanatakiwa wakiingia majini waingie mita 50, mita 50 kwenye kina ni unatoka Kunduchi una fika Unguja ndiyo unakuta hichi kina. Kwa hiyo, wanapata hii changamoto, lakini wana miundombinu hafifu, wanakuwa na bodi, zile boti *engine* yake ndiyo unashikia mkononi. Kwa hiyo, mawimbi yakimkuta katika ya bahari anazama na kupoteza maisha tuiangalie hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ushirikishwaji katika utungaji wa sheria tunaomba wavuvi hawa wadogo wadogo washirikishwe kwa sababu kwenye taarifa zetu, wavuvi wadogo wadogo wanachangia asilimia 98 ya pato la sekta hii, kwa hiyo, tuwaangalie kwa uwangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, changamoto zote wavuvi hawa wameweza kuvuna wastani wa tani 350 za samaki kwa mwaka hichi ni kiwango kidogo ukilinganisha na jinsi gani tulivyo na maeneo yetu, hiki ni kiwango kidogo na kwa sababu ni kiwango kidogo samaki hawatoshelezi kwa soko la ndani. Imelazimisha Serikali kuagiza samaki kutoka nje, samaki zinaagizwa tani 24 kutoka nje ambapo ni sawa na dola za Kimarekani milioni 25 uki-*calculate* kwa pesa ya Tanzania ni shilingi bilioni 690,000 kwa mwaka. Pesa hii ni nyingi na inakwenda nje kwa sababu sisi hatuna nyenzo za kutosha kusaidia wavuvi wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu kwa sababu naona Waheshimiwa Mawaziri ni wasikivu na wanachukua kwa sababu tunapokwenda ni kuzuri, walikuwa wanalamika nyavyu zinachomwa lakini sasa hivi elimu naona inafika na nyavyu hazichomwi na sasa hizi milimita 16 imeshaeleweka kwa wavuvi. Kwa hilo, nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini nishauri pia tujue idadi halisi ya wavuvi wetu hili tuweze kuwasaidia wavuvi, wanalamika

hawasaidiki kwa sababu hawakopesheki, hatujui hata idadi yao, hatuna jinsi ya kuwasaidia kuweza kupata nyenzo nzuri na thabitii za kuweza kuingia majini.

Niombe Mheshimiwa Waziri unapokuja ku-*wind up* uweke vitu muhimu na *facilities* ambazo zitasaidia hawa wavuvi waweze kuingia kwenye *deep sea* bila ya kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, lakini niombe kwa sababu sekta hii ni muhimu sana, tunaweza kutanua wigo, tutanue wigo wa wawekezaji; wenzangu wamesema tutanue wigo kama tunaona tunafika hapa tunaweza kupiga hatua 100 mbele, tutanue wigo, tutafute wawekezaji waweze kuwekeza kwenye hii sekta, tuna utajirisho wa kutosha. Tukiweza kuweza vyta kutosha sekta hii inaweza kuwa ya kwanza kwa kuingiza pato la Taifa. Inaweza kuwa ya kwanza kuajiri vijana wetu. Niki-refer kule nyuma kwenye Mpango wetu wa Pili wa maendeleo tuli-*target* mpaka mwaka 2020 asilimia 4.6 ichangie pato la Taifa sekta hii kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, lakini hatukufika kwa sababu hatuna nyezo kwa hiyo hatuna nyenzo, mafunzo na hatuna vifaa muhimu, lakini mpaka 2019/2020 ni asilimia 24 tu ilitengwa katika sekta hii ya uvuvi. Kwa hiyo twende tukapitishe bajeti na itekelezwe ili tuweze kwenda kusaidia watu wetu sekta hii imeajiri vijana, vijana wengi wamekwenda hawana elimu, wapate elimu ya kutosha, lakini tutapata pato la Taifa, tutapata ajira za kutosha, tutapata mapato ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa sababu muda ni mchache, nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante kwa kutumia muda vizuri.

Mheshimiwa *Engineer Hhayuma* atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Khamis Mborouk. Wote wawili hawapo Mheshimiwa Amour, tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi; cha kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo ameiwasilisha, lakini kubwa ambalo nataka nzungumzie sehemu mbili; nataka kuzungumzia kuhua *NARCO*, lakini pia nzungumzie kuhusu Bodi ya Maziwa ambayo hiko chini ya Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia kwanza kuhusu Bodi ya Maziwa na mimi kule Makete nina shamba la Kitulo ambalo ni shamba bora na ni shamba zuri ambalo Wizara yenye we inalismamia kwa sababu liko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Shamba lile juzi wakati nauliza swali hapa walini jibu kwamba Wizara inatenga kununua mitambo mitano ili kuliwezesha lile shamba kuendelea na uzalishaji wa maziwa. Mimi nisema jambo moja Wizara ninawaomba na ninawashauri uki langalia hapa kwenye matumizi ya fedha ambapo tunazitumia kuagiza maziwa nchini ni zaidi ya shilingi bilioni 30 tuna agizwa kutoka nje kuleta kutoka nje kuleta ndani ya Tanzania, lakini Makete tuna shamba la Kitulo ambalo ng'ombe mmoja tu ana uwezo wa kutoa lita 50 kwa siku; je, Serikali haioni haja ya kuwekeza kwenye shamba lile ambalo kwa muda mrefu limekuwa likizorota, sasa hivi liko katika hatua ambayo kwa kweli haipendezi lakini eneo ni kubwa lipo.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Wizara ili kukimbizana na hili jambo la maziwa njooni Makete kwenye shamba la Kitulo muwekeze. Wana Makete wako tayari wawekezaji wako tayari mfanye *partnership* na watu ili uweze kuwekeza tuwape maziwa ya kutosha, kwa sababu ukisoma kwenye hotuba ya waziri anazungumzia kwamba wanahitaji kuongeza vituo karibu 50 vya ukusanyaji wa maziwa nchini. Mnakusanya maziwa kutoka wapi wakati hamna mpango wa mkakati mzuri wa kuhakikisha mashamba haya ya Serikali ya uzalishaji wa maziwa yanatoa maziwa vizuri na naomba kwamba idadi ya ng'ombe waongezeke pale Kitulo.

Mheshimiwa Spika, lakini miundombinu ya shamba lile iongezeke, lakini pia maslahi ya wafanyakazi pale Kitulo

yaboreshwani ili lile shamba liweze kufaidisha Watanzania wetu, lakini Wanamakete wenzetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ambalo jana Mheshimiwa Spika jana alizungumzia, suala la *NARCO* lisiwe tena mjadala Wizara ni lazima iende ijithathmini jinsi ya kuipa majukumu mapya *NARCO*.

Mheshimiwa Spika, na uzuri ni kwamba mnasehemu ya kuanzia kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri nilizungumza Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2002 Waraka Namba 2 walionyesha kabisa kwamba *NARCO*kuna mambo ambayo wameshindwa, kuyafanya ni vema Serikali ikaingia sasa mkakati wa kuwapa *private sector* maeneo yale muweze kuyasimimamia na kuyaendesha.

Lakini pili nikazungumzia kwamba kwenye kikao cha Waziri Mkuu cha tarehe 26 Februari, 2016 pale Kagera na bahati nzuri na mimi nilikuwepo kwenye kikao hicho, Waziri Mkuu aliagiza akasema kubainisha mpango bora wa matumizi ya ardhi ya *NARCO* ili kama Serikali haina uwezo wa kuendesha tujue ni nani aweze kupewa mashamba hayo. Waziri Mkuu alitoa hapa mna sehemu ya kuanzia na Waziri Mkuu alikuwa ni huyu Kassim Majaliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe watu wa Wizara ya Mifugo *NARCO*ibadilishieni majukumu ya kazi ili maeneo yale ambayo Spika mwenyewe ameyazungumzia kwamba yamebaki wazi muda mrefu, Watanzania na vijana wa Kitanzania waweze kupewa na Wizara iweze kuwasimamia mashamba yale yaweze kuendeshwa, kwa sababu ukiangalia Kagera tu ina ranchi karibu nne, *NARCO* kazi wanayoifanya kule Kagera ni kutatua migogoro, hawajikiti kwenye kutatua suluhisho la hizi ranchi ziwezekufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, leo hii *NARCO* wanakuja na mpango wa mkakati wa kwamba Mtanzania awekeze kwa mkataba wa mwaka mmoja, hata mimba yenye ya huyo ng'ombe ndani ya mwaka mmoja haiwezi ikawa amepata

mimba jamani, tusema jambo jema muwe na vitu vyenye tija kama Wizara kusaidia wananchi wetu utawekaje mkataba mwaka mmoja mtu akaweke uwekezaji pale, ongezeni kwenye majukumu kwenye *NARCO* iweze kufanya kazi ambayo sisi watanzania tutaona ina tija.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusisitiza pia kwamba *NARCO* wenyewe watambue kwamba ule Mradi wa Ruvu na mtupe majibu leo hii hapa, Serikali mradi wa Ruvu wa shilingi bilioni 5.7 kwa nini hadi leo umelala huko kwenye *coma*, uko *ICU*, haujawahi endelea zaidi ya miaka kumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba muendelee kutupa majibu hayo ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simoni Songe atafuatiwa Mheshimiwa Janejelly James na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi hii nami nichangie Wizara hii ya Mifugo na Uvuuvi, lakini kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanafanya pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, leo nataka kuchangia tu mambo mawili katika Wizara hii ya Uvuuvi. Hapa nyuma kidogo tumekuwa na wimbi kubwa la upungufu au uhaba wa samaki viwandani, leo nataka niishauri Wizara jambo mojawapo ambalo linalosababisha kuwa na uhaba wa samaki katika viwanda yetu.

Mheshimiwa Spika, ijulikane ya kwamba tuna samaki aina ya sangara hasa kwenye Ziwa letu la Victoria na samaki huyu kwa kilo moja anauzwa shilingi 9,000 mpaka shilingi

10,000 pale Mwaloni. Sasa chukulia samaki wa kilo tano kwa shilingi 9,000 atauzwa shilingi 45,000; lakini ijulikane ya kwamba bondo ndani ya ile samaki ndio lenye samani kubwa kuliko mnofu. Sasa wanapokuwa wanaiza pamoja na bondo lake kwa shilingi 9,000 na akipeleka kiwandani atauza kilo moja kwa shilingi 12,000 ina maana kwa samaki mwenye kilo tano atamuza shilingi 60,000; lakini bondo linauzwa zaidi ya shilingi 60,000 samaki mwenye kilo tano.

Mheshimiwa Spika, sasa mvuvi amekuja na *option* ambayo ni ya kawaida tu kwamba badala ya kumpeleka yule samaki kiwandani bora mnofu wake awauzie wananchi halafu ye ye anufaika na lile bondo. Anajikuta kwa wananchi anaweza kumuza yule samaki wa kilo tano mpaka shilingi 40,000 mpaka shilingi 50,000 na bondo pia akaiza kwa shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, hapo atajikuta ameingiza shilingi laki moja kwa samaki mwenye kilo tano, lakini atakapompeleka kiwandani atamuza kwa bondo lake kwa shilingi 60,000 hata ningekuwa mimi nisingeweza kupeleka samaki yule kiwanda.

Sasa mimi niishauri Wizara, waruhusiwe wavuvi au wafanyabishara ambao wanapeleka samaki kiwandani basi kuwepo na thamani ya mnofu na thamani ya bondo liuzwe peke yake, hii itasababisha kunufaisha huyu mvuvi kwa sababu thamani ya samaki itaongezeka, na kama hazitafanya hivi maana yake wataendelea hao wavuvi kutaka samaki vipande vidogo vidogo, wanawauzia wananchi na viwanda nyetu vitaendele kuwa na uhaba kama ambavyo imeonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ijulikane ya kwamba matumizi ya ndani yameongezeka ya watumia samaki kama kitoweo hata marafiki zangu hapa Wagogo wanataka samaki kutoka Ziwa Victoria kule Usukuman, sasa ni lazima tu viwanda vikose samaki. Kwa hiyo mimi niishauri Wizara kwamba pia lazima tujikite sana kwenye mabwawa ili

tuendelee kupata samaki wengi na hawa samaki waweze kutumika katika matumizi yale ya kawaida ya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kupunguza ukiritimba hawa wawekezaji wanapokuja kwa ajili ya vizimba, ukija na kizimba utapewa masharti makubwa, tafute eneo kijijini, nenda katafute kibali, lete mtu wa *TAFIRI* aje apime, huu mlolongo unasababisha wawekezaji wanaondoka; nilitamani sana Wizara iliangularie hili ili mwisho wa siku tuwe na malighafi ya kutosha kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo nilitaka kushauri ni tozo kwa wavuvi; kuna tozo nyingi hapa kwa wavuvi kuna tozo inayotozwa na *TASAC* ambao wanakuja kukagua ubora wa mtumbwi wanatoza shilingi 70,000.

Mheshimiwa Waziri umefika pale kwangu ulikuja wananchi walikulalamikia na ulisema utalishulikia hili lakini bado halijashughulikiwa bado wanatoza shilingi 70,000 kukagua ubora wa mtumbwi. Sasa hapa wananchi wangu wameniuliza swali ndogo sana kama leo mtumbwi ni mpya unakuja kukaguliwa nalipa shilingi 70,000 wakati ni mpya wala haujatumika, sasa wanakagua ubora upi wakati bado ni mpya.

Mheshimiwa Spika, hili swalii ni *very technique* kidogo, mimi niishauri Wizara kwamba wananchi wetu hawajakataa kulipa, lakini wanaona shilingi 70,000 ni kiwango kikubwa sana ukilinganisha na kazi ambayo inakuja kufanyika. Kwa hiyo niiombe Wizara iweze kuliangularia hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tozo kama leseni ya mtumbwi inayotozwa na halmashauri shilingi 30,000 lakini pia kuna leseni kwa mvuvi mmojammoja shilingi 20,000 hapa pia na penyewe nilitamani sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja, lakini tuangalie bei ya samaki ukilinganisha na bondo. Ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Saimoni Songe siku nyingine utuletee samaki wa Ziwa Victoria bwana, hata Wagogo tunakula.

Mheshimiwa Janejelly James atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ataniwezesha kuchangia ninayoenda kuchangia.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na niwapongeze kwa kazi wanayofanya, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Lakini pia naungana na Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo asilimia 100 kwa yale yote ambayo wameshauri.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nijikite kwenye bajeti inayotolewa kwenye Wizara husika. Ukingalia bajeti iliyoletwa mbele yako kuombwa hapo bajeti ya Wizara yote ni shilingi 199,194,996,810; lakini uvuvi peke yake imepewa shilingi 122,350,470,000; mifugo imepewa shilingi 47,844,949,810.

Mheshimiwa Spika, ukitafuta *percentage* uvuvi wamepata asilimia 71.7; mifugo wamepata asilimia 28.3; ukiliangalia kwa macho ya kawaida uvuvi inaimeza mifugo, lakini hapa tunasema asilimia 60 ya Watanzania wako kwenye kilimo, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Spika, lakini Idara moja ya Mifugo imemezwa na uvuvi, hapa watatokaje? Hatuwezi tukaona utendaji ulio bora kwenye mifugo lakini pamoja na bajeti hiyo kuwa ndogo, inachelewa kupelekwa kwenye Wizara na inapelekwa kwa asilimia ndogo sana, lakini tunataka mifugo na uvuvi viendelee. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge wa muda mrefu ndani ya Bunge hili, unakumbuka historia nyuma Wizara ya Maji, Nishati na Madini zilivyokuwa pamoja, Idara ya Madini ilikuwa inazimeza Wizara zingine idara zingine hazikuonekana kabisa zilichokuwa zinafanya. Lakini kwa makusudi ya ushauri wenu kama Bunge mkashauri Wizara zikatoka tatu mle; ikatoka Wizara ya Maji, Nishati na Madini na mafanikio tumeyaona. Mimi niombe tu kwa kiti chako Mheshimiwa Balozi juzi alichangia akasema Bunge la Kumi na Mbili nasi tutoke na alama kwenye kilimo, uvuvi na mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuishauri Serikali isiangalie gharama ichukue maamuzi magumu ya kuzitenga hizi idara mbili; uvuvi iwe na Wizara yake na mifugo iwe na Wizara yake. Baada ya kulifanya hilo utendaji unaweza ukaonekana. Kwa kweli Waziri akiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi mtu mmoja ni pasua kichwa, kwa sababu anagusa maisha ya wananchi chini kabisa kila Mtanzania anamgusa, lakini anamgusa kwa mazingira magumu sana ya bajeti kutotosha na ya kwamba kila mwananchi anatakwa aguswe. Lakini hapo hapo idara moja inapewa hela kidogo, idara nyingine inapewa hela kubwa, ni ngumu sana kufanya kazi kwenye mazingira hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pili nishauri kwenye uvuvi; niliwahi kusema kwenye Mpango wa Maendeleo kwamba Tanzania tumebalikiwa kuwa na maji ya kutosha, maziwa, bahari na mito lakini bado hatujawekeza kwenye uvuvi bado hatujajikita kwenye uvuvi. Leo hii kama Serikali ikichukuwa makusudi mazima kujenga vizimba kila maziwa yetu, wakawapa wananchi hata kwa kukodisha, tukawekeza mapato yatapatikana, ajira zitapatikana na uvuvi utaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly Ntate kwa kweli *analysis* yako ni kubwa tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Askofu Josephat Gwajima.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, muda ni mchache sana, lakini napenda kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Tanzania tumebarikiwa madini ukiacha madini, kuna maliasili na utalii lakini kilimo kwa maana kilimo chenyewe, mifugo na uvuvi. Natambua kabisa Rais wetu Mama Samia amewachangua Waziri na Naibu Waziri *strategically*, Waziri anatoka kwenye jamii ya wafugaji na Naibu Waziri anatoka kwenye jamii ya uvuvi.

Kwa hiyo, tunatarajia kuona matokeo chanja na dhamira ya dhati ya mama alivyokuwa anahutubia Bunge hapa *lime-reflect* kwenye bajeti ya mwaka huu ambapo ametenga kweli fedha za maendeleo shilingi bilioni 99 sasa kutenga ni kitu kimoja na utekelezaji ni kitu kingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti umekuwa ukisausua mathalani mwaka 2016/2017 bajeti iitengwa lakini zilienda asilimia 3.25 mwaka 2018/2019 bilioni nne lakini hawakwenda chochote kile na 2018/2019 ilienda asilimia 39 tu. Bajeti ya maendeleo ikitelezwa vizuri ina maana Wizara hii itaenda kufanya tafiti za kina kuweza kugundua fursa mbalimbali, kuweza kugundua mbegu mbadala matharani kwa kuwa na ufgaji wa tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maana yake najua Tanzania tuna ufgaji wa asili na huu wa ranchi ambao huu nao unasuasua, ufgaji wa asili wapo wale ambao wapo awalimi wanafuga tu na wengine tunalima na kufuga kwa maana ya *agropastoral* kama sisi hapa Wakurya tunafuga na kulima. Sasa mkiweza kugundua kwa kiwango kikubwa ambacho cha mifugo tulichonacho lakini tija ni ndogo sana na ukafanya tafiti ya kina kuweza kugundua tatizo ni nini, tutaenda mbali.

Mheshimiwa Spika, ufugaji na uvuvi ni sekta ambayo ikiwekezwa kwa kina kabisa tutaenda kupata pato kubwa sana Taifa na shilingi bilioni 23 kwa maana mifugo shilingi bilioni 10 na uvuvi shilingi bilioni 13 mmepeleka shilingi bilioni 11 tu. Lakini makusanyo ni shilingi bilioni 51; sasa mnakusanya shilingi shilingi bilioni 51 mnashindwa vipi kuwekeza shilingi bilioni 23 ili tija iongezeke maradufu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama hata Kamati iliyoshauri kwamba wadau mbalimbali wanalamika kuwa sera, sheria na kanuni zimepitwa na wakati, ifanyike *review* twende na ufugaji wa kisasa. Hata kama Ranchi ya Taifa ambayo ni asilimia tano ya uwekezaji katika mifugo tulionayo nayo inasuasua yaani *capacity* ni ng'ombe 80,000 mpaka 90,000 mpaka sasa ranchi zetu za Taifa kulingana na takwimu zilizopo 12,000 na ... ni bora tufanye ugawaji mzuri wa ardhi, tutafute na tuvutie wawekezaji, tutoke kuwekeza kwa *government* iende kwenye sekta binafsi. Wawekezaji waje wengi ili sasa hata tuweze kupata na masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye mazao ya mifugo, nyama tuna viwanda 25 lakini *capacity* yake ni kuweza kuchakata kilo 627,000. Lakini sasa hivi wanafanya *under capacity*, kilo 81,000 tu. Tatizo ni nini; labda teknolojia imepitwa na wakati, labda kuna *factors* nyingi, lakini tukiwekeza tukafanya tafiti tutagundua na tuweze kuwekeza kwa kina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hata tunapopeleka nje, yaani tuna-*export* tani 2,000 na tuna-*import* tani 2,000. Lakini tunazozi-*export* zinakuwa na bei ndogo kuliko zile ambazo tuna-*import* sisi, *what is this?* Tuangalie ubora wa nyama zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata ukija kwenye zao la ngozi utaona ngozi zetu za kondoo, ng'ombe, mbuzi, hazipati *markethuko* nje na sababu ni nyingi. Tumesema hata upigaji chapa, maeneo ya machinjio, makaro yenye we na kila kitu, ni wakati hata wa kuwekeza kuhakikisha kwamba walau katika kila Wilaya au Majimbo yanakuwa na machinjio ya

kisasa kama ambavyo mmewekeza kule Dar es Salaam.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Spika, kwenye maziwa sasa ndiyo unaweza ukalia, yaani hapa ninyi mna-document kwamba tunazalisha maziwa bilioni 2.7 kwa mwaka na target ni kufika bilioni nne, lakini uchakataji wa maziwa ambayo yanazalishwa ni *two percent*. Na mbaya zaidi kwa mfano mwaka 2018/2019 Serikali mmetoa vibali 417 vya kuingiza maziwa kutoka nje ambapo zilitumika zaidi ya bilioni 22 na kitu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, hizi bilioni 22 na kitu zingetumika kuboresha viwanda vya Tanzania na kujenga viwanda vingine ili waweze kuchukua haya maziwa tungeweza kutoa fedha nyingi kwa hawa wafugaji na kutoa ajira nyingi hapa Tanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, Mnada wa Magena kabla sijasahau; pale Magena tuna mnada wa kimkakati ambao ng'ombe wengi wamekwenda Kenya kutoka Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara. Na tukifanya mnada ule wa Magena pale tutapunguza wizi wa mifugo kutoka pale Tarime.

Mheshimiwa Spika, wewe ni mwenyeji pale, unajua, ng'ombe wanatoka Rarya, Serengeti kuja pale wanakwenda Maabera, Kenya, lakini sasa hivi ukiuza ng'ombe kule unachukua hela za Kenya, inabidi ubadilishe upate hela za Tanzania. Lakini ukipeleka ng'ombe umetoka Simiyu au Mara kupeleka Kenya, ikifika jioni ng'ombe wa laki saba utauza laki tatu kwa sababu uko Kenya ili uweze kurudi Tanzania. Tunapoteza fedha nyingi sana za mapato. Tunaomba Serikali ifungue ule mnada wa Magena kwa maslahi mapana ya uchumi wa Wanatarime, Mara na Taifa kwa ujumla. *(Makof)*

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nitaandika mchango wa maandishi, muda ni mchache sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Askofu Gwajima simuoni, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Uko wapi?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Haya, changia huko uliko.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ni ufupi tu ndiyo umekufanya usinione. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Mashimba Ndaki ambaye ni Waziri wa Wizara hii pamoja na rafiki yangu, Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara hii. Ingawa siku ya futari ya Waziri Mkuu alisoma Dua mbaya mvua ikanyesha tukashindwa kula vizuri futari, lakini namshukuru hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kawe, jimbo lile limezungukwa na Bahari ya Hindi. Kata za Msasani, Kawe, Kunduchi, Mbweni, Mikocheni na Bunju zote hizi ziko kati ya Bahari ya Hindi na kwa sababu hiyo, kwa uzito sana nalazimika kuchangia hii hoja ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama yalivyo majimbo mengine ambayo yana shughuli kubwa za kilimo, ndivyo ilivyo katika Jimbo la Kawe, shughuli kubwa ya wenyeji wa eneo hilo hasa

wale wazawa wanaoishi mwambao wa bahari ni uvuvi. Kwa hiyo, huwezi kuwatenga na uvuvi; ili wale, wanywe, wasomeshe watoto, wajenge nyumba au wafanye shughuli yoyote, maisha yao ni uvuvi. Kwa hiyo ninapojadili kwa habari ya uvuvi kwenye Jimbo la Kawe, ni uti wa mgongo wa wenyeji wa Jimbo la Kawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilipofika ofisini kwake kwa sababu kule Jimbo la Kawe tulikuwa na shida ya uvuvi, wavuvi walikuwa wamezuiwa kutumia *ring net* wakati wa mchana, kwa hiyo, wavuvi wengi walikuwa wameshindwa kuvua kabisa kwa sababu uvuvi wao wanahitaji kuvua mchana na ili kuvua mchana wanahitaji kutumia *ring net*.

Mheshimiwa Spika, lakini nikafika kwenye ofisi ya Waziri pamoja na Nailbu wake, nikazungumza nao na wakaagiza kwamba wavuvi wote wa Jimbo la Kawe waachwe watumie *ring nets* mchana wakati Serikali inaendelea kutafakari sheria hiyo na leo wavuvi wangu wanaendelea kufanya vizuri, wanaendelea kuvua murua kabisa, nimshukuru kwa sababu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ile sheria ambayo tulijaribu kui-*discuss* na Naibu Waziri pamoja na Waziri ya kwamba wavuvi wanatakiwa kuvua kwenye mita 50 chini. Mimi ni mdau wa *aviation*, kwenye *aviation* kuna kitu kinaitwa *transponder* ambacho ni chombo chenye uwezo wa kuangalia kina cha maji, nimesafiri siku moja pamoja na meli kutokea Dar es Salaam kwenda Zanzibar tukiwa na chombo hicho kinaitwa *transponder* ambacho kinaangalia kina cha bahari kutokea kwenye *surface* ya bahari mpaka chini.

Mheshimiwa Spika, kusafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Zanzibar, kina kirefu kuliko chote tulichokipata ni mita 52. Sasa ni ajabu kweli mtu akisema wavuvi wavue kina cha bahari mita 50, maana yake wasafiri kwenda mpaka zaidi ya Zanzibar wakawapate hao samaki, hicho kitu hakiwezekani na kama Waziri akiendelea nacho, basi nitamuondolea shilingi kwenye bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru kwa sababu nilipofika ofisini kwake nikajadiliana na yeye akasema kwamba wavuvi waendelee kuvua mahali ambapo wanataka kuvua mpaka hapo Serikali itakapoangalia namna ya kuitengenezea hii sheria mchakato mzuri ili watu waruhusiwe kuvua na wawe na maisha salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri Wizara hii, katika nchi zinazozungukwa na bahari duniani kama ilivyo Japan na nchi zingine, uvuvi pamoja na shughuli za bahari ni ajira kamili inayowasaaidia wananchi kupata mapato yao. Kwa mfano, kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tumesema kwamba *tuta-create* ajira milioni nane, na kama Wizara hii itakuwa na ubunifu wa kubuni na kuikuza *industry* ya uvuvi kwenye maeneo yetu ya Jimbo la Kawe na sehemu zingine, inaweza kuchangia sehemu kubwa sana kwenye kutengeneza ajira za kutosha na kufanya hizi ajira milioni nane zilizoahidiwa na Chama cha Mapinduzi zitokee mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuongeza pato la Taifa, ni muhimu sana kama Serikali ikiwekeza si tu kwenye uvuvi, bali kwenye michezo ya bahari pia na shughuli mbalimbali za bahari na kuitumia bahari sawasawa. Hili linaweza kutusaidia sana kuongeza pato la Taifa na hapo hapo kuwasaidia wavuvi wetu kupata fedha ya kutosha na wakati huo huo kuisadia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima. Mlipokuwa mjisema kwamba kina kirefu kati ya Dar es Salaam na Zanzibar ni kama mita 50 hivi, nilikuwa naangalia pale juu pale hadi hapa chini, hapa si *fifty meters?* Haifiki eeh?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, haifiki hapo, hapo inaweza kuwa 38 hivi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** *Point* yangu ni kwamba inaelekea siyo mbali sana, inaelekea Dar es Salaam – Zanzibar kina cha bwawa tu kama la Hombolo pale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara hii wote wawili pamoja na Wakurugenzi kwenye Wizara hii. Mimi nimefanya kazi nao na nime-*interact* nao, watu hawa ni watu makini sana na iwapo Bunge lako litawashauri vizuri, tutapata mapinduzi makubwa sana kwenye sekta hii, hiyo ndiyo imani yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo sikupenda nichangie kwa sababu ya mazingira yalivyo na mfumo na muundo wa Wizara hii bado haunishawishi kwamba maoni yetu yanaweza kuzaa matunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mapori yote ya Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Tabora, Katavi, mikoa yote ambayo wewe unaifahamu ambayo haikuwa na mifugo, mapori yote yamejaa ng'ombe. Madhara yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, madhara yake ni kwamba katika muda mfupi ambao unaweza ukaupima kabisa kwa miaka, Tanzania inakwenda kuwa jangwa; na kwa nini tumefikia hapo? Tumefikia hapo kwa sababu wafugaji wetu kwanza hawana ardhi ya kufugia; lakini pili, hakuna malisho. Kwa hiyo wanahama, wanasaafiri, wanakwenda, wanajaribu kuhangaika; lakini la tatu; ubora wa mifugo yetu ni duni, tunafuga wanyama wengi lakini tija ndogo kwenye ufugaji. Hizo ni baadhi ya sababu ambazo nilitaka nizitaje.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kumaliza tatizo hili ni ndogo kwa sababu tatizo la kuhama wafugaji halihusu Wizara ya Mifugo peke yake na

ndiyo maana nilikuwa nachelea kushauri Bunge lako liishauri Serikali iunde tume au iunde *coordination team* ambayo itahusisha Wizara zisizopungua tano, wafanye pamoja kazi hii ya kuratibu ufugaji nchini.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanahitaji ardhi, wanamuhitaji Waziri wa Ardhi, wanapotaka kuingia kwenye eneo kuna Maliasili, kuna Kilimo, kuna Mazingira, Wizara hizi zote kama hazitaamua kufanya kazi pamoja hatutakuwa na ufugaji bora nchini, tuta-*fall tu*. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakuongezea na Wizara ya Maji.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, na Wizara ya Maji, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niombe na nashindwa kwenda zaidi, hatuwezi kutoka hapa tulipo. Leo nchi hii inakwenda kuwa jangwa. Mimi ni mfugaji na nina ranchi, ninafuga lakini nikienda Songea Vijijini kila pori wapo wafugaji na ukiwaliza wanasema hatuna pa kufugia, hatuna ardhi.

Mheshimiwa Spika, leo tunashauri kwamba wapewe ranchi za Serikali, *well and good*, lakini kama hatuwajengei uwezo wa kuzalisha chakula cha mifugo kwa maana ya *pastures*, uwezo wa kutengeneza visima vya maji, uwezo wa kuzalisha ng'ombe bora, hatutamaliza tatizo hili kwa sababu tutamaliza hizi ranchi za Serikali lakini bado zitakuwa hazitoshi kwa sababu ng'ombe ni wengi sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nikuombe na nitashika shilingi baadaye; Serikali ianzishe *coordination team* ya kuratibu ufugaji nchini. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Chaya utakuwa mchangiaji wa mwisho, baada ya hapo tutamsikia Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nimshukuru sana Waziri, mtani wangu, Mheshimiwa Ndaki pamoja na rafiki yangu, Mheshimiwa Ulega, kwanza kwa wasilisho lao zuri sana la jana la bajeti yao ya Mifugo na Uvuvi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi natoka kwenye maeneo ya wafugaji, nimesomeshwa na ng'ombe, mfugaji. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna zaidi ya ng'ombe 160,000, tuna mbuzi zaidi ya 100,000 na tuna zaidi ya kondoo 40,000. Lakini unapoongelea Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kiasi kikubwa unaongelea wafugaji na wafugaji hawa wengi wapo ndugu zangu na watani zangu Wasukuma, lakini vilevile ndugu zangu Wagogo nao ni wafugaji wengi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo hii nina mambo matatu ambayo ninapenda niishauri Serikali kuitia Waziri wa Mifugo; jambo la kwanza ni kuhusu majosho. Hatuwezi kuongelea ufugaji kama hatutawekeza kwenye masuala ya majosho.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki, nina upungufu wa majosho nane katika Kata za Heka, Makutupora, Mvumi, Majiri, Ipururu, Malampaka, Iseke na Simbagulu. Sera inasemaje; sera inasema kwamba mifugo haitakiwi kusafiri zaidi ya kilometra nane na angalau tumevumilia kilometra 16. Lakini mifugo yetu inasafiri umbali mrefu sana kwenye hizi kata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimuombe mtani wangu, Mheshimiwa Ndaki, josho moja linagarimu takribani shilingi milioni 15 kulijenga kukiwa na ushirikishwaji wa wananchi. Nakuomba basi angalau mwaka huu hebu nipe majosho matatu kwa shilingi milioni 45 na ninaamini kabisa hii mifugo itakusaidia na tutakuza pato la Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu malambo; katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki tuna upungufu wa malambo nane. Wote ni mashahidi, bila kuwa na malambo ya uhakika ya kuhifadhi maji kipindi cha kiangazi, bila kuwa na mabwawa ya uhakika ya kuhifadhi maji kipindi cha

kiangazi, suala la mifugo na suala la mifugo katika ukuzaji wa ajira na pato la Taifa litabaki kuwa ndoto.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuna malambo ambayo ni mabovu, lakini kuna maeneo ambayo yanahitaji kujengewa malambo. Kwa mfano...

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Kiruswa. Mheshimiwa Dkt. Chaya, kuna Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nimpe Taarifa mzungumzaji, kwamba tunapoongelea suala la kuimarisha majosho na malambo au mabwawa ya kunyweshea mifugo, ni vizuri Wizara ikajua kwamba kuna maeneo mengi ambayo ni makame na hakuna chanzo cha maji ukijenga josh, kwa hiyo lazima kila lambo liambatane na josh la kuogeshea mifugo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. DKT. P. S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa hiyo Taarifa na inajazia pale ambapo nilikuwa nimeelezea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naelezea umuhimu wa kuwa na malambo katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Kuna Kata zifuatazo; Mpandagani, Majiri, Mbweko, Mhalala, Mkwese Kintinku, Makanda; hizi kata zina wafugaji wengi sana. Lakini vilevile kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Mbunge, haya ni maeneo ambayo ni makame sana na kipindi cha kiangazi kwa kweli tunakuwa na upungufu mkubwa sana wa maji.

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri, rafiki na mtani wangu, Mheshimiwa Ndaki, hebu njoo unijengee angalau malambo matatu. Kuna malambo ambayo

yalijengwa kipindi cha nyuma yanahitaji kufufuliwa tu, sidhani kama ninaweza kutumia hata shilingi milioni tano kufufua haya malambo. Kwa kweli ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri uwekeze kwenye hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, soko la maziwa; tuna ng'ombe zaidi ya 160,000 katika Wilaya ya Manyoni, lakini hatuna hata *collection point* moja ya kukusanya maziwa, ni aibu. Tuna mbuzi zaidi ya 100,000 Manyoni, tuna kondoo, hatuna *collection* hata moja. Hilo ndilo eneo ambalo tunahitaji kuwekeza. (*Makof*)

Nikuombe Mheshimiwa Waziri, katika vitu vya ubunifu ambavyo unahitaji kuja navyo mwaka huu, moja wapo ni kwenda kuwekeza kwa wafugaji kuhakikisha unasogeza masoko ya kukusanya maziwa. Na ninakuomba ushirikiane na *private sector*, ingia ubia na *private sector* ambaao wamewekeza kwenye suala la viwanda vya maziwa, waje huko kwetu kwa watani zako Wagogo na kuna Wasukuma wengi sana wamehama huko kwao wamehamia Ugogoni, waje wakusanye maziwa kutoka huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala la upungufu wa watumishi. Manyoni tuna watumishi kumi tu wa kada ya mifugo, mahitaji ni zaidi ya watumishi 80; nikuombe Waziri, hebu niletee angalau mtumishi mmoja tu kila kata baadaye utajipanga kwa ajili ya kupeleka mtumishi kila kijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, umeona taarifa hii ya kwamba tuna mifugo mingi. Tuna mifugo mingi, lakini hatuna watumishi kwa hiyo inakuwa ngumu sana kwa hawa watumishi wachache kumi kujigawa kwa ajili ya kutoa huduma, hasa huduma ya kutibu ng'ombe na ushauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Chaya. Wale Wasukuma waliojaa Manyoni mpaka Kongwa ni wakimbizi, siyo wahamiaji. Ahsante sana. (*Kicheko*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwekeze kwenye uchumi wa bahari yaani uvuvi, usafirishaji wa mizigo baharani, magari, makontena na kadhalika. *Cruse tourism*, utalii wa bahari, uuzaji wa mapambo ya bahari, uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, naonga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena leo nianze mchango kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kusimamia Wizara hili. Niwapongeze pia watendaji wote ktika Wizara hii na niwatie moyo kwani changamoto ni sehemu ya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi ndio mkoa uliopokea wafugaji waliohamishwa toka lhefu, walipokelewa katika Wilaya za Liwale na Kilwa. Lakini hapakuwa na maandalizi yoyote ya kupokea mifungo. Mfano katika Wilaya ya Liwale vijiji vilivycopangiwa kupokea mifugo ni vijiji vya Kimambi, Ndapata na Lilombe. Lakini sasa mifugo imesambaa kila kijiji, mbaya zaidi vijiji hivyo havijafanyiwa upimaji wa matumizi bora ya ardhi, hivyo kusababisha migogoro mingi ya ardhi inayosababishwa na kutokuwa na mipaka halisi inayoleweka kisheria.

Jambo lingine hapakuwa na ushirikishwaji wa kutosha kwa jamii hasa katika nyanja za elimu juu ya namna ya kukaa na wafugaji, ukizingatia kwa asili watu wa Kusini si wafugaji. Palihitajika maandalizi mahususi namna ya kupokea mifugo. Hadi leo sisi wakazi wa Kusini hatuoni faida ya kuwa na mifugo kwani hatuna minada, majosho wala malambo.

Hivyo basi naiomba sana Serikali kuleta wataalam wa ufugaji ili kuelimisha wananchi juu ya faida za mifugo, lakini

kama haitoshi tunaomba tupatiwe wataalam wa minada ili kufungua minada ambayo itaweza kukuza kipato cha wafugaji na hata Halmashauri yetu ya Liwale.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuititia Wizara ya Mifugo na Uvubi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Wizara kwa kuandaa vizuri taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvubi kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuimarisha utafiti katika maeneo ya uvubi ili kupata fursa ya kutumia vyema eneo la uvubi wa bahari na maziwa makuu.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali kuimarisha miundombinu ya uvubi; tatu, kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa viwanda vya minofu ya samaki na kuendelea kutafuta masoko ya bidhaa zinazotokana na samaki; nne, Serikali iendelee kutoa huduma bora kwa wadau wa sekta ya uvubi ili kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii; tano, Serikali iendelee kuwekeza katika maziwa makuu kwa kununua meli za uvubi kama Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa na sita, Serikali kuweka mazingira mizuri, sera na kanuni ili kuendeleza ufugaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali kuweka misingi rafiki ya wafugaji ili kuondoa migogoro iliyopo baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie pia kwa maandishi mambo machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza, hali ya mialo kwa upande wa Ziwa Nyasa si nzuri. Hakuna miundombinu ya barabara kiasi kwamba watu hulazimika kubeba mizigo mikubwa kichwani. Nashauri nanyi msaidie kusemea mnapokuwa na Wizara husika kama sehemu ya kuendeleza sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifikishe umeme kwenye mialo. Pia kuwe na mpango maalum wa kutambua na kulinda maeneo ya mazilio ya samaki, yajengwe madogo kila mualo. Pia kuwe na utaratibu wa kutambua ujuzi wa wavuvi (*RPL*) ili kuwatia moyo kama ilivyo kwenye ujenzi, useremala na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya fukwe zina mmomonyoko mkubwa wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo; angalau kila kata kuwe na Afisa Mifugo mtaalam mmoja ili kuwashauri wafugaji pamoja na kutoa huduma za kitabibu hali ya sasa ni kuwa kila mfugaji atumie uzoefu wake.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha matumizi ya Ranchi za Serikali wananchi wakatiwe vipande vya hekta 50 hadi 150, wakodishwe kwa bei ndogo lakini Serikali iendelee kumiliki *asset* yake ya ardhi kwani ni vigumu kupata tena maeneo makubwa kama hayo.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mifugo na Uvuu na wataalamu wa Wizara na wadau wa sekta hizi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo na uvuvi inatoa mchango kidogo sana katika uchumi wa Tanzania pamoja na ukweli usiofichika kwamba tuna idadi kubwa sana ya mifugo na tunalo eneo la Bahari Kuu ya Hindi, Maziwa Makuu Matatu na Mito mingi iliyosambaa nchi nzima ambayo ina utajiri mkubwa wa samaki.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una uhaba mkubwa wa ardhi. Pamoja na hilo, Kilimanjaro kuna fursa nyingi za kufuga aina fulani ya wanyama na samaki kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa malisho, maeneo ya mlimani (Kilimanjaro) yanaweza kutumika vizuri

sana kwa ufugaji wa ndani (zero grazing) wa mfugo ya kimkakati kama vile ng'ombe na mbuzi wa maziwa, nguruwe, sungura, kuku na bata. Hali ya hewa ya mkoa inaruhusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wenye tija kubwa kama ilivyo kwenye nchi za Ulaya. Vilevile eneo la Ukanda wa Chini (Kata za Arusha Chini na Mabogini) lenye wafugaji wa nje, lina uwezekano wa kuzalisha kwa tija ng'ombe, mbuzi na kondoo wa nyama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi za wafugaji wa Jimbo la Moshi Vijijiini, aina za kienyeji za wanyama (ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku) wanaofugwa ni kikwazo kikubwa kwenye maendeleo ya sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, kwa kuwa Mkoani Kilimanjaro kuna maji mengi ya kutosha, kuna uwezekano mkubwa sana wa kuwapatia wananchi kipato kizuri kuititia sekta ya uvuvi kwa kuboresha aina ya samaki waliopo kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu, na kuanzisha ufugaji mpya wa samaki kwa kuchimba mabwawa na kufuga samaki wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hili litawezekana ikiwa wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijiini watapatiwa mafunzo ya kitaalamu ya jinsi ya kufuga na kukuza samaki kwa kutumia teknolojia ya maji kidogo yanayozunguka. Ufugaji wa samaki hauna gharama kubwa ikiwa mfugaji atachimba bwawa.

Mheshimiwa Spika, ufugaji endelevu wa samaki unaweza kutatua changamoto za umaskini kwa kuwaongezea kipato na kuchangia kikamilifu kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Arusha Chini kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu, wavuvi wanaweza kusaidiwa na Maafisa Ugani wa uvuvi mbinu bora za ufugaji wa samaki, ikiwepo matumizi ya vizimba.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa vizimba ulioko Ziwa Victoria na kwenye mabwawa machache Tanzania

unaweza kufanyiwa majaribio kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ufugaji wa samaki na mifugo ya kimkakati katika Jimbo la Moshi Vijijini, ninaishauri Wizara itusaidie yafuatayo; kwanza, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mifugo na uvuvi wafanye utafiti na kuangalia changamoto na fursa zilizopo katika Jimbo la Moshi Vijijini, ili wajue pa kusaidia.

Pili, Wizara ipeleke wataalamu wa mifugo kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo ya kimkakati yenye tija katika Jimbo la Moshi; tatu, kuwe na programu maalum ya kuzalisha mitamba wa maziwa wenye sifa zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na mifugo mingine kama mbuzi wa maziwa, ng'ombe wa nyama, nguruwe na kuku. Wafugaji wengi hawana mbegu bora za ng'ombe wa maziwa, kwa ujumla huwa wanabahatisha.

Mheshimiwa Spika, nne, Wizara ihamasishenkuanzishwa kwa vikundi vya ushirika wa wafugaji mifugo na samaki ambavyo itakuwa rahisi kuwapatia huduma za mitaji na utaalamu.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara itupatiate wataalamu wa kuchimba mabwawa; Wizara ianzishe vituo vya kanda vya kuzalisha vifaranga wa samaki ili wafugaji wavipate kwa urahisi kwani viro tu kwenye Mikoa ya Morogoro, Tabora, Ruvuma, Lindi, Tanga na Geita.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwezeshe wazalishaji vifaranga binafsi ili wasaidie juhudzi za serikali kwenye kukuza hii sekta; Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Moshi, wawezeshe kupandikiza vifaranga bora vya samaki katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, kwani wavuvi waliniambia kwenye kampeni kuwa samaki wamehama, ikiwa na maana kuwa wamebungua.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwe na huduma za uhakika za ugani zikizingatia lishe ya samaki; Serikali iwekeze kwenye

kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji bora wa mifugo ya kimkakati na samaki jimboni kwangu Moshi Vijiji ili wajifunze kwa vitendo (kama ilivyowasilishwa kwenye hotuba ya bajeti 2021/2022).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sasa uchangie kwa dakika kumi halafu Mheshimiwa Waziri mwenyewe dakika ishirini, tuone tunakwendaje baada ya hapo, karibu sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote nianze kwanza kwa kutoa shukrani zangu za dhati sana kwako kwa fursa hii ambayo umenipatia, lakini nitoe pia shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri sana na mikubwa mliyotupatia ya fikra na mawazo chanya kwa ajili ya kuweza kupeleka mbele sekta zetu hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Mashimba Ndaki na Makatibu Wakuu wote wawili pamoja na wataalam wetu na Wakuu wa Taasisi na Idara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizi nitoe pongezi nyngi pia kwa Wabunge kwa namna ambavyo wametupa michango yenyeye kujenga sana, wakiongozwa na wewe mwenyewe ambaye kiasili ni mfugaji, tunakushukuru sana na tuna hakika kwamba michango yenu hii tunakwenda kuifanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa uchache wa muda ninaomba nijielekeze katika kujibu hoja kadhaa za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitaanza na upande wa mifugo na naomba niseme juu ya mipango yetu ya kibajeti kama ambavyo inasomeka katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge walio wengi wameeleza wazi juu ya kutokuridhika kwao kwa namna ambavyo nchi yetu ina mifugo mingi sana, lakini bahati mbaya sana mifugo hii kutokuwa na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa na katika pato la mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeliona jambo hili, jambo hili linatufanya sisi kama wauzaji wa mifugo tusifanikiwe sana kwa maana *suppliers* na *demand* (mahitaji) ni makubwa sana. Kwa hiyo sisi Watanzania wote tunaowajibu wa kuhakikisha tunalichukua kama fursa jambo hili. Na nini ambacho tumejipanga nacho ili sisi Watanzania tuweze kuitumia vyema hii *advantage* ya kuwa ni *suppliers* wa mifugo tena duniani.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo kubwa linalotusumbua kwa kipindi kirefu, mifugo haina *insurance*, ni *perishable good*, jambo hili limetufanya hata *bankers* wasiwe na *appetite* ya kuweza kuingiza pesa katika shughuli za mifugo. Leo hii tunakwenda kwa mfano katika Eid, wakati wa Eid biashara nyngi sana ya mifugo inafanyika, jamii ya Kituruki peke yake inanunua na kuchinja ng'ombe wasiopungua 15,000, jamii moja tu hiyo, lakini utatazama namna biashara ile inavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, ukiitazama biashara ile inavyokwenda yule mnunuzi anataka awe *supplied* wale ng'ombe na akishakuwa *supplied* wale ng'ombe ndiyo sasa baada ya wiki moja hadi mbili aweze kulipa. Jambo hili linawafanya watu wetu wasifanikiwe kwa sababu hawana *cash* na wanapokwenda benki hawawezi kupata hii pesa kwa sababu tu mifugo *as a perishable good*, haikubaliki katika kupewa pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumefika hatma ya jambo hilo, *NIC* wanaenda sasa kutupa uhakika wa kuwa na bima ya mifugo ambayo itawafanya wafugaji wetu wawe na uhakika wa kwenda kukopesha katika miaka minne hii *TADB* Benki yetu ya Kilimo imeweza kupata *application* za mikopo ya shilingi

bilioni 85, mikopo pekee waliyoitoa katika miaka minne hii ni shilingi bilioni 26. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka twende mbele ni lazima tutoke mahala huko, lakini kama haitoshi moja ya mkakati ambao wameusoma Waziri hapa ni kuhakikisha kwamba tunaboresha kosafu zetu, kwa nini kosafu zetu, tunahitaji kuwa na *quality* ya ng'ombe, tunahitaji kuwa na *quantity* ya uhakika, tunahitaji kuwa na *constant supply* ya ng'ombe. Kwa sababu leo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri alishiriki kikao cha Mheshimiwa Rais pale Ikulu, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, watu wapo tayari kununua ng'ombe wetu, lakini leo hii mtu mmoja akiambiwa apeleke *constant supply* ya tani saba kila mwezi hapa tutatafutana, ni kwa sababu ya *constraint* ya kuwa na kosafu na mipangilio yetu haijaka sawasawa. Wizara imejipanga vyema katika risala hii utaona tumeweke pesa zaidi ya milioni 600 kwa ajili ya kufanya *massive artificial insemination*, tunakwenda katika Halmashauri zote zenye mifugo na kuhakikisha kwamba hatuishii kuwapandisha tu, lakini kuna gharama kubwa ya kuwaweka kwenye *heat*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wale ng'ombe jambo linalowasabisha wafugaji wengi washindwe ni kukaweka kwenye *heat*, tunataka tuwapeleke kwenye *heat synchronization* kwa makundi, tutakuja Kongwa, tutakwenda Kiteto, tutakwenda Monduli, tutakwenda Longido, tutakwenda kote kwa wafugaji na kule kwa Dkt. Chaya alipopasema ambapo ni Manyoni. Tukiyafanya haya ya kupata *massive artificial insemination* tutapata kosafu zetu na baada ya muda tutaanza ku-realize juu ya kuwa na ng'ombe walio bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, biashara ya unenepeshaji ng'ombe ni biashara ya uhakika sana, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea kuhamasisha jambo hili sisi wenyewe pia vilevile tuwe ni mfano mzuri sana, ni utajiri wa wazi ambao mimi ningeomba sana Wabunge

wengi tuingie, leo unamnunua ng'ombe ana kilo 150 ambaye huyu ukimchinja *carcass weight* yake ni nusu maana yake kilo 75, ukimpeleka sokoni hakubaliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ng'ombe huyo ukienda katika *project* ya kunenepesha maana yake ni siku 90; kwa hii *breed* yetu ni nusu kilo kwa kila siku, lakini kwa *breed* ya *boran* ni kilo moja kwa kila siku, kwa hivyo huyu ukimpa siku zako 90, huyu ng'ombe anakwenda kuwa na kilo zaidi ya 150 kwa hiyo atakuwa na kilo takribani 240 mpaka kilo 300 ambayo akipata *carcass weight* anapata kilo 150 hadi 200 na ukimpeleka sokoni anauzika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeeleza hili, ili kuwapa Waheshimiwa Wabunge matumaini na namna ambavyo Wizara yetu ilivyojipanga hiyo ni sambamba na kwenda kutatua kero kubwa inayotusumbua kwa muda mrefu ya ghamama za *flight* na Serikali kuititia Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi, umeona tumejipanga vyema eneo hili katika kuhakikisha kwamba...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nasikia kengele hiyo.

**SPIKA:** Bado dakika tano

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi imeandaa kununua ndege mwaka huu ndege ya *cargo* itakayobeba *a straight destination*, kwa hiyo hapa tutachukua nyama zetu zitakwenda Jeddah, zitakwenda Oman, zitakwenda wapi moja kwa moja, kwa hivyo hii ni fursa kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia vilevile tulikuwa na tatizo kubwa la *delay* pale katika bandari yetu ya Dar es Salaam kwa sababu mizigo yetu hii ikienda inakaa kwa muda mrefu.

Wizara ya Ujenzi imejitahidi, naomba tusikate tamaa, tunawaombeni kwa heshima kubwa tupidishieni bajeti yetu, mipango ya Serikali tuliyonayo ni mikubwa ya kuhakikisha sekta hii inakuwa ili kusudi sasa iweze kuchangia vyema katika pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie sasa kwa upande wa uvuvi; uchumi wa *blue*; uchumi wa *blue* umesemwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika risala ya Mheshimiwa Rais ameeleza vizuri sana, tutanunua meli, meli nne Zanzibar, meli nne Bara na katika mwaka huu 2021/2022 tunaanza nalo jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge wengi wa Zanzibar walitaka kujua jambo hili linafanyika Bara tu au linafanyika na Zanzibar tunafanya kwote kuwili hapa bara tunanua meli mbili na kule Zanzibar tunanunua meli mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tena tuna pesa za kutosha za kuhamasisha ufugaji wa samaki katika Ukanda wa Pwani, tunazaidi ya shilingi bilioni 15 zinazokwenda kufanya kazi hii, hii ni pamoja na mwani, hii ni pamoja na kaa unenepeshajji, hii ni pamoja na majongoo bahari, hii ni pamoja na kazi zingine zote zitakazowasaidia vijana sio tu Bara tunakwenda mpaka Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tunawaombeni sana mjiipange katika mkao ule wa vyama vya ushirika na vikundi vya vijana hawa ili tuweze kuitumia vyema hii fursa. Nataka niwahahakishie kwamba jambo hili lipo tayari na tumejipanga nalo vyema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi katika kuhakikisha kwamba tunaongeza *productivity* kule baharini, tunacho kitu tunaita *FADS*yaani *Fish Aggregative Devices*, hii tunakwenda kuweka kule katika bahari, tunazo hizi ni takribani tisini zitaenea katika ukanda wote ule wa Pwani, hii nia yake ni kuwavuta wale samaki.

Mheshimiwa Spika, mmoja katika Waheshimiwa hapa, Mheshimiwa Asya Mwadini alisema kwamba samaki sasa wanakosa maeneo ya kuzaliana. Tumeliona jambo hili na sayansi yake ndiyo tunakwenda kuweka zile *fish aggregative devices* kuanzia Moa mpaka kule Mtambaswala zitaenea hizi, hizi nia yake nikuongeza mazalia ya samaki, hilo jambo tayari tunalo tuitishieni huu mpango ili tuhakikishe kwamba tunakwenda kuyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, jambo lingine zuri tunalokwenda kulifanya ni kuanzisha vichanja nya samaki; ukanda wote huo utapata vichanja nya kukaushia dagaa wetu, hatutaki kuona dagaa wanaoza, hatutaki kuona samaki wanaoza, hii ni rasilimali ya Taifa letu, tunataka tuone watu wanaendelea *ku-export* na nimewasikia Wabunge wengi wanazungumzia juu suala la kuhakikisha kwamba wale *foreigners* wanaokuja kununua, sisi wenyewe ndiyo tuwawezeshe watu wetu wazawa ili waweze kununua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa sababu ya muda naomba nimalizie kwa kuwaeleza na kuwapa matumaini Waheshimiwa Wabunge wote, Serikali yetu imejipanga vyema katika hii *blue economy* na pesa za kununua meli zimeandaliwa, zipo tayari kwa maana mradi huo upo, ujenzi wa bandari hili lipo tayari pia vilevile na tunashirikiana vyema sana, kwa maana ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Bara, lakini na Wizara yetu kwa upande wa kule Tanzania Visiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa umuhimu, katika kujibu changamoto inayowapata wafugaji wengi tunakuja na teknolojia mpya ya malisho inaitwa *JUNCAO*, hii imeonesha mafanikio makubwa duniani. Ndugu zetu wa China tunaendelea nao na majadiliano.

Mheshimiwa Spika, hii itakwenda kujibu hata yale maeneo ya Longido, Monduli, Kiteto yenye kuonesha ile hali ya ukame na kwako Kongwa tunataka tufanye ni sehemu ya kwanza kabisa ya kwenda kupanda hii *JUNCAO* na hii

*JUNCAO* itaenda kuondoa ile *Kongwa wheat* inayoonekana pale kama maua meupe hivi, lakini kumbe ni mtihani ule. (*Makof!*)

Nataka nikuhakikishie ng'ombe akiiona *JUNCAO* anaikimbilia ye ye mwenyewe, tumejipanga kuhakikisha tunashirikiana na wenzetu watafiti na wengineo ili kuleta teknolojia hii itakayokwenda kujibu kilio cha malisho cha wafugaji wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru sana, waarabu wanapenda sana wale mbuzi wadogo wadogo wa *Masai breed*, nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge tunaleta kopa ng'ombe, lipa ng'ombe, kopa mbuzi, lipa mbuzi, nendeni mkahamasishe tuhakikishe kwamba wanataka wale mbuzi wa kilo saba mpaka kilo nane, hawataki mambuzi yaliyokomaa sana. Tafadhalini sana hili ni fursa tunataka tuwatoe Watanzania katika umaskini na tuweze kupandisha pato la Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega, tunakushukuru sana kwa ufanuzi ambao umeutoa na kwa matumaini ambayo tumetupatia Watanzania, umesema neno moja kunenepesha kaa. Kaa ananenepeshwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana tena kwa fursa hii, biashara ya kaa *fattening* inaitwa kaa, *sorry crab fattening* kwa maana ya kwamba yule kaa tunachukua wakiwa wadogo wadogo kutoka kule baharini, kwa sisi watu wa kule Ukanda wa Pwani tunafahamu jambo hili. Kwa hiyo, wale wanaokotwa, tena unaokota, kwa muda mrefu sasa sisi watu watu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvu tumekuwa tukikimbizana na Watanzania wanaotumia fursa ya kuwauzia Wachina wanahitaji sana tena wanahitaji sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tumeona kwa nini tukimbizane nao, tuwatengenezee utaratibu uliokuwa mzuri, watu wafundishwe, waokote wale kaa wakiwa wadogo wadogo, watengeneze majaruba kule pwani, wakishatengeneza yale majaruba, wanakula, tena wale ulaji wao huwawekei chakula chochote ni yale yale maji, *law types* na *high types* maji yakiingia na kukupwa tayari wewe unakuwa umenene pesha na unaiza unapata pesa nydingi sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilishangaa kidogo ingawaje Wagogo, Wamasai hatuwezi kula kaa, maana kwanza kaa kwanza liliowyokaa tu namna ile. (*Makofi/Kicheko*)

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, tafadhalii, karibu sana, karibu uhitimishe hoja yako. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuhitimisha ama kutoa mchango wangu kwa hoja iliyokuwepo jana na leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi sana, sana, kwa kutuongezea mjadala wetu jana, pamoja na kwamba ulisaidiwa kidogo jioni, lakini pia umeendelea leo, lakini nikushukuru sana wewe pia kwa kuongoza mjadala vizuri. (*Makofi*)

Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, kwa uwezo na umahiri wao kuliendesha Bunge letu, lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Majaliwa, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamekuwa wakikaimu nafasi yake wakati hayupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu amekuwa makini sana katika kusimamia shughuli za Serikali, aidha napenda

kuwashukuru sana, sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao mlipata nafasi kuchangia hotuba yetu, lakini hata wale ambao hamkupata nafasi mmechangia, kwa sababu katika hili ni Wabunge 48 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge watatu, wamechangia kwa kuandika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto za Wizara yangu kwa kweli ni nydingi na dalili yake kwamba changamoto ni nydingi ni uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wengi na wewe imekulazimu angalau kupunguza dakika za Mbunge kila mmoja kuchangia. Sasa inaonesha ni kwa namna gani sekta hizi mbili ya mifugo na uvuvi ni sekta muhimu na za msingi sana kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kusema ukweli sekta hizi zinabeba watu wengi, lakini pia wengi wao kipato chao siyo kile cha juu, ni kipato cha chini na cha katiki dogo. Kwa hiyo, ni sekta ambazo kwa kweli zina umuhimu mkubwa na ndio maana zinapojadaliwa kweli zinavuta hisia za watu wengi.

Mheshimiwa Spika, nipende kushukuru sana, ushauri wa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, ushauri wao ulikuwa mzuri sana na niahidi tu kwamba tutauzingatia wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu michango ni mingi sana na mimi nimechanganywa na makaratasi mengi ya wasaidizi wangu hapa yaani wana majibu karibu yote ya Waheshimiwa Wabunge, sasa niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge hoja zenu, maoni yenu na mapendekezo yenu tutayazingatia katika utekelezaji wa bajeti yetu ya mwaka 2021/2022 na tutatoa majibu kwa njia ya maandishi kwa kila hoja ambayo imezungumzwa na kila Mheshimiwa Mbunge, wale walioandika, pamoja na wale waliopata nafasi ya kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi hapa niseme mambo machache tu ambayo nadhani si muhimu sana kuliko mengine, lakini nadhani kwa sababu ya muda wetu yale nitakayoweza kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la ushirikishwaji hafifu wa wadau wakati wa kutunga sheria, kanuni na taratibu, inawezekana kwa sababu kama kawaida sekta hizi ni pana hasa kwenye upande wa uvuvi, ukisema uvuvi ukanda wote wa bahari, zaidi kilometra 1,400 ni ukanda mrefu na watu ni wengi. Ukija Ziwa Victoria ni kubwa watu ni wengi, nenda Ziwa Tanganyika, nenda Ziwa Nyasa ni watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushirikishwaji unaweza usionekane sana ingawa watalaan wetu kwakweli wamekuwa wakijitahidi sana wanapofanya utafiti juu ya jambo linalotaka kufanyiwa mabadiliko au linalotaka kufanyiwa marekebisho, wamekuwa wakijitahidi kupita kwenye maeneo ya wadau ili kupata taarifa zao ili kupata maoni yao.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba Wizara itajitahidi, tutajitahidi kuhakikisha ya kwamba kila mdau anayehusika kwenye masuala ya uvuvi, kila mdau anayehusika kwenye masuala ya mifugo kama tunataka kutunga sheria ama kubadilisha ama kupitia upya lazima tutawashirikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna wakati tulienda Mafia tukakutana na wavuvi walisema hiyo changamoto na kwa sababu changamoto kule ilikuwa ni kubwa zaidi, tuliamuru watafiti na watalaan wetu warudi tena kule na walirudi wakaenda kushirikisha wadau wetu mbalimbali ili kusudi tu tuweze kupata majibu ya changamoto ambazo zinawakabili wavuvi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la wavuvi kuhitaji elimu kutoka Wizarani badala ya kuwachomea zana zao za uvuvi. Hili suala ni la msingi sana na tumeliona baada ya kufanya mikutano na wavuvi, tulifanya mkutano mkubwa na wadau wa uvuvi Dar es Salaam, tukafanya mkutano mkubwa na wadau wa uvuvi Mwanza, tumeliona na hawa wadau wengi wanakuwa hawana habari na mambo mengi yanayotokea ndani ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na hivyo tumeamua ndani ya Wizara kuanzia Katibu Mkuu wangu anayehusika na Uvuvi na watendaji wake, Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Idara, Wakurugenzi wa Taasisi zilizo chini ya Uvuvi wote tumeamua sasa twende kwa hawa wadau, kujaribu kuzungumza nao na kuwaelimisha juu ya sheria tulizopitishaa na kanuni tunazozitunga na kuzipitisha ili wazifahamu. Kwa sababu wadau wengi wanakuwa hawazifahamu, kwa hiyo, tumekubaliana kwamba tutatoa elimu juu ya sheria, kanuni na taratibu zilizoko, lakini pia tutatoa elimu juu ya tozo mbalimbali ambazo zinapitishwa na Bunge lako Tukufu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tutatoa elimu juu ya tafiti mbalimbali tunazozifanya sisi ngazi ya Wizara ili kuhakikisha tu kwamba tuko kwenye ukurasa mmoja na wadau wetu badala ya kwenda tu na kuwachomea nyavyu zao, badala ya kwenda tu na kuwalamu, badala ya kwenda tu na kupora labda mitumbwi yao, hapana; lazima tuwape elimu halafu ndio tuweze kuanza kushughulika nao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tutashirikiana pia na wadau wengine wanaoshiriki kwenye mazao ya uvuvi kama *TASAC* ili ya kwamba tuone ni kwa namna gani elimu inaweza ikafika mapema.

Lakini kulikuwa na suala la wavuvi wa Ziwa Tanganyika waruhusiwe kutumia taa za *solar* zenyе *watts* 200 badala ya *watts* 50 kwa chombo. Serikali tuliruhusu matumizi ya taa kumi zenyе *watts* tano kwa kila moja kwenye uvuvi wa dagaal katika Ziwa Tanganyika na hii inatokana na utafiti uliofanyika pia hatufanyi vitu hivi bila kuwa na utafiti bila kuwa na taarifa kamili zinazohusiana na utaalam wa jambo fulani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utafiti unaonesha kwamba mwanga wa taa hizo kumi kwa *watts* tano unafika kina cha mita 150. Sasa ukisikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge hapa, wanasema ni chini ya hapo, lakini utafiti wetu unaonesha hivyo. Ongezeko la mwanga halina tija sana

kutokana na sababu kuwa zaidi ya kina cha mita 150 hakuna samaki kwa kuwa hakuna hewa ya *oxygen* kule chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sijaelewa vizuri labda kwa sababu tutahitaji kuzungumza na kukutana na wadau, tutaelewa vizuri wanachokimaanisha labda kina maana gani.

Kwa hiyo, tutaendelea kuwatemeblea wavuvi wetu walioko Ziwa Tanganyika, tuelimishane nao juu ya habari hii ya taa na ingawa pia wengine wana maoni kwamba taa za *solar* pia zisitumike, yaani kuna wakati maoni mbalimbali yanakuja na yanafika mahali yanatuletea shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala la lingine lilikuwa linahusu kuruhusu uvuvi wa kambamiti uanze Disemba hadi Mei; Mheshimiwa Mpembenwe nadhani alizungumza suala hili.

Mheshimiwa Spika, uvuvi wa kambamiti kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo unaruhusiwa kufanyika kuanzia mwezi Machi hadi Septemba kila mwaka kwa Kanda ya Kaskazini inayohusisha Wilaya za Bagamoyo, Pangani, Chalinze na kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti kila mwaka kwa Kanda ya Kusini inayohusisha Wilaya za Mkuranga, Kibiti pamoja na Kilwa. Aidha, kipindi kilichobaki kimeachwa ili kambamiti waweze kuzaliana na kukua.

Mheshimiwa Spika, maamuzi haya yamefanyika baada pia ya taarifa za utafiti wa kisayansi na kuzingatia uendelevu wa rasilimali za kambamiti. Hayo ndio tuliyoyazingatia katika kuangalia ni kipindi kipi ukanda ule wa Kaskazini wavue na ni kipindi kipi ukanda huu wa Kusini wavue. Kwa hiyo, hayo ndio tuliyoyazingatia, lakini ni baada ya kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kufanya utafiti na kuona kama maoni ya Waheshimiwa Wabunge ndio *valid* kwa sasa ili tuweze kuamua pia. Sisi hatuko *stagnant* sana, hatuko *rigid*sana kiasi kwamba tunashirikiana, tunasikiliza kile

kilio cha wavuvi wetu, cha wadau wetu kuhakikisha kwamba tu tunakwenda pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye mifugo; muda wetu ni mchache, lakini nizungumzie kuhusiana na uhaba wa miundombinu ikiwemo majosho, mabwawa, visima na minara. Niseme tu kwamba kwa kweli uhitaji ni mkubwa na kwa namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmechangia, mmeona pia namna fungu letu livilyo. Sasa kwa sababu uhitaji ni mkubwa kwa mwaka huu wa fedha hatutaweza kukamilisha kila jambo walilohitaji Waheshimiwa Wabunge tulifanye kuhusiana na miundombinu ya mifugo. Tutafanya kwa sehemu lakini sehemu zingine tutafanya kwa miaka inayokuja.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumeweza kujenga majosho 12 tu, mengine 59 yanaendelea kujengwa, tuna majosho 199 yamekarabatiwa na majosho 111 yanaendelea kukarabatiwa. Kwenye mpango wetu wa mwaka huu tumesema tutajenga majosho 129; kwa hiyo, tutaangalia tutaanza na mahali ambapo majosho hayapo kabisa. Tutawapa kipaumbele mahali ambapo ng'ombe wako wengi, lakini pia majosho hakuna. Kwa hiyo, tutaangalia hilo lakini miaka inayofuata tutaendelea kwenda kwenye maeneo mengine pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusiana na mabwawa; mabwawa pia tunayo kidogo kwa mwaka huu wa fedha ambao ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtupitishie tuna mabwawa matano. Sasa tutayagawaje kwa Wabunge na majimbo 260 na kitu, hiyo pia ni changamoto yetu nyingine. Lakini nawaombeni tu kwamba tukubaliane maeneo ambayo yatapata mabwawa basi ukipata moja, ninaomba tu tushirikiane, siku nyingine tutapata nyongeza kwa kadri ambavyo tutakuwa tumepata fedha.

Ndugu yangu Mheshimiwa Nicodemus Maganga alisema tutachukua shilingi asipopata, lakini nimhakikishie tu kwamba mpango wetu ni kila mmoja aweze kupata kulingana na fedha tulizonazo. Lakini niombe tu kwamba

ikiwa hautafanikiwa kupata kwa mwaka huu, kuna mwaka utafanikiwa kupata. Kabla ya 2025 unayoihofia, tutakuwa tumekupa malambo au mabwawa ambayo tutatuliza wapiga kura wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusiana na upatikanaji wa malisho, jambo hili pia limechangiwa na Wabunge wengi. Sasa Wizara tunaendelea kuboresha malisho. Mheshimiwa Naibu Waziri wangu amelizungumza kidogo, lakini mpango wetu ni kwamba tunataka mashamba ya Serikali na mashamba ya Taasisi za Serikali, tuyape mbegu kama ambavyo Naibu Waziri amezungumza tuwape mbegu waweze kupanda. Taasisi zetu za utafiti pia tutazipa mbegu waweze kupanda na wakishapanda tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kuwaleta wafugaji wetu waweze kujifunza kwenye maeneo haya ambayo tumesema tutapanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesema tutaenda Halmashauri 20 ili ziwe na mashamba darasa ya malisho, sasa Halmashauri hizi 20 bado ni pungufu, haziwezi kuenea kwenye maeneo ambayo wafugaji wetu wametawanyika. Lakini ninaomba sana, sana maeneo ambayo tutafika na malisho na mbegu hizi za malisho, basi wafugaji walioko kwenye maeneo hayo wajifunze namna ya kustawisha malisho ili tuweze kuwa na malisho ya kutosha. Lakini pia tunataka tuhamasishe wadau wetu Serikali za Mitaa na wao maeneo wanayotenga wajaribu pia kupanda mbegu ambazo sisi tutakuwa nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kuna Halmashauri ambazo zimetenga maeneo ya wafugaji vizuri, lakini kuna Halmashauri zimetenga maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima, lakini kwa upendeleo sana ambao sio mzuri na upendeleo huu umeleta mgongano kwenye baadhi ya Halmashauri. Utakuta eneo la Halmashauri zima, limepewa wafugaji asilimia 70, wakulima asilimia 30 wakati idadi ya wafugaji na wakulima iko sawa, sasa utakuta lazima maeneo kama haya kutakuwa tu na ugomvi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawasihi sana Halmashauri zetu kwamba tunapopanga maeneo ya malisho tuzingatie pia uwiano wa watu walioko kwenye Wilaya yetu, tuzingatie pia uwiano wa shughuli za kimaendeleo zinazofanyika kwenye Halmashauri zetu hizo, vinginevyo tutaendeleza ule ugomvi. Lakini nafurahi kusema kwamba kuna Wilaya ambazo zimeamua zitaanza kutenga maeneo na kufanya kama ranchi.

Mheshimiwa Spika, nawaunga mkono Halmashauri za namna hiyo na ninawaombeni Halmashauri za namna hii badala ya kuomba fedha za miradi ya kimkakati za kujenga stendi, za kujenga sijui vitu gani basi pelekeni kwenye ranchi hizi mlizotenga. Hizi ranchi zinaweza zikawapa fedha nyingi kuliko mnavyoweza kutarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu niseme sisi ranchi tunakodisha kwa hekari moja shilingi 3,500; sasa ukikodisha wafugaji wengi kwenye ranchi mtakazokuwa mmetenga, wafugaji wengi ukawa na hekari za kutosha ni chanzo kimojawapo cha mapato ya Halmashauri zenu. Badala ya kung'ang'ania na miradi ya *stand*, miradi ya masoko sijui na miradi ya namna gani, utakuwa umetatua tatizo la kipato cha Halmashauri yako, lakini utakuwa umeondoa mgogoro kati ya wakulima na wafugaji au wafugaji pamoja na wawekezaji wengine wanaotaka kutumia ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuongeza upatikanaji wa huduma za ugani na vitendea kazi, hili suala pia limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ambao ndio wanahuksika hasa kwenye ajira za Maafisa Ugani wetu hasa wale wote wa uvuvi pamoja na wale wa mifugo. Lakini tutaimarisha mifumo yetu ya huduma za ugani kiganjani ikiwemo *m-kilimo* ambao ni mfumo unaosaidia kufikisha elimu ya ufugaji bora wa samaki, ufugaji bora wa mifugo kwa wadau wetu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo. Lakini tumesema kwenye taarifa yetu tutawezesha

safari hii kununua pikipiki 300, ambazo tutazigawa kwenye maeneo ambayo tunaona ni *critical* kwenye baadhi ya halmashauri. Mahali ambapo wafugaji au shughuli za ufgajji ziko nyingi, tutagawa pikipiki ili kuweza kuwasaidia hawa watu wetu pia waweze kusafiri na kukutana na wadau wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda niende sasa nizungumze kidogo kuhusiana na suala la *NARCO*, wewe umetoa mchango wako juu ya jambo hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya muda umeisha, lakini basi nakupa *bonus* dakika tano umalizie.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, basi nakushukuru sana ahsante sana, nikushukuru sana. Mengine sasa tutatoa majibu kama nilivyosema kwa maandishi, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANO YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhitimisha hoja yako vizuri na hoja imeungwa mkono tunakushukuru sana. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi sekta ya Mifugo ukurasa wa 495 kitabu cha pili, matumizi ya kawaida.

### **KITABU CHA PILI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **FUNGU 99 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (MIFUGO)**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 2,819,246,570

**MWENYEKITI:** Hapa ndio mshahara wa Mheshimiwa Waziri, tunaanza na wale wenye hoja za kisera wenye kuhitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Charles Mwijage uwe wa kwanza.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru; katika mchango wangu nikiongea mbele ya Bunge lako nilijaribu kuishauri na kuishauri Serikali katika ajenda ya kuleta tija katika maeneo yanayomilikiwa na taasisi inaitwa *NARCO*. Nikaenda mbele ili tuondoe migogoro ya ardhi, lakini tupate tija kubwa nikashawishi kwamba *NARCO* ingepunguza eneo lake, ibaki na eneo kidogo na haya maeneo mengine iyaachie Wizara zingine zigawie wawekezaji lakini iwasimamie wafanye vizuri sana yenye ijiondoe kwenye shughuli za kuchunga ambalo ukiangalia kiutendaji hazina tija na iiachie sekta binafsi ya Kitanzania sio ya Tanzania ya Kitanzania kwa sababu shughuli hiyo wanaimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka kusikia kauli na *commitment* ya Serikali na niseme awali na mwanzo kwamba kama sitoridhika basi nitashika shilingi kusudi suala hili tulifanyie maamuzi tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi tafadhalii.

**WAZIRI WA MIFUGO NA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niombe tu kwamba eneo hili la *NARCO* kwanza tumepokea ushauri waliota Bunge lako Tukufu pamoja na wewe, lakini pia suala analozungumza Mheshimiwa Mwijage ni suala la msingi sana, la kuongeza tija kwa *NARCO* lakini pia kwa ufügaji kwa ujumla wake na mimi nakubaliana kabisa.

Sasa sisi tumeamua kwamba tufanye tathmini ya kina ya jambo hili linalohusu *NARCO*, namna ya utendaji kazi wake na makusudi yake ilipokuwa ikianzishwa halafu tuone ni kwa namna gani tunaweza kuleta mageuzi juu ya namna ya uendeshaji wa mashamba haya ya *NARCO* ili tuweze kuleta tija kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu ni kweli tumeona namna inavyoenda haijafikia kiwango kile ambacho wananchi na Taifa hili lilikuwa linategemea. Kwa hiyo, tunaomba tupate muda ili tuweze kujipanga vizuri tufanye tathmini ya kina, tupitie upya na kisha tuje na mkakati wa namna gani tutakuwa na tija kwenye mashamba haya makubwa. Kwa sababu tumejitahidi kuweka mkakati wa haraka haraka wa kukodisha haya mashamba ya *NARCO*, kama asilimia 75 hivi yamekodishwa *NARCO* yenyewe imebaki na asilimia kama 25 ambako inaweka mifugo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana bado haitoshi na tumekodisha kwa watu wote wa aina tatu, wadogo, wa katni na wakubwa, lakini bado tunaona mkakati huo haujalenga kabisa haujaleta tija. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tupate nafasi Bunge lako litupe nafasi, tufanye tathmini halafu tutakuja na mkakati wa namna gani tunaongeza tija kwenye mashamba ya *NARCO*, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage, umesimama.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri amesema

aliyotekeleza hayakufanyika na kwenye taarifa yake ameandika, ina maana ameshafanya tathmini, yaani amejaribu hiki na kile hakuona tathmini, migogoro anajua, mimi nimefanya kazi na yeYe mikutano zaidi ya minne, kwa hiyo tathmini ameshaiona kwamba hapa hapaendi na hatuna muda wa kusubiri 2025 ni kesho. Kwa hiyo, ili tuanze leo, ninachokiomba ni kuona tunaamua sasa na kwa sababu tumezunguka sana naomba nisimame hapa niwaombe Waheshimiwa Wabunge nitoe hoja ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, nawaombeni tusifike huko Mheshimiwa Mwijage. Nakuomba sana, wewe *senator*.

Kwa kweli Mheshimiwa Waziri amesikia, Naibu Waziri, Katibu Mkuu yupo, Baraza la Mawaziri lipo hapa, jambo hili wala si la leo tu, ni lina miaka na limezungumzwa sana na kama ni *studies* Serikalini zimeshafanyika nyngi za kutosha na majibu yako kwenye ukuta wazi kabisa. *NARCO* hata kodi ya Mheshimiwa Lukuvi sijui kama wanalipa. Sidhani, hii kodi ya ardhi. Hata uwezo wa kulipa kodi ardhi sidhani kama wanayo. (*Kicheko*)

Na sio jana au juzi, *over the years*, yaani kuna kila sababu na ushauri tuemtoa. Hoja aliyotoa Mheshimiwa Waziri ni nzuri tu Mheshimiwa Mwijage, tuwape muda wajiridhishe, wafanye kazi ndani na *reforms* hizi zina *processes* ambazo baadhi yake lazima ziende Baraza la Mawaziri na kadhalika, kwa hiyo, *it takes time*. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana.

Lakini tukubaliane tu kwamba tunapokutana hapa mwakani Mheshimiwa Waziri kwa kweli wenzetu msije na lugha hizi tena kwa sababu hazisaidii. Lazima twende mbele, lazima twende mbele isaidie kwenda mbele. Hata sisi

tuliowapa mawazo yetu myachukue. Hata mhangaika namna gani Mheshimiwa Ulega, hatuvuki, huo ndiyo ukweli. (*Makofii*)

Unajua ni vizuri duniani ukiujua ukweli, kwa sababu wanasema ukweli utakuweka huru. Lakini tukiendelea kujidanganya na mambo haya ya *state* kuweza kuchunga ng'ombe, haiwezekani. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mipango yote mizuri ambayo imeelezwa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri hapa itategemea wafugaji wadogo na wakubwa kuwa na ardhi ambayo wanaweza kufuga, wakaendeleza malisho na maji na kwa vile upatikanaji wa ardhi ya aina hiyo unategemea pia Wizara zingine ikiwemo Wizara ya Ardhi, TAMISEMI, Wizara ya Maji na Mifugo pamoja na Killmo; ni lini sasa Serikali iko tayari kuunda Tume au Kamati ya pamoja kwa maana ya *coordination team* ambayo itaunganisha Wizara zote ili kuhakikisha mfugaji mdogo nchini anapata ardhi, anaimiliki kihalali, ana uwezo wa kuendeleza malisho, maji na kadhalika ili mipango yote aliyoipanga pale iweze kutimia ikiwemo kupeleka nyama nchi za nje kwa sababu huwezi kufanya hivyo kama huna wafugaji wanaofuga kwa kufuata utaratibu. Huwezi kukopa fedha benki kama huna mfugaji mwenye shamba ambaye ameratibiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata *commitment* ya Serikali nitashika shilingi Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Nadhani swali hilo ni vigumu sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kulijibu kwa sababu ni la uratibu, unachotaka ni uratibu. Labda nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Uratibu - Mheshimiwa Jenista. Namna gani ya kuratibu hizi Wizara zote tufikie huko ambako kunaomba na Mheshimiwa Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo utaratibu wa uendeshaji wa shughuli

za Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa na mimi niko hapa kwa niaba yake kuhakikisha yale yote ambayo yanahusu Serikali kwa umoja wetu na hasa yale ambayo yanahitaji uratibu wa kisekta wa Serikali. Tuko hapa kwa ajili ya kuyasikiliza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na hatimaye kuyachukua na kuyafanya kazi.

Kwa hiyo, kama ulivyosema kuhusu hoja ya Mheshimiwa Joseph Mhagama na maelekezo ya Kiti chako, tunaomba hili waliache ndani ya Serikali. Tutaona namna ya kufanya na kuzitazama sekta husika na hasa mtengo wa bajeti, vipaumbele na programu ambazo zinafanyiwa kazi kwenye sekta mbalimbali, basi ili tuweze kujipanga na kuangalia utekelezaji bora wa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati zetu na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa ni wadau muhimu wakikagua utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia kwenye Wizara, tutaendelea kushauriana na kupima mwelekeo na namna bora ya kuliweka jambo hilo likakaa sawasawa. Nakushukuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama. Ahsante sana kwa ukarimu wako.

Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Lengo la Serikali kuweka hifadhi ndani ya ziwa ni jambo jema lakini kama nilivyochangia kwenye mchango wangu kumekuwa na changamoto katika maeneo hayo ya hifadhi kwa kuwa hakuna alama matokeo yake inatumika kama kichaka cha kuwapa adhabu wavuvi wanapofika kwenye maeneo hayo na kwenye majibu ya Waziri sijasikia akizungumza lolote.

Mimi sitaki kuondoka na mshahara wa Waziri, nataka ufanuzi ili wakafanye kazi; ni namna gani wataweza

kuondoa changamoto hii kwa kuweka alama sehemu za hifadhi?

**MWENYEKITI:** Hifadhi za majini? *Okay*, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Aida na naomba nijibu tu kwa kumuomba jambo hili ambalo anahitaji ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye baadhi ya maeneo yetu hasa upande wa Magharibi, Kigoma, Katavi na Rukwa kwenye mbuga zetu kwa maana ya hifadhi zetu zile za maliasili zimeingiliana. Baadhi ya maeneo yetu na Ziwa Tanganyika na baadhi ya maeneo zimeingiliana na Ziwa Rukwa na mito mikubwa ambayo wenyehi wamekuwa wakitumia fursa ile miaka na miaka kwa ajili ya kuweza kwenda kupata kitoweo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na hata biashara pia vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa la muda mrefu, lakini sisi kama vile ambavyo amejibu Mheshimiwa Waziri wa Uratibu, wenyewe tunajiratibu kwa sababu maeneo haya yako ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, wako mle *games* na walinzi wengine ambao wanaangalia.

Kwa hiyo, sasa tumeamua tuanze mazungumzo na wenzetu wa Maliasili ili kusudi pawepo na utaratibu *proper* wa kuwaruhusu wavuvi wetu wakati fulani waingie. Kwa sababu bila kufanya hivyo ile rasilimali inakuwa imekosa matumizi na hivyo haimsaidii mtu ye yote. Haimsaidii yule mvuvi kwa maana ya mwananchi hata sisi Serikali vilevile na Taifa kwa ujumla wake, haitusaidii. Kwa hiyo, hili tunaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sio huko peke yake, tunalo pia katika Ziwa Victoria tunalo jambo hilo, ukienda pale kama Chato na Rubondo maana yake, lakini vilevile ukienda katika visiwa vyta Saanane na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Aida Khenani na Waheshimiwa Wabunge wote wenye *interest* na jambo la namna hii wawe na subira sisi Serikalini tunaendelea na mchakato wa kukaa pamoja kwa haraka sana tupate majibu ili rasilimali hizi ziweze kuwasaidia wananchi wetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida ameridhika nashukuru. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hapa alizungumzia habari ya kambamiti; mimi ninajua kambakochi, ni *specie* mbili tofauti?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kiingereza nitawasaidia zaidi Waheshimiwa Wabunge kuelewa; kambamiti ni *prawns* na kambakochi ni *lobster*. Yes! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Okay! (*Kicheko*)

Ahsante sana. Haya mambo yanataka mazoea kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Esther Matiko, nimekuona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; na mimi sitarajji kuondoka na mshahara wa kaka zangu pale lakini nataka tu *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara kama nilivyosema wakati nachangia, ukitoa Madini, Maliasili na Utalii basi Wizara ya Kilimo kwa maana ya Kilimo, Mifugo na Uvubi uu Mifugo na Uvubi ni Wizara ambayo tukiwekeza itaenda kuchangia kwenye pato la Taifa. Lakini Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha bajeti hapa lakini fedha za maendeleo haziendi kama ambavyo tumeidhinisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nifanye rejea kidogo; mwaka 2016/2017 kama nilivyosema awali bilioni nne zikaenda milioni 130 tu, sawa na asilimia 2.3; mwaka 2017/2018 shilingi bilioni nne, haikutolewa hata *single cent* pamoja

na kwamba waliweza kukusanya maduhuli lakini haikwenda hata *single cent* kwenye maendeleo. 2018/2019 ilikuwa upande wa mifugo Fungu 99 bilioni tano ikaenda bilioni 1.9...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, maana hoja yako ni kubwa ili Waziri wa Fedha akusikilize vizuri hebu ianze tena.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *commitment* ya Serikali kwa kuzingatia kwamba Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara ambayo kwa kweli tukiwekeza kwenye miradi ya maendeleo kama vile kufanya tafiti kuweza kugundua kwenye maziwa ni maeneo gani ukienda utakuwa na uvuvi wenye tija bahari kuu lakini pia mifugo yetu tukiweza kuwekeza tukafanya tafiti ya kina tutajua ni vipi tutaweza tukawa na mifugo ambayo itatoa *products* za tija.

Sasa hivi tunaambiwa ng'ombe wa Tanzania mmoja ni kilo 100 -150 wakati huko nje kilo 500 - 600. Lakini tunaambiwa pia maziwa ni lita tatu kwa ng'ombe wa Tanzania wakati huko nje tunaambiwa ni lita 20, 30 na kuendelea. Sasa hayo yote yanahitaji fedha za maendeleo ambazo tunazitenga ziende. Bunge lako Tukufu limekuwa likitenga fedha za maendeleo lakinihaziendi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 tulitenga bilioni nne zikaenda milioni 130 tu; mwaka 2017/2018 bilioni nne haikwenda hata *single cent*; mwaka 2018/2019 Bunge lako Tukufu liilitenga Fungu 99 bilioni tano ikatoka bilioni 1.9; Uvuvi tulitenga bilioni 7.13 ikaenda bilioni nne tu; mwaka 2020/2021 tulitenga bilioni 23 zimeenda bilioni 11 tu licha ya kwamba Wizara hii maduhuli kutoka Fungu 99 na 64 imefika mpaka Mei, bilioni 51. Hiyo ingetosha kuona kwamba tumewekeza kidogo lakini bado tunakusanya maduhuli mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiwekeza kwa kina, hizi fedha zikaenda kuwafikia hata kuweza ku-*train* ma-veterinary, doctors wengi, tukaweza ku-*train* technicians wengi, tukaweza kuwa na maafisa ugani wengi wa mambo

ya mifugo na uvuvi kuweza kuwafikia hata hawa wafugaji wadogo wadogo wa kuku, tungeweza kufika mbali. Ni Wizara ambayo ingechangia pato kubwa sana kwa Taifa.

Sasa ningetaka *commitment* ya Serikali, hizi bilioni 96 za maendeleo ambazo tuemzitenga mwaka huu wa fedha 2021/2022 zitaenda zote ili mwakani tuweze kuongeza na ukizingatia *Declaration* ya Malabo tutenge *ten percent* ya bajeti kuu ambayo tulitakiwa tutenge *more than three trillion*. Lakini hata hizi bilioni 96 zitaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivyo, nataka tu *commitment* ya Serikali ili tuweze kutoa ajira nyngi na kukuza uchumi wa Taifa letu. Tutoke kwenye uchumi wa chini wa kati, twende kwenye uchumi wa kati na baadaye uchumi wa juu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kweli kwa *trend* hii nafikiri ufanuzi kidogo kutoka kwako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru maelezo yaliyotolewa na Mbunge na mara nyngi takwimu ni *fact*. Lakini kitu kimoja ambacho hata kwenye mjadala Wabunge wengi wamechangia wakielekeza hoja kwa Mheshimiwa Waziri wa sekta kwamba ameanzia wapi kupandisha kiwango kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa na Waziri pamoja na timu yake; tumekaa na Waziri wa Maliasili na timu yake na Waziri wa Mifugo na timu yake tukiwa Wizara ya Fedha pale na timu yetu; tukapanga namna ya kuanza utaratibu mpya wa kutoka kwenye huu ufugaji wa asili ambao kwa kweli wafugaji wanakuwa *scattered* hata ukitaka kusema uwekeze, uwekezaji wake pia unakuwa ni mgumu kwa sababu kila mmoja yuko na njia yake.

Kwa hiyo, tunavyoongea hivi tumeongea na hizi sekta tatu; yaani, Wizara ya Mifugo, Maliasili tukiwa tumejumuisha na Wizara zingine kwenye ile kazi kubwa ambayo ilikuwa

imefanyika tuone namna ambavyo tunaweza tukaenda kwenye *modernization* ya Sekta hii. Kwa maana hiyo sasa *modernization* itahitaji uwekezaji ndiyo maana tumeona tuweke kiwango ambacho ni kikubwa. Tuko *determined* kwenye hilo na hatua tu ambazo zimesalia ambazo ningombwa nisizitaje kwa sasahivi kwa sababu *tax measures* hazijapata *authority*, hazijapita kwenye mamlaka, lakini tunapanga twende kwenye *modernization* na tumeshatumia ripoti ya timu hii kubwa iliyoundwa ya Baraza la Mawaziri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually* Baraza la Mawaziri lilishabariki upande wa mpango wa Wizara ya Mifugo ikihusisha na Wizara zingine. Kwa hiyo, itakuwa inahitaji *financing aspect* kwenda kwenye *modernization* ya aina hiyo. Uwekezaji kwa namna iliyopo ya sasa ambako kila mfugaji yuko na mpango wake na njia yake, uko *scattered* mno. Ni ngumu sana kum-task Waziri wa Mifugo aseme anaweza akawekeza. Kwa hiyo, tunawaza twende kwenye njia ambayo itakuwa na namna ambayo tutaitaja wakati tunakuja na *tax measures* na hotuba kubwa tunachokipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishaenda kwenye utaratibu huo sisi kama Wizara ya Fedha tunaamini tunatengeneza na utaratibu ambao utawezesha Wizara hii ipate fedha ambalo ndilo swalii la msingi la Mheshimiwa Mbunge. Tunaamini tutafanya hivyo. Tupewe tu muda huu tutakavyokuja kwenye hotuba kubwa. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amejitahidi kuzunguka sana. Mimi ombi langu lilikuwa dogo tu, nina imani mpaka Wizara imeleta hizi *96 billion* za maendeleo imeshafanya kila kitu. *To start with, commitment* ya hapa ninayoitaka kwa hizi *96 billion* zitaenda *with this financial year* ambayo tunaianza *July to June 2022* hizi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo zingine nazibariki. Hizo hatua zote zingine ni kuanzia huo mwaka. Hizi *96 billion* zitaenda ili tusiende kwenye *two percent, three percent* sio kusema mkifika hapo ndiyo mtajua. *Just go straight kwamba zitaenda hizi 96 billion or not? (Makof)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vipengele viwili; moja, hivi vitabu hata wewe na Bunge lako mnatumia muda mwingi kuvipitisha, haya sio maonesho, yaani tuko *determined* kama Serikali kwamba tunaenda kutekeleza hali. Lakini la pili, utoaji wa fedha unategemea ku-*finance program*. Hatufanyi kazi ya kugawana, tunafanya kazi ya kutekeleza *programs*. Waziri ametoa *programs* na zitakuja *certificate*, hakuna *certificate* sisi tutaziacha hatuzillipi. (*Makof*)

Kwa hiyo, mimi niweke *commitment* hiyo kwamba tunaenda kufanya jambo hili na tumpitishie Mheshimiwa Waziri aanze kazi yake na mambo haya yatawafurahisha wafugaji wote wa nchi nzima. Sisi Wanyiramba kwa nyama, ndiyo habari ya mjini kwetu. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Hili sisi tunai-*task* Kamati ya Bajeti. Kamati ya Bajeti mnayo nafasi kubwa sana ya kufuatilia bajeti, utekelezaji wake na ndiyo maana tukimaliza hapa tunatunga na sheria, tuna *appropriate* na kadhalika. Ni wajibu wetu kufuatilia bajeti inavyotekelizwa, kwa sababu *data* zinavyoonesha kwa kweli inatisha. Kama Bunge hili lilikuwa linapitisha bilioni nne halafu hata shilingi moja haiendi kwenye Wizara hii, inapitisha bilioni nne inaenda milioni 130 yaani hata bilioni moja haifiki. Kwa hiyo, *data* hizi zinatuonesha kuna *tendency* fulani ya kutokumbuka hii Wizara ya kitoweo. (*Makof/Kicheko*)

Na hata mgao wa fedha hapa leo Malaigwanan wamenyamaza tu lakini wangesimama wafungue miyo yao ng'ombe anapewa milioni 40 halafu samaki anapata milioni

120, hawaelewi kabisa huu ni mgawanyo gani huu. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini ni kwa sababu ya mazingira maalum. Kwa hiyo hiki kidogo ambacho wanapatiwa kwa sababu kwa kweli tunajua wanapata hela kidogo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, basi angalau hicho kidogo msisitizo wetu angalau kitoke ili mambo yazidikuwa mazuri zaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti mtusaidie katika *monitoring* yenu muwe mnafanya *special monitoring* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Mifugo na Uvuvi na Kilimo wanakumbukwa kidogo kwa sababu hizi ndio Wizara za wananchi na zingine pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Mkundi Michael.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati natoa mchango wangu niligusia suala la wavuvi wetu wadogo wadogo kuchomewa zana zao za uvuvi hasa nyavu na Mheshimiwa Waziri katoa maelezo, lakini wavuvi wetu hawa wanapoenda kununua nyavu wana imani kwamba mamlaka zinazohusika za udhibiti wameridhia nyavu zile na inapotokea sasa kuchomewa nyavu zao na kutiwa umaskini ni kuwaonea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata kauli ya Serikali ni hatua zipi zinazchukuliwa ili kudhibiti jambo hili, ili kama kuna tatizo la *size* za nyavu basi Serikali iwe inadhibiti wazalishaji na waingizaji wa zana zile badala ya kwenda kuwaadhibu wavuvi wadogo, jambo ambalo linawatia umaskini, kitu ambacho sio dhamira ya Serikali. Nini kauli ya Serikali katika kushughulikia jambo hili? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. suala la udhibiti wa nyavu au zana za uvuvi pia ni suala la Wizara yang una wataalamu

wa Wizara, sisi ndio tunaotoa kibali cha nyavu ziingizwe na wafanyabiashara au wauzaji wa zile nyavu kwa wavuvi.

Sasa ni kweli kwamba kwenye mazoezi ya *operations* pamoja na doria zilizofanyika wavuvi wengi walikutwa na nyavu ambazo hazihitajiki kulingana na sheria na taratibu zetu na wanaopata adhabu wengi ni wavuvi wala sio hawa wanaoagiza na kuzileta hapa ndani na kuwauzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulipofika kwenye Wizara kweli tulilliona hilo kwamba hatuwezi kuendelea na utaratibu wa kuzifuata nyavu kule baharini au ziwani mvuvi anavua wakati sisi ndio tunatoa kibali cha watu hawa kuingiza. Kwa hiyo, tumeweka utaratibu ngazi ya Wizara, tutakuwa tunafanya tathmini ya wale wote tuliovapa kibali cha kuleta nyavu, kabla hawajazipeleka kuziuza kwenye maduka yao Mkurugenzi wetu wa Uvuvu ambaye ndiye kisheria anatoa hivyo vibali atapita na kuangalia kama nyavu zilizoletwa ziko kulingana na viwango kwa kadri taratibu na sheria zetu zinavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo habari ya kwenda kuadhibu wavuvi itapungua sana, isipokuwa labda mahali ambapo kwa sababu nyavu hizi nyingine tunesikia zinatokea Malawi kwa njia za panya, zinaingia halafu zinakuwa kama zinaenda Zambia hivi, halafu zinarudia pale Tunduma. Lakini utaratibu tuliouweka sasa hivi ndio huo kwamba, waagizaji wote wa nyavu na watengenezaji, maana tuna kiwanda pia kinatengeneza nyavu kule Mwanza, wote tutakuwa tunawakagua kabla nyavu hizo hazijaenda kwenye soko ili kuhakikisha tu kwamba, tunapunguza hizi nyavu haramu ambazo zimetapakaa kwa wavuvi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi umeridhika?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika, labda niombe tu kwa wale ambao wamechomewa nyavu kwa mazingira ya kuonewa basi,

Serikali ione namna ya ku-compensate ili angalao kufidia hayo, nashukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya, acha wakaangalie hilo kwa bajeti hii ndogo waliyonayo.

Mheshimiwa Mpembenwe nikupe nafasi, tumia fursa hii.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo kidogo linanitatiza sana kuhusiana na majibu ya Serikali jinsi tulivyokuwa tumeweza kuyatoa kuhusiana na suala zima la uvuaji wa kambakoche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashughulika na wananchi wengi sana wako nyuma yetu ndio ambao wametutuma na ndio lengo la Serikali kuwaangalia wananchi hawa, lakini mimi nimesikitishwa sana na majibu ya Serikali yamekuwa mepesi, kwa sababu wananchi hawa wanavyokuwa wanazuiliwa kuvua katika muda fulani wanaambiwa waende wakavue katika muda ambao hawana uwezo wa kwenda kule bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kwamba sisi kama Serikali sijui tunaliangalia vipi jambo hili na hapa tunazungumzia watu wasiopungua 250,000. Nilikuwa naomba tu nipate maelezo ya Serikali ya ziada kwenye hili.

**MWENYEKITI:** Hawa ni *lobster* au ni?

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hao.

**MWENYEKITI:** *Lobster* eeh, okay. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, misimu ya uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kumjibu ndugu yangu, jirani yangu, Mheshimiwa Twaha Mpambenwe, Mbunge wa Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwanza ninaomba kwa heshima kubwa na taadhima nimuweke sawa, anazungumzia kambakoche. Kambakoche sisi hatuzuwii, hakuna mahali anazuiliwa mtu, nadhani anaowazungumzia kwa maana ya misimu ni kambamiti ambao ni *prawns* ambao tumeweza misimu kuanzia upande wa Kaskazini kwa maana maingilio...

**MWENYEKITI:** Ambao wanapatikana pale kwenye mdomo wa Mto Rufiji?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam. Kwa kawaida ikolojia ya hawa kambamiti inataka maingilio, wakati maji baridi na maji chumvi yanakutana na ile mikoko aliyokuwa akiizungumza Mheshimiwa Amour nadhani, ndio mahali hapo wanakozalliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili analolisema Mheshimiwa Mpembewenwe juu ya *season*, wakati gani wavue ni kweli; kwa kule kwetu, kuanzia kwanza Kaskazini kwa maana ya Mto Pangani kuja Mto Rufiji kwa maana ya Mkuranga na *Kibiti Delta* na kwa upande wa Mto Ruvuma kwa maana ya Mtwara pamekuwa na malalmiko ya muda na kwa nini ni malalamiko ya muda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi, wale kamba wanaanza kuzaliana kuanzia mwezi Septemba mpaka Disemba, wanazaliana kwa upande wa *zone* ya Kibiti - Mkuranga na wanapozaliana ni huku tuliko sisi wananchi huku, vijijini huku, kwa maana ya huku pwani/mwambao. Ikifika mwezi Januari mpaka Machi wanapata makuzi yao; makuzi nayo vilevile yanafanyikia huku huku pwani huku tuliko sisi wananchi, yaani kwa maana katika mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika mwezi Aprili mpaka Julai wanakuwa wameshapata nguvu wanaondoka huku wanakwenda na maji mengi ambako sisi wananchi hatupo kule maji mengi na sisi tunavua kwa kutumia makasia, hatuna uwezo wa kufika kule maji mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mgongano ulioko hapa mimi mvuvi wa Mkuranga, Shungubweni, Kisiju, Mdimni, Kifumangao na jirani yangu Mbunge wa Kibiti kwa maana ya kuanzia pale Mkenda, Nyamisati, Mbwera mpaka unafika kule mpakani na mwenzetu yule Bwana Kasinge panaitwa Marendego, muda huo wavuvi wetu hawana uwezo wa kwenda kule mbele. Nimeshawahi kuzungumza jambo hili na wataalamu wetu wa uvuvi, wataalamu hawataki kujiongeza kwa sababu hii ni fursa kubwa ya kuhakikisha kwamba tunazalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie ni *under utilization* ya ile resource pale, lile eneo ni kubwa, tuna uwezo wa kuzalisha pale tukalisha kamba dunia nzima. Hivi leo mazao ya bahari katika mchango huu unaoambiwa tani 350,000 *only 15%* ndio inayotoka baharini, *only 15%*, hiyo iliyobaki yote inatoka Ziwa Victoria, ndio ukweli wenyewe, lakini ukichukua ukaingiza pale utafiti na hatimaye ukafanya uzalishaji zaidi tunapata *foreign currency* kwa sababu kamba wenyewe sisi wenyewe hapa tunakula kidogo sana kwa kiasi kikubwa sana tuna *export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Mpembenwe na Wabunge wote tumeshatoa maagizo Wizarani mimi na Mheshimiwa Waziri, ya kwamba *TAFI/RI* wakatie kambi pale watoke na utafiti na programu kubwa itakayokwenda kujibu hili jambo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kwamba tunafanya *zoning* halafu kuna wakati watu wavue, kuna wakati hawavui, anatunza yeye rasilimali, *mind you* mtu huyu wa Mkuranga na Kibiti anatunza yeye rasilimali wakati inazaliana, wakati inakua, muda wa kuvua unafika anaiona inaondoka inakwenda kule ambako yeye hawezi, Wizara inataoa kibali aende akavue mtu mwenye meli kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia hilo jambo Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan

haiwezi kukubali. Tunataka tuzalishe zaidi, wananchi wapate zaidi na Taifa letu lipate zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa muda wetu sasa, Katibu ni *guillotine* sasa.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**FUNGU 99 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (MIFUGO)**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh. 2,819,246,570
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 867,696,609
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 1,075,738,000
Kifungu 1004 – <i>Research, Training and Extension Unit</i> .....	Sh. 8,536,949,808
Kifungu 1005 – <i>Information, Education and Communication Unit</i> .....	Sh. 293,016,000
Kifungu 1007 – <i>Internal Audit</i> .....	Sh. 215,675,400
Kifungu 1008 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 395,634,601
Kifungu 1009 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 156,462,000
Kifungu 1010 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 229,566,000
Kifungu 1011 – <i>Environmental Management Unit</i> .....	Sh. 114,662,500
Kifungu 7001 – <i>Veterinary Services</i> .....	Sh. 8,334,083,396
Kifungu 7005 – <i>Veterinary Council of Tanzania</i> ..	Sh. 314,512,000
Kifungu 8001 – <i>Livestock Production and Marketing</i> .....	Sh. 6,297,002,116
Kifungu 8002 – <i>Grazing Land and Animal Feed Resources Development</i> .....	Sh. 1,145,016,000
Kifungu 8003 – <i>Animal Breeders Rights Unit</i> .....	Sh. 177,948,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **FUNGU 64 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (UVUVI)**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management Division*.....Sh. 2,094,704,000  
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*....Sh. 999,126,380  
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*....Sh. 847,725,860  
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 336,326,410  
Kifungu 1005 – *Legal Unit*.....Sh. 344,744,940  
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 469,916,410  
Kifungu 1007 – *ICT Unit*.....Sh. 271,826,000  
Kifungu 1008 – *Environmental Management Unit*.....Sh. 116,920,000  
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*.....Sh. 7,191,851,882  
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*.....Sh. 1,805,700,170  
Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research, Training Extension Services*....Sh. 6,815,377,948

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **KITABU CHA NNE**

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

## **FUNGU 99 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (MIFUGO)**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management Division*.....Sh. 0  
Kifungu 1002 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 400,000,000  
Kifungu 1004 – *Research, Training and Extension Unit*.....Sh. 3,000,000,000  
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*.....Sh. 5,433,441,000  
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing*.....Sh. 5,762,200,000  
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development*.....Sh. 2,276,100,000  
*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 64 – WIZARAYA MIFUGO NA UVUVI (UVUVI)

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*....Sh. 1,378,649,666

Kifungu 9001 – *Fisheries Development*

*Division*.....Sh. 76,589,887,249

Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*...Sh. 18,000,000,000

Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research,  
Training Extension Services*....Sh. 3,175,829,085

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba  
Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae.

Mheshimiwa Waziri, tupatia Taarifa.

### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Namba 123(3)(a) na (b), naomba kutoa Taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katika hatua hii sasa ili tuweze kuifanyia haki, kuitendea haki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, ninaomba niende

kuwahoji ili mkubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, wote kabisa wameafiki, Bunge limepitisha bajeti hii kwa kauli moja. (*Makofi*)

Kwa kweli ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na timu nzima, Wenyeviti wa Bodhi mliopo ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*)

Tunajua mnafanya kazi katika mazingira magumu kwa sababu rasilimali hizi za mifugo na uvuvi zina changamoto nyingi katika nchi yetu, yaani nyingi sana. Namna hata ya kuwafikia wafugaji na kuwasaidia ni ngumu, hata wavuvi; ukitembelea kambi za wavuvi wana maisha duni sana kule pwani, angalau wavuvi wa Ziwa Victoria kidogo afadhali, lakini wavuvi wa pwani kule yani wana maisha duni kweli.

Kwa hiyo, mna kazi kubwa kabisa katika kupambana na umasikini mojawapo ni umasikini wa wavuvi na hasa wa pwani.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri, tunaamini kabisa mtaenda kuchapa kazi na sisi kama tulivyosema kupitia Kamati yetu ya Bajeti tutajitahidi kuwakumbusha Wizara ya Fedha, kuwasukuma kidogo ili hili ambalo tumelipitisha leo kwa kweli kwa kiasi kikubwa liweze kuwa *realized*.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri tuko pamoja nanyi, mkayaangalie haya mambo, muwasaidie wafugaji, yapo mengine ni madogo madogo, lakini muhimu.. (*Makofi*)

Kwa mfano, unajua mfugaji hawezi kuuza mnadani bila dalali na dalali ni mtu anatoka tu nyumbani kwake anaenda pale mnadani, lakini wewe huwezi kumfikia mnunuzi, wewe mwenye ng'ombe, lazima umpe yeye halafu yeye amuuzie mnunuzi. Kwa hiyo, anadamka asubuhi ng'ombe wa shilingi 700,000 yeye anakwambia nitakupa shilingi 500,000 hapo hapo, halafu anamchukua anamuuzia mtu shilingi 700,000, yeye pale pale anatengeneza shilingi 200,000 kwa ng'ombe mmoja tu, mpaka jioni anauza ng'ombe wangapi? Sasa hawa madalali-dalali hawa wa katikati hawa hivyo hawawezi kuondoka? (*Makofi*)

Hata kwenye kilimo hivyo hivyo, madalali katikati yaani hivi jamani hiki kitu dalali, kuna wakati tulitunga sijui utaratibu wa madalali hapa, lakini ni utaratibu fulani ambao hebu tuutazame. Wakati ule wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Nyerere, Serikali ile ya Awamu ya Kwanza walileta mizani nchi nzima, Mheshimiwa Lukvi na wenzangu mimi nafikiri tunaweza tukakumbuka. Palikuwa na kampuni ilianzishwa kampuni enzi hizo, Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania, ilikuwa inaitwa KABIMITA. Vijana wengi mambo haya ya historia, hamuwezi kukumbuka, hamuwezi kujua maana hamkuyakuta, Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania – KABIMITA, iliweka mizani maeneo mengi sana ya Tanzania, mizani ya chuma. Ilikuwa ukileta mnadani ng'ombe anapita pale kwenye mzani anachukuliwa kilo zake.

Kwa hiyo, ng'ombe alikuwa anauzwa kwa *live weight*, ambalo lilikuwa ni jambo jema kweli; ilipigwa vita ile mizani wakaaminishwa wafugaji kwamba wanaibiwa, ikarudi ile ya wale, hawa watu wa .... *top*, mizani yote ikaharibika ile. (*Kicheko*)

Sasa nadhani ni vizuri tukarudi kwenye mizani ili watu wauze kitu kwa bei ambayo ni halisi, bei ambayo ina usawa kwenye minada mbalimbali ya nchi yetu tuangalie uwezekano, kama iliwezekana miaka ya 1970, inawezekana leo. Na huenda leo tukawa na mizani bora zaidi kuliko ile ya zamani. Tuangalie sana hili, litatusaidia sana kuwapatia haki wafugaji wetu. (*Makofi*)

Tunashukuru mmesema habari ya pikipiki; muangalie tu na wale wa kilimo nao wanunuua pikipiki pia kwa sababu baadhi ya maeneo yetu Afisa Mifugo ndio Afisa Kilimo huyo huyo sasa msije kukuta afisa wa Serikali akapata pikipiki ya mifugo, akapata pikipiki ya kilimo mtu huyo huyo mmoja, itakuwa tena ni *duplication* ya mambo, nawa-caution tu. (*Makofi*)

Halafu lile la mwisho kama tulivyosema tutakutana mwakani, la *NARCO*, nafikiri mtakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi. Kwa kweli, ziko *paper* nyingi sana wala hamuhitaji kwenda mbali. Ni kuangalia tu *reference* ziko nyngi *study* mnazo wenyewe. Hata enzi ya Mheshimiwa David Mathayo alipokuwa Waziri, *papers, papers* hata nani nyuma, *papers, papers* na zilikuwa zinaenda mpaka karibu na Baraza la Mawaziri halafu zinataka kwenda halafu zinarudi, kwa hiyo, *references* mnazo za kutosha na haya ni mashamba tunayoyaongelea na mashamba haya yote yalitaifishwa mwaka 1967, yalikuwa ni mashamba ya mikonge yalitaifishwa, leo yako wapi? Serikali bado inamiliiki mashamba ya mikonge? Yalikuwepo mashamba ya kahawa, Serikali bado inamiliiki? Yalikuwepo mashamba ya chai, mashamba ya nini, yaliyobakia ni mashamba ya ng'ombe, mengine yote yamekwenda *private* sasa unafikiri haya yata-survive?

Ndio maana nasema haina haja ya *study*, ni kwenda tu kutekeleza kwa sababu inaonekana wazi kabisa hii habari ya mashamba ya kumilikiwa na Serikali. Badala ya Serikali kukusanya kodi ya ardhi, kodi ya nini, tunakuwa tunajikosesha mapato sisi wenyewe kitu ambacho hakina tija. Lengo ni Watanzania wafaidike, tuweze kusonga mbele, wala lengo sio jina la kampuni kwamba lina matatizo au halipendezi, hapana. (*Kicheko*)

Basi baada ya maelezo hayo, aah, kuna watu wa kuwatambulisha; kuna ugeni wa Mheshimiwa Waziri, Meneja Mkuu wa Benki ya Kilimo, *TIDB*, Japhest Justin, sasa amekuja. (*Makofi*)

Tulikutafuta asubuhi hatukuwa tumekupata Meneja Mkoo, lakini tunashukuru sasa umekuja. Jamani huyu ndiyo Meneja Mkoo, hoja kubwa ni kwamba hujafungua tawi Dodoma angalau ili wakulima kutoka sehemu mbalimbali wawze kufika, Dar es Salaam ni kushoto sana. Kwa hiyo, anzia Dodoma badaye utaenda Kanda ya Ziwa, badaye Mbeya, baadaye Arusha, badaye mpaka Kongwa kule nako. (*Kicheko*)

Ahsante sana, lakini pia amefuatana na Meneja wake anaitwa Ndugu Mwanakatwe, karibu sana Ndugu Mwanakatwe, karibu sana. (*Makofi*)

Kipekee ninaye mgeni ambaye ni binti wa Katibu Mkoo - Mifugo, Profesa Ole Gabriel. Ni Neema Elisante, Neema? (*Makofi*)

Ahsante sana kwa kufika. Sisi Wagogo tuna msemo kwa kigogo, lakini sitasema kwa kigogo, tafsiri yake, *of course* hata kwenye Kiswahili upo kwamba, panya hakosi mkia. Kwa hiyo, Profesa Katibu Mkoo ni mchunga ng'ombe ni vizuri na wewe ukawa mfugaji pia, Neema. Ufuate nyayo uwe mfugaji pia, ahsante sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge tulikubaliana kwamba saa 07:00 mchana tutamaliza shughuli zetu na sasa ni saa 07:00 mchana, wakati mwingine muwe mnatupigia makofi kwa uendeshaji wa mambo kwa uhakika. (*Kicheko/Makofi*)

Nawatachia kila la heri, nawatachia *weekend* njema.

Basi, naomba tuahirishe shughuli zetu hadi siku ya Jumatatu ijayo, saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 31 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi*)